# Nipashe

Ijumaa Februari 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580148

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Waziri Mkuu amjibu Mbowe kuhusu tume huru uchaguzi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Saa 5 dakika 30 za Membe kikaangoni

**ASEMA** ulikuwa mjadala mzuri, adai amefurahi kutoa maoni yake kuimarisha chama...*Endelea ukurasa wa 2*




Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Bernard Membe (kushoto), akiwasili katika Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuhojiwa na Kamati ya Maadili ya chama hicho. Picha ndogo: Membe, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kumaliza mahojiano na chama. **PICHA: PETER MKWAVILA/ IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**ZITTO AHOFU KUREJEA NCHINI**
MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), ameeleza wasiwasi wake wa kukamatwa, kufunguliwa mashtaka na kufungwa pindi atakaporejea nchini...

**UKURASA WA 3**

**SERIKALI YAKODI NDEGE KUKABILIANA NA NZIGE**
SERIKALI imekodi ndege moja kutoka Shirika la DLCO kwa ajili ya tahadhari ya nzige wa jangwani na wekundu...


## WAAJIRI WABURUZWA MAHAKAMANI KISA NSSF

UKURASA 11

# JPM awashukia wapelelezi utitiri mahabusi magerezani

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** SIMBA YAIPIGIA HESABU KALI JKT UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Saa tano dakika 30 Membe kikaangoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika serikali ya awamu ya nne, Bernard Membe, jana alihojiwa kwa zaidi ya saa tano na Kamati ya maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) huku mwenyewe akifunguka mazito yaliyojiri katika kikao hicho. Membe ambaye ni mmoja wa makada walioitwa kuhojiwa na kamati hiyo kwa madai ya kukiuka kanuni za chama, akiingia kuhojiwa saa 3:10 asubuhi na kutoka saa 8:40 mchana.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kuhojiwa katika kikao kilichofanyika kwenye makao makuu ya CCM jijini hapa, Membe akiwa ndani ya gari lake, alisema anashukuru kwa kupata fursa hiyo ambayo imemfanya kuwa mwenye furaha kubwa.

Aidha Membe, alisema katika kikao hicho kilichotumia zaidi ya saa tano, amepata nafasi nzuri ya kufafanua mambo ambayo chama chake kilihitaji kujua kutoka kwake.

"Lakini pia nimepata nafasi ya kushiriki mjadala mkubwa unaohusu mambo mbalimbali ya kukijenga chama changu pamoja na kutoa mawazo yangu katika mambo mbalimbali. Niseme tu kwa ujumla safari hii ya Dodoma imekuwa ya mafanikio makubwa sana," alisema Membe.

"Kwa leo (jana) niseme hayo tu kuwa nina furaha sana. Mimi na mke wangu leo (jana) tutakwenda kula chakula katika hoteli nzuri sana ambayo bado jina lake halijafahamika na baadaye safari ya Dar es Saalam ianze. Lakini kwa ujumla safari hii ya Dodoma imekuwa na manufaa makubwa sana," aliongeza. Membe ambaye alikuwa Mbunge wa Mtama kwa miaka 15, aliwasili Makao Makuu ya CCM majira ya saa 9.10 asubuhi akiwa katika gari lake aina ya Range Rover rangi nyeusi lenye namba za usajili T 748 CNV.

Baada ya kuwasili akiwa na wasaidizi wake, alipokewa na maofisa watano wa CCM ambao walimwongoza kuingia ndani ya ofisi. Pia katika eneo hilo ulinzi uliimarishwa na mara kwa kwanza walionekana walinzi kutoka kampuni ya ulinzi ya Suma JKT waliokuwa wakilinda geti la kuingilia na kutokea.

Katika jengo hilo, mara nyingi wamekuwa wakilinda walinzi wa kawaida lakini jana walionekana Suma JKT huku waandishi wa habari wakikataliwa kuingia hata ndani ya geti.

Mbali na Membe, wengine wanaotakiwa kuhojiwa na kamati hiyo ni makatibu wakuu wastaafu wa chama hicho tawala, Abdulrahman Kinana na Yussuf Makamba.

Vigogo hao, walikuwa mjadala hivi karibuni baada ya sauti za baadhi yao kusambaa mitandaoni wakizungumzia kupasuka kwa CCM.



Rais Dk. John Magufuli akigana na Majaji baada ya kuhutubia katika maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Magufuli awashukia wapelelezi

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema wapelelezi wa kesi na wasimamizi wa sheria nchini wanawaumiza mahabusi wengi kutokana na kuchelewa kukamilisha kazi kwa wakati.

Amesema wapelelezi wa kesi ni chanzo cha watu kuwekwa kwenye magereza bila hatia yoyote, huku wengine wakiwekwa mahabusi kutokana na shinikizo la matajiri.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya sheria iliyokuwa na kaulimbiu, Uwekezaji na biashara: Wajibu wa Mahakama na wadau kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

Kutokana na hali hiyo, Rais Magufuli aliwataka viongozi wa dini nchini kuwaombea wapelelezi wanaofanya vitendo hivyo wapate laana.

Alisema idadi ya wafungwa waliopo katika magereza nchini ni ndogo kulinganisha na mahabusi waliopo, ambayo alitaja wafungwa ni 13,455 wakati mahabusi ni 17,632.

Alisema idadi ya mahabusi walioachiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) baada ya kubainika kubambikiziwa kesi ni 1,422.

"Lakini niwaombe ndugu zangu wapelelezi, ufalme wa mbinguni utakuwa shida kwenu msipotubu kwa Mungu, kwa sababu roho za wasiokuwa na hatia zinaangamia kule, mnawapa shida sana mahakimu na majaji na roho za watu, ninawaambia ukweli mtaenda kuyalipa badilikeni," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Mimi nimeshuhudia ukienda kwenye magereza yetu watu wanalia na wengine ni kesi za kusingiziwa, wapo wengine wamewekwa kule ndani kwa sababu ya matajiri kwamba ni akukomeshe utaenda kwanza mahabusu," alisema Rais Magufuli.

"Roho za watu wasiokuwa na hatia zinaangamia kule gerezani na wala msiwasingizie majaji na mahakimu kwa sababu hamuwapelekei na saa nyingine hata kupelekwa mahakani ni lazima uhonge ili kesi yako isomwe, mnawapa shida mahakimu na majaji ninawaambia ukweli mtakwenda kuyalipa badilikeni."

Rais Magufuli alisema idadi ya wafungwa waliosamehewa katika kipindi cha miaka minne ni 38,801 na baadhi yao walikuwa na kifungo cha maisha.

Alisema kwa sasa serikali iko katika mazungumzo ya kuwarejesha wafungwa raia wa kigeni wakiwamo kutoka Ethiopia 1,451 ili warudi kwao.

INAENDELEA UK. 8

# Zitto ahofu kurejea nchini

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), ameeleza wasiwasi wake wa kukamatwa, kufunguliwa mashtaka na kufungwa pindi atakaporejea nchini.

Hofu hiyo inatokana na kile alichokiita mfululizo wa vitisho vilivyotolewa na viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hofu hiyo ya Zitto imeibuka baada ya Kiongozi Mkuu huyo ACT Wazalendo kuandika barua kwa Benki ya Dunia (WB) kuitaka kusitisha mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 kwa Tanzania kutokana na kile alichodai kuna ubaguzi katika elimu kwa watoto wa kike waliopata ujauzito wakiwa shuleni.

Zitto alieleza hofu yake hiyo jana, akidai kuwa analichukulia kwa uzito suala hilo kwa kuwa upo mfano wa aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu (Chadema), kupigwa risasi mjini Dodoma na hadi sasa ameshindwa kurejea nchini kutokana na hofu ya usalama wake.

"Ninachukulia vitisho hivi kwa uzito kwa sababu tuna mfano wa mwenzetu Lissu, lakini usije kushangaa ukisikia nimekamatwa na kufungwa nitakaporejea Tanzania kwa sababu sasa hivi kesi za utakatishaji fedha zinatumika kuwanyamazisha wakosoaji kwa sababu mashtaka yake hayana dhamana," alisema.

Wiki iliyopita, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Adelardus Kilangi, kuchunguza kitendo cha Zitto kuiandikia barua WB kuzuia mkopo huo ili kuona kama kuna jinai au la na kumchukulia hatua mbunge huyo kufuatia hoja binafsi iliyowasilishwa bungeni na Mbunge wa Siha, DK. Godwin Mollel (CCM), kutaka kuchunguzwa kwa jambo hilo.

Zitto kwa sasa yuko Amerika ya Kaskazini kwa shughuli ambazo chama chake hakijaziweka wazi kwa umma.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisikiliza swali kutoka kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, bungeni, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Serikali yaijibu hoja ya Mbowe

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema hawajawahi kumwona Rais akiingilia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wala chama cha siasa kikiingilia, kwa kuwa tume hiyo iko huru na inafanya kazi yake kama ambavyo imetakiwa kwa mujibu wa katiba ya nchi.

Majaliwa alitoa kauli hiyo bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu swali la nyongeza la Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe katika kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu'.

"Suala la tume hii kuonwa kwamba si huru ni mtizamo wa mtu, lakini katiba na utendaji wake iko huru na pale ambako kunaonekana kuna shida, basi kwa utaratibu ule paelezwe kwamba hapa kuna shida.

"Lakini, hatujawahi kuona Rais akiingilia, chama cha siasa kikiingilia, ile tume iko huru na inafanya kazi yake kama ambavyo imetakiwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuuri ya Muungano wa Tanzania.

"Ukiwa na jambo lolote lile, unao uhuru wa kubadilishana mawazo ili tuone wapi tunaweza kusaidia kufanya jambo hilo liweze kwenda sahihi," alisema.

Kuhusu hoja kwamba vyama vya siasa vya upinzani vimezuiwa kwa miaka minne sasa kufanya shughuli za uenezi, Waziri Mkuu alisema: "Mbowe ni kiongozi, tunazungumza, tunabadilishana mawazo, lakini muhimu zaidi Watanzania wanahitaji maendeleo na kwa maana hiyo kunapowekwa utaratibu wa namna ya kuwafikia wananchi na kupata maendeleo, jambo hilo si la chama kimoja, ni la nchi nzima.

"Sote tunabadilishana mawazo, tunalenga kulifanya taifa hili liwe na usalama, liwe tulivu ili shughuli zetu ziweze kwenda, lakini muhimu zaidi Watanzania wanahitaji maendeleo.

"Hakuna mbunge wala diwani kwenye eneo lake amezuiwa, asifanye siasa na watu wake, kunaweza kuwa labda kuna tatizo mahali fulani, lakini kwa utaratibu ule tunaozungumza, tunakutana tunazungumza wapi kuna shida.

"Shida kama ziko kwenye ngazi ndogo ndogo huko, ni suala la kuzungumza kwenye eneo hilo na pale ambako kuna shida ya namna hiyo tuendelee kuwasiliana," alisema.

Katika swali la msingi, Mbowe wakati anajenga hoja yake alisema miaka minne sasa tangu serikali iweke zuio kwa vyama vya siasa kufanya wajibu wake kwa mujibu wa katiba na sheria ya nchi; na mpaka anazungumza jana, ni siku ya 262 ambazo zimebaki kufika Oktoba 25, siku

INAENDELEA UK. 8

## Serikali yakodi ndege kukabiliana na nzige

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imekodi ndege moja kutoka Shirika la DLCO kwa ajili ya tahadhari ya nzige wa jangwani na wekundu, itakayogharimu Dola za Marekani 2,000 kwa saa inapokuwa angani.

Pia, imeagiza Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI) kuhakikisha inafuatilia wauzaji mbegu feki kwa wakulima ili wachukuliwe hatua kali na kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Ddooma kuhusiana na uzalishaji wa pembejeo nchini.

Alisema serikali imechukua tahadhari zote kuhusu nzige na ndege hiyo imekodiwa ili kuwa tayari kukabiliana nao iwapo wataingia nchini.

"Kwa sasa nzige wamebadilisha uelekeo wa kuja nchini, lakini serikali imekodi ndege hii kama moja ya hatua za kujiimarisha endapo kundi la nzige ambao walionekana nchi jirani, litaingia nchini," alisema.

Aliwataka wananchi katika mikoa ambayo wanaona kuna viashiria vya nzige hao, kutoa

INAENDELEA UK. 8

# Tanzania yatoa somo AU haki za binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeieleza Tume ya Haki za Binadamu na Watu wa Afrika ya Umoja wa Afrika (AU) kuwa kuna tofauti kati ya makosa ya kitaalamu na makosa ya jinai.

Kutokana na tofauti hiyo, imesema sheria inapochukua mkondo wake isitafsirike kuwa ni kukiuka haki za binadamu kwa kuwa Tanzania hakuna raia yeyote aliye juu ya sheria pale anapotenda kosa la jinai.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, ameyasema hayo katika majadiliano ya taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu katika mkutano wa 33 wa Baraza la Mawaziri wa Umoja wa Afrika unaofanyika Addis Ababa, Ethiopia.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema Waziri Kabudi alibainisha Tanzania inaheshimu haki za binadamu, uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari kama ilivyo katika Katiba yake.

Prof. Kabudi aliongeza kuwa Tanzania hakuna raia wake aliye juu ya sheria na kwamba pale mwanataaluma anapofanya makosa ya kijinai, huchukuliwa hatua za kisheria kama ilivyo kwa wananchi wengine kwa kufikishwa katika vyombo rasmi vya kutoa haki kama mahakama ambayo iko huru kufanya uamuzi wake.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Kabudi alisema kuna baadhi ya Watanzania ambao wamekuwa wakitumia taaluma zao vibaya, hivyo kuwafanya kutenda makosa ya jinai na kufikishwa mbele ya sheria.

Watu hao, alisema mashauri yao yako mahakamani na vyombo vingine vya sheria na ana imani mahakama na vyombo hivyo vitatoa haki dhidi ya mashtaka yanayowakabili baada ya kutoa utetezi wao.

Hivi karibuni kumekuwapo na mjadala kutoka kwa baadhi ya wanaharakati, wanasiasa na jumuiya za kimataifa zikiishutumu Tanzania kukiuka haki za binadamu jambo ambalo serikali imeiambia AU na jumuiya za kimataifa kuwa si kweli na kwamba Tanzania haiheshimu haki za binadamu na uhuru wa kujieleza.

Mkutano wa kawaida wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika unafanyika Addis Ababa, ukitanguliwa na mikutano mbalimbali ya Baraza la Mawaziri. Mkutano huo unatarajiwa kumalizika Februari 10, mwaka huu.


**KUMBUKUMBU**



CAROLINE MONGERE MUSIKA

LEO NI MWAKA MMOJA UMETIMIA TANGU MPENDWA WETU ALIPO FARIKI DUNIA TAREHE 7.2.2019, KWA AJALI YA GARI MKOANI MOROGORO.

TUNAENDELEA KUMKUMBUKA MPENDWA WETU KWA UTU NA UPENDO ALIO UISHI KATIKA KIPINDI CHOTE CHA UHAI WAKE.

ATAENDELEA KUKUMBUKWA NA BABA, MUME, WATOTO, KAKA, DADA, NDUGU NA MARAFIKI WOTE.

**JINA LA BWANA LIHIMIDIWE NA KUTUKUZWA MILELE (AYUBU 1:21) AMINA.**

# PM amaliza kilio cha Mbunge Sugu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amemaliza rasmi malalamiko ya Mbunge wa Mbeya Mjini (Chadema), Joseph Mbilinyi maarufu kama 'Sugu' kuhusu madai ya kuzuiwa na polisi kufanya mikutano yake ya siasa jimboni na wapigakura wake.

Akizungumza jana bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu swali la Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB), Freeman Mbowe, wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa hapo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema, hivi sasa Sugu yuko sawa na ameungana na Mkuu wa mkoa pamoja na Kamanda wa Polisi mkoani humo.

"Wiki iliyopita Sugu alieleza kule Mbeya anazuiwa na OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), na mimi nilimwita hapa tumezungumza, Mkuu wa mkoa ameungana naye, Mkuu wa Polisi mkoa ameungana naye."

"Shida kama ziko kwenye ngazi ndogo ndogo huko, ni suala la kuzungumza kwenye eneo hilo na pale ambako kuna shida ya namna hiyo tuendelee kuwasiliana."

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, hakuna Mbunge wala Diwani kwenye eneo lake, amezuiwa asifanye siasa na watu wake, isipokuwa kunaweza kuwa labda na tatizo mahali fulani, lakini kwa utaratibu ule tunaozungumza tunakutana tunazungumza wapi kuna shida.

Katika swali la msingi, Mbowe alimuuliza Waziri Mkuu kwamba ni miaka minne sasa tangu serikali imeweka zuio kwa vyama vya siasa kufanya wajibu wake kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi, na mpaka anavyozungumza jana ni siku 262 zimebaki kufika tarehe 25 Oktoba, siku ambayo nchi itafanya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani.

Kwa Busara zake binafsi katika serikali ambayo yeye ni kiongozi mwandamizi, anafikiri ni lini wataruhusu vyama vya siasa vifanye wajibu wake wa uenezi kujiandaa na uchaguzi mkuu?



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakichimba mchanga wa kujengea kwenye Mto Msimbazi, eneo la Kigogo, jana, kwa ajili ya kwenda kuuza ili kujipatia riziki. **PICHA: JOHN BADI**

# TRA yatakiwa kuwekeza teknolojia ya kisasa

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetakiwa kuwekeza kwenye teknolojia ya kisasa kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki inayosaidia ukuzaji wa uchumi kupitia ushuru wa forodha unaotozwa katika eneo hilo.

Katibu Mkuu wa Shirika la Forodha Duniani (WCO), Dk. Kunio Mikuriya, aliyasema hayo jana alipotembelea TRA ikiwa ni sehemu ya ziara ya kikazi nchini.

"Ili kusimamia ushuru wa forodha ipasavyo, suala la teknolojia halikwepeki, hivyo ni muhimu TRA ijikite zaidi katika kuendelea kuwekeza kwenye mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa na watumishi wenye uwezo wa kuendesha mifumo hiyo," alisema Dk. Mikuriya. Dk. Mikuriya alisema kwenye mazungumzo baina yake na Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, wamezungumzia umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika kudhibiti na kusimamia ushuru wa forodha kwenye Bandari ya Dar es Salaam na maeneo mbalimbali nchini.

Naye, Dk. Mhede alisema, ziara ya Katibu Mkuu huyo imelenga kuimarisha uhusiano baina ya nchi wanachama wa WCO na alitokea nchini Kenya kwa ajili ya kazi hiyo pia.

"Tanzania ni mwanachama wa WCO na kuna ushirikiano ambao tunafanya kwa pamoja kuhakikisha eneo la forodha linatekeleza majukumu yake ili kuhakikisha kuna usalama wa bidhaa kwenye eneo la biashara," alisema Dk. Mhede.

Alisema Tanzania ni kitovu cha biashara kwa kuwa inahudumia nchi zote ambazo hazina bandari kama vile Zambia, Malawi, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ambao wote wanatumia Bandari ya Dar es Salaam, hivyo ni muhimu kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa katika kusimamia masuala yote ya kiforodha.

Katibu Mkuu wa WCO, Dk. Kunio Mikuriya baada ya kutembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania alielekea jijini Dodoma kwa lengo la kukutana na baadhi ya watunga sera kwa ajili ya kuimarisha uhusiano uliopo.

# Mwisho kusajili huduma ndogo za fedha Oktoba

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATOA huduma ndogo za kifedha nchini wametakiwa kukata leseni zao au kusajiliwa kufanya biashara hiyo kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia madaraja husika.

Imeelezwa kuwa ifikapo Oktoba 31 mwaka huu, itakuwa ndiyo mwisho kwa mtoa huduma kuruhusiwa kuendelea na shughuli hiyo bila kukamilisha taratibu.

Utekelezaji wa agizo hilo utaanza rasmi baada ya kutungwa sheria mahususi ya kusimamia na kuendeleza sekta ya huduma ndogo ya fedha ili kuondoa vikwazo vya kisheria vilivyokuwapo na kuchangia kuathiri usimamizi, udhibiti na ustawi wa sekta ndogo ya fedha.

Tayari serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeandaa kanuni mahususi na kanuni za jumla za utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, iliyoanza rasmi kutumika Novemba mwaka jana.

Katibu Mkuu wa Hazina, Dotto James, aliyasema hayo jana mjini Morogoro katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja.

Alisema vikwazo vilivyoathiri usimamizi, udhibiti na ustawi wa sekta ndogo ya fedha ni pamoja na taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa mikopo kwa wananchi kwa vigezo na masharti magumu, hivyo kusababisha madhara kwa wananchi, ikiwamo viwango vikubwa vya riba na tozo, kukosekana kwa uwazi wa masharti ya mikataba na mikopo.

Alisema vikwazo vingine ni utoaji holela wa mikopo uliosababisha malimbikizo ya madeni kwa wateja, utaratibu usiofaa wa ukusanyaji wa madeni unaosababisha wananchi kupoteza mali zao na kujitokeza kwa baadhi ya wananchi wasio waaminifu na wanaotumia mwanya wa kutokuwapo kwa sheria mahsusi, kutoa huduma ndogo za kifedha.

"Mengine yaliyoathiri ni kuwapo kwa baadhi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zisizotoa gawio au faida kwa wanachama au wateja wanaoweka fedha kati ya asilimia 25 hadi 30 kama dhamana ya mikopo na ukosefu wa takwimu au taarifa sahihi za uendeshaji wa taasisi za watoa huduma ndogo za fedha pamoja na kukosekana takwimu na taarifa tajwa na kusababisha serikali kutojua mchango wa sekta ndogo ya

INAENDELEA UK. 8

# Sweden kuendelea kusaidia Tasaf

**Na Elizabeth Zaya,** KIBAHA

SELIKALI ya Sweden imesema itaendelea kusaidia utekelezaji wa Mpango wa tatu (Tasaf III) awamu ya pili wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), unaotarajia kuanza hivi karibuni

Kauli hiyo imekuja baada ya mpango huo wa kunusuru kaya maskini (Tasaf III) awamu ya kwanza kumalizika na kuanza maandalizi ya awamu ya pili ya mpango huo.

Mwakilishi kutoka Ubalozi wa Sweden nchini, True Schedvin, alitoa kauli hiyo jana katika Kijiji cha Vikuge, alipofanya ziara kwaajili ya kushuhudia utekelezaji wa mpango huo, kujifunza, na kusikiliza changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake.

"Tumejionea na kujifunza mambo mengi katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini wa Tasaf III awamu ya kwanza unaomalizika, tumeona bado kuna uhitaji na tutaendelea kusapoti katika miaka mingine minne inayokuja," alisema Schedvin.

Mratibu wa Tasaf Halmashauri ya Kibaha, Sijaona Muhunzi, alisema vijiji 45 vinanufaika na mpango huo.

Alisema miradi iliyotekelezwa katika mpango unaomalizika ni pamoja na uhawilishaji fedha kwa kaya maskini, ajira za muda kwa walengwa, kuweka akiba na kukuza uchumi wa kipato kwa kaya na miradi ya ujenzi wa miundombinu.

Muhunzi alisema mpango umekuwa na mafanikio makubwa na umesaidia kuboresha maisha ya walengwa.

"Tunashukuru sana kwa sababu mpango umekuwa wa mafanikio makubwa, kutokana na malipo wanayopata katika ruzuku ya fedha, ajira za muda na miradi ya kujiongezea kipato kama ufugaji, kilimo na vikundi wanavyoanzisha, hali za maisha yao zimeboreka sana," alisema Muhunzi.

"Wapo ambao wametoka katika maisha ya kuishi katika nyumba za udongo na sasa wamejenga za block (matofali) na kuezeka na bati. Na pia wanapata hudumaza afya."

Mmoja wa walengwa wa mpango huo kutoka katika kijiji hicho cha Vikuge, Mgomba Selemani, alisema kabla ya kuingizwa katika mpango huo alikuwa na maisha magumu, lakini kwa sasa umemsaidia na amemudu kulea watoto wake sita, kuanzisha miradi mbalimbali na kumudu kujenga nyumba ya kisasa.

Mtendaji wa kijiji cha Vikuge, Maximillian Mutobu, alisema kijiji hicho kina walengwa 142 na kupitia mpango huo umesaidia ongezeko la chakula ndani ya kaya za walengwa na kuanzisha shughuli za maendeleo.

# Michikichi kumaliza uhaba wa mafuta nchini

**Na Ashton Balaigwa,** KILOSA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kula nchini, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), imeanza kusambaza miche bora ya zao la michikichi mkoani Morogoro.

Lengo ni kuanza uzalishaji wa zao hilo kwenye ukanda wa Mashariki unaohusisha mikoa ya Tanga, Pwani, Morogoro na Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa upandaji miche ya michikichi uliofanyika katika Taasisi ya Utafiti Tari Ilonga, wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Taasisi hiyo imepewa jukumu la kutoa utalaamu wa kilimo hicho kwa mikoa ya Kanda ya Mashariki.

Alisema miche itakayosambazwa kwenye mikoa hiyo ni aina ya Tenera ambayo ina sifa ya kutoa mafuta tani tatu mpaka tano kwa hekta, ambayo itakapoanza uzalishaji itasaidia kupunguza tatizo la uagizaji mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kwa sasa Tanzania inaagiza mafuta ya kula kwa asilimia 60 kutoka nje ya nchi hatua inayoifanya serikali kutumia gharama kubwa kuagiza mafuta nje ya nchi.

Dk. Mkamilo alisema katika kuitikia wito wa kilimo hicho ameshajitokeza mwekezaji wilayani Kilosa ambaye ataanza kulima kwa kuanzia na ekari 12,000 ambazo zitapandwa miche 650,000 ya michikichi kwa awamu tofauti katika mashamba ya Madoto na Kivungu, wilayani humo.

Naye Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia kutoka Tari Ilonga, Magreth Mchomvu, alisema kilimo cha michikichi katika mikoa ya Kanda ya Mashariki ni kipya, Tari itashirikisha Mabwana Shamba wa Wilaya ya Kilosa na nyingine kwaajili kusambaza teknolojia ya kilimo cha michikichi ili kiweze kusaidia tatizo la upungufu wa mafuta ya kula.

Mkurugenzi wa Tari Ilonga, Dk. Joel Meliyo, alisema kituo hicho kimeshagundua aina mbili mpya za mbegu ya alizeti kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya kula, na kuanzishwa kwa kilimo cha michikichi kutaongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini. Kwa upande wake mwekezaji huyo, Felix Temu, kutoka Kampuni ya Sumagro Limited, alisema ameamua kuwekeza katika kilimo cha michikichi baada ya kuona nchi ina upungufu wa mafuta ya kula na kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi.

Alisema lengo la kuwekeza katika kilimo cha michikichi ni kujenga kiwanda cha kisasa kwaajili ya kukamua mafuta ya mawese ili kurahisisha upatikanaji wa mafuta ya kula kutoka nchini kwa kutumia zao hilo.

Akizindua upandaji wa miche ya michikichi katika mashamba ya Tari Ilonga, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoy, alisema katika kuunga mkono agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wilaya hiyo ipo tayari kuendesha kampeni ya kilimo cha michikichi, ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ndani ya nchi.

Alisema lipo eneo la kilimo hekta 460,000 na lililolimwa kwa sasa ni hekta 160,000 na kwamba bado kuna eneo kubwa lililobaki kwa ajili ya kilimo ikiwamo cha michikichi na kuwataka wakulima wa ndani na nje kuchangamkia fursa ya kilimo hicho katika wilaya hiyo.

IITA Transforming African Agriculture

IRRI

**POSITION ANNOUNCEMENT**
**Seed Systems Specialist**
**IITA-TZ-2020 - R4D-001 -NRS-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Seed Systems Specialist**

**Background:** IRRI develops and promotes new rice technologies such as high yielding varieties, climate and stress resilient varieties and technologies that offer the promise of increased productivity with optimum resources and hence ensure the welfare of farmers. There is a need to scale up the adoption of these varieties /technologies for better impacts. Tanzanian national program has released many rice cultivars, but the adoption is very low. Farmer-to farmer exchange of seeds is considered to be the main mechanism for the widespread dissemination of varieties. The dimension of farming system has changed in terms of the preference of the farmers, use of mechanized agriculture, men moving out for work and women holding the charge for farming. It's important to conduct research that can suggest interventions to improve the awareness creation, demand creation, adoption and impact of new varieties. It is also important to compare and find the pros and cons of different delivery/extension approaches for dissemination of these varieties and research around this also needs to be strengthened. Under the minimum supervision of Senior Scientist I - Plant Breeding, this position will work around, strengthening seed systems and extension research, promoting rural innovation, partnership and liaisoning, monitoring and evaluation of seed systems' development. Monitor the strategic collaboration around seed systems and extension research, conceptualize, design and execute research with the aim of evaluating the ongoing seed systems activities across different key project sites in Tanzania and strengthen the same; and interact vigorously with the regional team in relevant activities

**Duty Station:** The position will be based Morogoro, Tanzania.

**Criteria for Success / Qualifications**
- Master's degree in Agriculture/Rural management/Agri business/Rural development with minimum 5 years or relevant work experience around social sciences, rural livelihoods , sustainable agriculture/development and project management
- PhD in Agriculture/Rural management/Agri business/Rural development with minimum 3 years or relevant work experience around social sciences, rural livelihoods, sustainable agriculture/development and project management and gender

**Skills and knowledge**
**mandatory**
- Knowledge and extensive experience in the field of social science, business planning, rural development, agri and allied subjects
- Strong oral and written communication skills and scientific documentary skills
- Strong organization and interpersonal skills
- experience in working with government stakeholders (Ministries, nationals partners)
- experience in extensively working with and managing partners
- experience with gender and rural development approaches
- experience in data analysis and statistical tools like SPSS/STATA, research designer software like Survey Be/ODK/CSPRO etc

**Preferred**
- Working experience in social science, development research, rural development and applied economics
- Work experience with international organizations and area of international development
- Good understanding of rural livelihood systems

**Responsibilities**
**3.1. Purpose**
- To Monitor and manage the strategic collaboration around seed systems and extension research, conceptualize, design, execute collaborative research to evaluate, improve or strengthen varietal ad quality seed demand creation approaches across various project sites in Tanzania
- To Promote, manage various rural development and innovation models around extension/seed system/climate smart technologies engaging various institutions, change agents and stakeholders
- Lead development of gender- and market-responsive seed systems interventions and extension approaches for enhancing livelihoods, including demonstration of new varieties to generate demand and capacity building of local institutions.
- Lead development of approaches for promoting seed entrepreneurship amongst women and youth and their collectives
- Design, manage and monitor research activities including necessary protocols, research tools, data collection, analysis and interpretation
- Establish and promote strategic partnership, innovation forums and partner management for key projects.

**3.2. Engagement**
- Coordinate research with NARES/ Govt and Non Govt extension agencies, and private sector partners for strengthening seed systems and extension research and new approaches in seed and delivery systems
- Manage partners, facilitators, enumerators for executing surveys and various research-oriented interventions
- Lead coordination with NGOs, Community based institutions (CBOs), women's groups for innovation in extension approaches, gender responsive interventions and piloting seed entrepreneurship models
- Engage with Knowledge agencies, training institutions and experts for stakeholder capacity building and strengthening partnership
- Monitor and manage field technical staff for strengthening outreach programs, monitoring, evaluation, action research and experiments

**3.3. Delivery**
- Strategic Partnership and Collaboration managed and established for research and development activities
- Research studies designed, managed, analyzed and interpreted
- Documentation of research findings including data collection, analyses and reporting, measured outcomes, impacts
- Technical literature and publication in scientist journals/websites
- Knowledge and communication products including website, blogs, newsletters, etc
- Various extension models and interventions for farmers, women farmers and key stakeholders monitored and evaluated
- Develop concept notes and projects for funding or technical collaborations for research and development jointly with relevant IRRI staff
- Develop and contribute towards documentary outputs like knowledge products and research document/ publications/scientific writing/policy briefs.

**General information:**
The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date: Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

215619402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Asante JPM kwa kuliona hili

**JANA** kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya sheria nchini, Rais John Magufuli aliwaonya wapelelezi wa kesi na wasimamizi wa sheria kwa alichokisema kuwaumiza wanaopelekwa mahabusu kwa kuchelewesha kazi kwa wakati.

Pia, akielezea suala hilo amesema wapelelezi wa kesi wamekuwa chanzo cha watu kuwekwa kwenye magereza bila hatia huku wengine wakiwekwa kutokana na shinikizo la matajiri.

Kauli ya Rais Magufuli imetoa faraja kubwa hasa kwa watu wenye ndugu zao wanaoteseka gerezani na mahabusu kwa kucheleweshewa upelelezi wa kesi zao huku kila siku wakipangiwa tarehe za kurudi mahakamani.

Baadhi ya watu waliopo mahabusu wanadaiwa kuwekwa huko kwa uonevu na kujikuta wakikaa miaka mingi bila kushughulikiwa madai yao kwa wakati.

Kumekuwa na malalamiko miongoni mwa familia zenye ndugu waliopo kwenye mahabusu kwa uonevu wa kufanyiwa visasi na watu wenye uwezo pengine kwa sababu ya kutoelewana kwenye kitu hata kisicho na msingi ili kumkomoa mtu asiyekuwa na hatia.

Kutokana na hali hiyo, Rais Magufuli aliwataka viongozi wa dini nchini kuwaombea wapelelezi wanaofanya vitendo hivyo wapate laana.

Ameeleza idadi ya wafungwa waliopo katika magereza nchini ni ndogo ikilinganishwa na mahabusi na kutaja idadi ya wafungwa kuwa ni 13,455 wakati mahabusi wakiwa 17,632.

Kwa takwimu hizi inaonyesha jinsi gani kiwango hicho cha mahabusi ambao kesi zao hazishughulikiwa wanavyoteseka. Wengine wanakaa zaidi ya miaka minne bila upelelezi kukamilika na suala lake linapofanyiwa kazi hukutwa hakuwa na hatia.

Jambo hili linakatisha tamaa na wananchi kutokuwa na imani na watu waliopewa mamlaka ya kusimamia haki zao.

Rais Magufuli alitaja idadi ya mahabusi walioachiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) baada ya kubainika kubambikiziwa kesi kuwa ni 1,422.

"Mimi nimeshuhudia ukienda kwenye magereza yetu watu wanalia na wengine ni kesi za kusingiziwa, wapo wengine wamewekwa kule ndani kwa sababu ya matajiri kwamba akitaka kukukomesha utaenda kwanza mahabusu."

Serikali kila mara imekuwa ikilalamikia gharama za kuwahudumia wafungwa na mahabusi za kuwalisha na pengine matibabu wanapokuwa wagonjwa.

Gharama hizi za kuwahudumia wafungwa na mahubusi, zingeweza kutumika katika suala lingine la maendeleo kwa kupunguza idadi ya watu wanaokaa kwenye magereza na mahabusu kwa muda mrefu kwa sababu ya kesi zao kutoshughulikiwa upelelezi kwa wakati.

Ni matarajio yetu kuwa kwa kauli hii ya Rais, waliotajwa kuwa chanzo cha msongamano kwenye magereza na mahabusu, wataichukua kama changamoto na kuifanyia kazi ili haki iweze kutendeka bila upendeleo na Watanzania wawe na Imani na waliopewa jukumu la kuwashughulikia.

Kila kazi ina changamoto yake, lakini zinapofanyiwa kazi huondoa malalamiko na hata wanaopewa huduma huondoa malalamiko kutokana na kuridhika na huduma wanayopewa.

Ni matumaini yetu kuwa changamoto iliyotolewa kwa wapelelezi itakuwa chachu ya utekelezaji wa majukumu yao kwa weledi na umakini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mabadiliko ya uongozi yasirudishe mgigoro CUF

**MACHI** mwaka jana, mgogoro wa uongozi ndani ya Chama cha Wananchi (CUF) ulifikia tamati baada ya Katibu mkuu wa chama hicho, Maalim Seif kukihama na kujiunga na Chama cha ACT- Wazalendo.

Ni mgogoro ulioanza Agosti mwaka 2015, baada ya Profesa Ibrahim Lipumba, ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, kutangaza kujivua kwenye nafasi hiyo na kubaki mwanachama wa kawaida.

Prof. Lipumba alichukua hatua hiyo, kupinga ujio wa Edward Lowassa ndani ya Chadema na kupewa nafasi ya kugombea urais, akiwakilisha vyama vilivyokuwa chini cha mwamvuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa).

Vyama hivyo ni CUF, Chadema, NCCR- Mageuzi na NLD, ambavyo kwa pamoja viliunga mkono mgombea wa urais kupitia umoja huo, lakini ikawa ni kikwazo kwa Prof. Lipumba na kulazimika kuachia madaraka.

Hata hivyo, baadaye msomi huyo aliamua kurejea kwenye nafasi yake hiyo, akidai kwamba aliandika barua ya kujiuzulu lakini haikujibiwa, hivyo ana haki ya kuendelea kuwa mwenyekiti.

Uamuzi huo ulikoleza mgogoro wa uongozi ndani ya CUF hadi kufikishana mahakamani, huku wanachama nao wakiwa wamegawanyika makundi mawili, likiwamo linalomtii Katibu Mkuu na lingine Mwenyekiti.

Lakini Machi mwaka jana, mgogoro huo ulifikia tamati baada ya mahakama kuupa ushindi upande wa Prof. Lipumba, huku Maalim Seif, akihama na kujiunga na Chama cha ACT- Wazalendo.

Wakati hali ya hewa ndani ya chama hicho ikiwa imeanza kutulia, kuna fununu za mgogoro wa chini kwa chini uliosababisha Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma, Abdul Kambaya, kuondolewa katika nafasi hiyo.

Mwenyewe anathibitisha kuondolewa na kusema: "Ni kweli nimeacha nafasi hiyo baada ya kuandika barua kwa mwenyekiti wa chama ya kujiuzulu, niachie wengine waendelee."

Kambaya anabainisha kuwa, uamuzi wake huo hauna maana kwamba anataka kujiondoa CUF, bali ataendelea kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

Uamuzi wa Kambaya kuondoka kwenye nafasi hiyo umefanyika kimya kimya, lakini baadaye taarifa zikaanza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na sasa imekuwa wazi kwamba siyo tena mkurugenzi.

Ni hali inayoonyesha kuwa, huenda kuna kitu bado hakijakaa sawa ndani ya CUF, ingawa mgogoro mkubwa wa uongozi uliosababisha Maalim Seif, kujiondoa katika chama hicho ulishamalizika.

Kambaya ni mmoja wa watu wa karibu wa Prof. Lipumba, ambaye wakati wote wa mgogoro wa uongozi ndani ya CUF, hakuyumba kumtetea mwenyekiti wake, lakini sasa ameamua kuachia ngazi.

Jambo hilo linaonekana kuwa na usiri mkubwa, kwani hata Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya anakaririwa na vyombo vya habari akisema kwamba, hayo ni mabadiliko ya kawaida ndani ya chama.

Lakini pamoja na hayo, kama kweli ni kuna mgogoro unafukuta kwa chini, ni bora ukamalizwa ili chama kiingie katika uchaguzi mkuu hali ikiwa shwari kuliko kuanza kuwa na minong'ono ya migogoro.

Hatua ambayo Chama cha Wananchi (CUF) kimepitia hadi kutulia ni kubwa, hivyo utulivu uliomo ni muhimu ulindwe kwa maslahi ya chama na wanachama wake kwa ujumla.

Suala wanachama kutofautiana kimtazamo, kimawazo, maoni na ushauri ni jambo la kawaida lakini lengo kuu liwe ni kujenga, na hayo yanatakiwa kuishia ndani ya vikao na kisha shughuli nyingine ziendelee.

Hivyo kama kuna mgogoro mpya ndani ya CUF, zifanyike kila njia za kuumaliza kimya kimya, ili hatimaye chama kiingie katika uchaguzi mkuu, huku wanachama wakiwa wamoja.

Yaliyotokea miaka ya nyuma na kuyumbisha chama kwa muda mrefu yasipewe nafasi, vinginevyo wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, CUF inaweza kujikuta ikakimbiwa na wapigakura.

Inawezekana uamuzi wa kumuondoa Kambaya kwenye nafasi yake na viongozi wengine 'waliotumbuliwa' unalenga kujenga CUF, lakini jambo la muhimu ni kuhakikisha chama hakirudi kwenye mgogoro.

Migogoro ni adui wa maendeleo ndani ya vyama, hivyo isipewe nafasi, badala yake zifanyike kila njia kuhakikisha kama ni mabadiliko ya uongozi, basi yanafanyika na kumalizika salama.

# Takukuru yachunguza ufisadi mradi wa josho

**Na Dege Masoli,** KILINDI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga imeikabidhi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuchunguza mradi wa ujenzi wa josho.

Mradi huo ulioko katika Kata ya Songe, umekwama kwa zaidi ya miaka 10 huku mkandarasi akiwa ameshalipwa fedha zote kwa mujibu wa mkataba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gratian Makota, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malalamiko ya wafugaji wa kijiji cha Kwamba ya kukwama kwa mradi huo.

Wafugaji hao walilalamika kuwa wamekosa josho katika maeneo yao, hivyo kuomba serikali kuwajengea bwawa lakini mpaka sasa haujakamilika na hakuna taarifa zozote kuhusu kukwama kwake.

Wafugaji hao walisema mifugo yao iko hatarini kutokana na kufa kwa sababu ya milipuko ya magonjwa kwa kukosa josho kwenye maeneo yao na kwambawameunda kamati ya kwenda kumwona Rais John Mafufuli kumweleza hujuma hiyo huku wakiamini atachukua hatua kwa viongozi waliohusika kuukwamisha.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwamba unapotekelezwa mradi huo, Abdi Makinda, alieleza changamoto ya mradi huo kuwa ni pamoja na kuwashawishi jamii ya wafugaji kuandamana hadi ofisi za halmashauri kutaka maelezo ya kutotekelezwa josho hilo.

Makinda alisema hatua zilizochukuliwa na uongozi wake ni kuifikisha kero hiyo kwenye halmashauri na kwamba licha ya jitihada hizo, bado hakuna ufumbuzi wa tatizo hilo.

Akielezea sakata hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri alikiri kukwama kwa mradi huo lakini akadai kwamba hata mkandarasi wa ujenzi huo alishalipwa fedha zote za kazi hiyo.

"Ni kweli tatizo hilo lipo. Huu mradi ni wa tangu mwaka 2009 na mimi nimeletwa hapa mwaka juzi nimekuta mkandarasi huyo licha ya kazi hiyo kushindwa kuikamilisha, kumbukumbu zinaonyesha alishalipwa fedha zote," alisema Makota.

"Kipi kilisababisha mkandarasi huyo kulipwa fedha zote kabla ya kukamilisha na kukabidhi kazi yake? Nani alihusika na dokezo la mkandarasi huyo kulipwa? Na kwa nini mradi mpaka sasa haujakamilika? haya maswali hakuna anayeweza kuyajibu. Si mimi wala wewe ndiyo maana tumeikabidhi Takukuru ichunguze maswali hayo na itupe majibu? Alisisitiza.

Hata hivyo, Ofisa Mifugo wa Wilaya hiyo, Mwarabu Hassan, alipoulizwa kuhusiana na gharama za mradi huo, mkandarasi wake na mwaka ulioanza kujengwa, alidai yuko nje ya ofisi kikazi lakini alitaka apigiwe simu wiki ijayo.

Mmoja wa maofisa wa Takukuru ambaye hakutaka kutajwa jina lake kwa kuwa si msemaji, alithibitisha kuanza kazi ya kuchunguza mradi huo na kwamba maelezo zaidi ya uchunguzi yatatolewa taratibu zote zitakapokamilika.



Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Newala, Geoffrey Nchimbi, akichangia mada jijini Dar es Salaam hivi karibuni, katika warsha ya Elimu Haina mwisho, programu ya kuendeleza maarifa ya ufundi kwa wanawake vijana iliyoandaliwa na Shirika la Karibu Tanzania Organization ('KTO). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jiji Arusha kukamilisha madarasa ya ghorofa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha iko katika hatua za mwisho kukamilisha mradi wa ujenzi wa madarasa manne ya ghorofa na matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Msingi Murieti B, ili kupunguza msongamano wa wanafunzi ulioko Shule ya Murieti 'A' jijini hapa.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arusha, Joseph Masawe, kukagua miradi mbalimbali ukiwamo mradi huo ikiwa ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya chama hicho, katika kuadhimisha miaka 43 tangu kuzaliwa kwake, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, alisema mradi huo hadi kukamilika kwake utatumia zaidi ya Sh. milioni 328.

Dk. Madeni alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Juni 7, 2019 kwa kutia saini mkataba na ulitarajiwa kukamilika kwa miezi mitatu ambayo ingeishia Septemba 7, mwaka jana.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema kutokana na changamoto za hali ya hewa, mkandarasi alishindwa kukamilisha kazi kwa muda uliopangwa.

“"Kutokana na changamoto hii mkandarasi aliomba muda wa nyongeza na hadi sasa mradi uko mbioni kukamilika ili tupokee wanafunzi wa eneo la Msasani katika Kata ya Murieti na viunga vyake," alisema.

Kwa mujibu wa Madeni, lengo la mradi huo ni kupunguza msongamano mkubwa ulioko Shule ya msingi Murieti 'A' na kuongeza ubora wa elimu ndani ya Jiji la Arusha.

Dk. Madeni alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi Construction Co. Ltd kwa kutumia makusanyo ya ndani ya halmashauri hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema kujengwa kwa shule hiyo kutaondoa msongamano ulioko katika Shule ya Muriet 'A'.

"Tutawahamisha watoto 600 toka pale Muriet na tunatamani tuchukue wale wa madarasa ya chini ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu," alisema.

Kwa mujibu wa Daqarro, barabara ya kuingia shuleni hapo itatengenezwa vizuri ili kuondoa tope na kuwezesha wanafunzi kutembea bila shida.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Msasani, Kata ya Muriet, Said Juma, alishukuru serikali kuwajengea shule hiyo ambayo itakuwa mkombozi kwa jamii yao.

Aliomba wazazi kutumia fursa hiyo vizuri kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shuleni, wanaenda kwa sababu hakuna haja ya kuacha kuwapeleka wakati wamesogezewa huduma karibu.

## Serikali kusajili wadau mnyororo uongezaji thamani mazao kilimo

**Na Mathias Canal,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kuanza usajili wa wadau wote katika mnyororo wa uongezaji thamani ya mazao ya kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema kuwa lengo la usajili huo ni kutaka kuwa na takwimu sahihi ya wadau mbalimbali wanaotoa huduma katika sekta ya kilimo nchini.

Alitaja wadau hao kuwa ni pamoja na wakulima, watoa huduma mbalimbali za pembejeo, wasindikaji, wafanyabiashara za mazao, taasisi za fedha, watoa huduma wa sekta binafsi katika kilimo kama Asasi za kiraia na mashirika ya ndani na nje ya nchi yanayotoa huduma kwenye kilimo, wenye viwanda vya kuongeza thamani, watengenezaji, wauzaji na wasambazaji wa zana za kilimo.

Alisema kuwa usajili huo utafanyika kwa njia ya kidijitali kwenye mtandao wa www.kilimo.go.tz na kupitia simu za kiganjani.

Waziri Hasunga alisema kuwa usajili huo utaanza rasmi Februari 15 na kukamilika Aprili 14, 2020.

Kupitia usajili huo, takwimu na taarifa muhimu zitapatikana kwa ajili ya kuendeleza kilimo zikiwamo watoa huduma za pembejeo, huduma za ugani, taasisi za fedha, wasindikaji na wenye viwanda, watengenezaji, wauzaji, wasambazaji wa zana za kilimo, na hivyo, kujua kiwango cha uwekezaji katika sekta ya kilimo.

Hasunga alisema kuwa Wizara ya Kilimo inaendelea na usajili wa wakulima kote nchini ili kuwatambua na kurahisisha utoaji wa huduma za ugani, mitaji kwa ajili ya kilimo, upatikanaji wa pembejeo na kupata taarifa sahihi za uzalishaji. Alisema kuwa usajili wa wakulima awamu ya kwanza hadi kufikia Januari 2020 ni jumla ya wakulima 1,279,884 na usajili unaendelea.

Kati yao, wakulima wa mashamba makubwa ni 147 wakiwamo 101 wa zao la kahawa, chai (12), mkonge (22) na miwa (12); na wakulima wadogo ni 1,279,737 wakiwamo 309,000 wa zao la Korosho (asilimia 98.4), 305,260 wa Kahawa (95.4), Pareto 10,687 (112), mkonge 6,885 (91), miwa wakulima 6,745 (96.4), chai wakulima 31,092, Tumbaku wakulima 53,757 (107.5%) na pamba wakulima 556,306 (92.7).

# Serikali yakodi ndege kukabiliana na nzige

INATOKA UK. 3

taarifa haraka serikalini ili hatua zichukuliwe.

Aliitaja mikoa ambayo inasadikiwa kuwa na viashiria vya mazalia ya nzige kuwa ni pamoja na Katavi na Kigoma na kuwataka watu wa mikoa hiyo kuwa makini na kutoa taarifa sehemu husika.

Kuhusu mbegu feki, alisema inasemekana kuna wafanyabiashara wa mbegu wanachukua mazao wanayapaka rangi na kuweka dukani huku wakiwadanganya wananchi kuwa ni mbegu bora, jambo ambalo halikubaliki. Aliagiza TOSCI kuhakikisha wanazunguka mikoa yote kuwasaka wahalifu wanaofanya vitendo hivyo na kuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kuwafungulia kesi za uhujumu uchumi.

"Naomba TOSCI piteni mikoa yote kuwatafuta watu wa aina hiyo wanaoiharibia serikali," Hasunga aliagiza.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa ili kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

Hasunga alisema kutokana na kuhamasisha uwekezaji katika kilimo, matumizi ya viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mazao, yameendelea kuongezeka katika kipindi cha mwaka 2015/2018, akibainisha kuwa uagizaji wa viuatilifu umeongezeka toka tani 343.5 hadi 6,387.97 mwaka 2018.

"Uzalishaji wa mbegu bora takwimu zinaonyesha mwaka 2019/2020 tani 187,197 hadi kufikia Januari 31 na kuongeza upatikanaji wa mbegu umefikia tani 71,207.65 ambapo kati ya hizo tani 66,031,85 zimezalishwa nchini ambapo ni sawa na asilimia 92.7," alisema.

Aliongeza kwa upande wa miche hadi kufikia Januari 31, jumla ya miche 22,707,871.63 ya zao la kahawa, korosho na chai imezalishwa nchini na kusambazwa kwa wakulima.

"Ni tani 5,175,79 za mbegu ndo zimeingizwa kutoka nje, na mihogo jumla ya pingili 38,860,300 zenye uwezo wa kupanda ekari 9,715 zimezalishwa," alisema.

Alisema katika msimu wa 2019/20, mahitaji ya mbolea ni tani 586,604 na hadi kufikia Januari 30 mwaka huu, upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 454,339, sawa na asilimia 77.5.

# Magufuli awashukia wapelelezi

INATOKA UK. 2

"Tunafanya mazungumzo na ninafikiri nitasaini hati mapema ndani ya siku mbili tatu ili hawa wafungwa waweze kurudishwa kwao na hii pia itatusaidia kupunguza wafungwa wanaokaa mahakamani," alisema Rais Magufuli. Kadhalika, alisema miongoni mwa kero ambazo alizipokea kipindi cha kampeni mwaka 2015 ni pamoja na wananchi wengi kulalamika ucheleweshaji wa kesi, kukithiri kwa vitendo vya rushwa, ubambikizaji wa kesi, ucheleweshaji wa upelelezi. Mlundikano wa wafungwa na mahabusi.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa mahakakama nchini na kwamba ili mahakama zote ziweze kufanya kazi kwa ufanisi kunahitajika kuwa na watumishi 10,351, kwa sasa kuna watumishi 5,947, ikiwa ni upungufu wa 4,404.

Alisema pamoja na Tanzania kuwa na sheria nzuri kuna mifano mingi ya wanaosimamia leseni, vibali, wanaokusanya kodi kuwa vikwazo na vizuizi vya biashara na uchumi badala ya kuwa wawezeshaji.

"Mafanikio ya sheria ni kutathmini kwa kiasi gani sheria hiyo imefanikisha maskini waingie katika biashara na uwekezaji, sheria inayowazuia maskini kufanya hivyo haiwezi kufanikiwa," alisema Prof, Juma.

Naye Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Rugemeleza Nshala, alisema ni lazima kuwapo na utengamano wa kisheria na mfumo wa kisheria, haki ili Tanzania iweze kufanikiwa katika uwekezaji.

Nshala alisema kinachowavutia wawekezaji sio kodi wala misamaha ya kodi bali utengamano uliojikita katika misingi ya sheria na kuheshimika kwa mfumo mzima wa haki.

Alisema Katiba inaelekeza wazi kunapokuwa na matatizo yoyote yanayohusiana na uwekezaji na biashara ni vyema yapelekwe mahakamani tofauti na inavyofanyika sasa.

Aliongeza kuwa endapo mahakama ikipewa fursa ya kuamua mashauri yake kwa haki bila shinikizo, wafanyabiashara na wawekezaji wataziheshimu na hivyo kampuni zitafuata na kutii uamuzi wa mahakama.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na rundo la takataka zilizotelekezwa, kando ya barabara katika eneo la Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwisho kusajili huduma ndogo za fedha Oktoba

INATOKA UK. 4

fedha katika uchumi wa taifa," alisema.

Kiongozi huyo alisema tatizo lingine lililobainika ni ukosefu wa utaratibu wa kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha na kuwapo kwa mianya ya utakatishaji wa fedha haramu kutokana na taasisi za huduma ndogo za fedha kutokuwa na utaratibu wa kisheria unaozitaka kutekeleza matakwa ya Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu.

Akizungumza kwa niaba ya wahariri wenzake, Mhariri wa Azam Media, Ben Mwang'onda, alisema wizara hiyo imefanya jambo jema kuwaelimisha wahariri kama mhimili mmoja wapo wenye nguvu na unaotegemewa kufikisha habari sahihi kwa jamii na kuondoa upotoshaji uliokuwa ukiendelea miongoni mwao, ikiwamo kwa baadhi ya watu kuamini sheria hiyo inalenga kukusanya kodi hadi kwenye vikao vya kifamilia, harusi na mambo mengine yasiyohusisha biashara za kifedha.

Awali, Kaimu Kamishna Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha, Dionisia Mjema, alisema nia ya serikali kufikisha elimu hiyo kwa wahariri na wanahabari ni kutoa tafsiri sahihi juu ya sera, sheria na kanuni ndogo za kifedha ili kupata uelewa na tafsiri sahihi na kufikisha kwa umma ili dhamira njema ya serikali kuendeleza sekta ndogo ya kifedha ifanikiwe na hatimaye kuondoa nchi kwenye lindi la umaskini.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo na Huduma za Fedha Vijijini (FSDT), Mwombeki Baregu, alisema ili kutatua matatizo yanayoikabili sekta ndogo ya fedha, serikali ilitunga sheria hiyo ili pamoja na mambo mengine, kuzitambua taasisi za huduma ndogo za fedha katika madaraja manne.

"Daraja la kwanza linahusisha taasisi za huduma ndogo za kifedha zinazopokea amana wakiwamo wakopeshaji binafsi, daraja la pili linahusisha taasisi za huduma ndogo za kifedha zisizopokea amana wakiwamo wakopeshaji binafsi, watoa huduma kwa njia za kielektroniki na kampuni ya mikopo.

"Daraja la tatu ni vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (Saccos) na daraja la nne ni vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kama vikoba, VSLA na vingine," alisema.

Akaongeza kuwa malengo mengine ni kuboresha usimamizi na uendelezaji wa sekta ndogo ya fedha nchini na kuipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha pamoja na kuwalinda watumiaji wa huduma hizo sambamba na kudhibiti matatizo yanayoweza kutokea katika sekta ndogo ya fedha.

# Serikali yaijibu hoja ya Mbowe

INATOKA UK. 3

ambayo nchi ifafanya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani.

Baada ya kujenga hoja yake, Mbowe aliuliza swali lake akisema: "Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa busara zako binafsi katika serikali ambayo wewe ni kiongozi mwandamizi, unafikiri ni lini mtaruhusu vyama vya siasa vifanye wajibu wake wa uenezi kujiandaa na uchaguzi mkuu?

"Pili, serikali ina mpango gani kuhakikisha taifa inapata tume huru ya taifa ya uchaguzi na kuhakikisha kwamba uchaguzi wa mwaka huu unakuwa huru na wa haki na wa halali?"

Majaliwa alimjibu Mbowe akisema vyama vya siasa havijazuiwa kufanya shughuli zake ila serikali imeweka utaratibu muhimu unaowezesha vyama kufanya shughuli zake za kisiasa kama ambavyo kumekuwa na uhuru kwa wote.

Alisema wanasiasa wote ambao waliomba ridhaa kwenye maeneo yao na wakapata ridhaa hiyo ya kuendelea kufanya shughuli kwenye maeneo ambako wamepata ridhaa kama vile madiwani, wabunge wanaendea kufanya shughuli zao za siasa kama kawaida.

"Lini tutajiandaa kwa ajili ya uchaguzi? Ratiba za uchaguzi zitatolewa na ratiba zile zitaeleza kuanzia lini, shughuli za kampeni zitaanza lini ili vyama vikaeleze sera zake kwenye maeneo yote ili sasa wananchi waweze kupata fursa ya kuendelea kufanya uamuzi ya sera ipi, ya chama gani kinafaa kutuletea maendeleo nchini.

"Kwa hiyo, hilo linaendelea na wote mnajua hata kulipokuwa na uchaguzi mdogo pale ratiba ilipokuwa inatolewa na kila chama kilikuwa kinaendelea kushiriki na huo ndiyo utaratibu ambao unaifanya hata nchi kuwa imetulia na watu wote kufanya shughuli za siasa kama kawaida na tutaendelea kufanya hivyo kwa vyama vyote.

"La pili ni suala la tume huru, jambo hili hata Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu juzi alitoa majibu hapa, na mimi nataka nirudie tu kwamba tume hii imeundwa kwa mujibu wa katiba, na kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi kipengele 78, 74 na kipengele kidogo cha 7, 11 na 12 kinaeleza kwamba hiki ni chombo huru."

Pamoja na majibu hayo, Majaliwa aliongeza kuwa chombo kimeelezwa pia kwenye katiba kinaundwaje na chombo hicho hakipaswi kuingiliwa na chombo chochote iwe Rais wa nchi, iwe chama chochote cha kisiasa au mamlaka nyingine yoyote ile haipaswi kuingilia.

"Sasa kunaweza kuwa kuna tofauti ya neno huru hili, tunataka itambulike vipi, chombo kipo, kinajitegemea na kinafanya kazi yake bila kuingiliwa na mtu yeyote kwa mujibu wa katiba yetu ya mwaka 1977. Hayo ndiyo maelezo sahihi na ambayo yapo kwa mujibu wa katiba na sheria ambazo tumeziweka," alisema.

HABARI KITAIFA

# Serikali: Hii ndiyo hali ya mafuta nchini

**Na Mwandishi Wetu**

UWEZO wa nchi kuhifadhi mafuta umeongezeka kutoka lita milioni 900 mwaka 2015 hadi lita bilioni 1.3 kwa sasa, imeelezwa.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kutunuku tuzo na zawadi kwa waendesha vituo vya mafuta vya Kampuni ya Puma Energy Tanzania.

Dk. Kalemani alibainisha kuwa kwa sasa Tanzania ina akiba ya mafuta ya petroli lita milioni 97 ambayo yanatosha kuendesha nchi kwa siku 38 kuanzia juzi, dizeli lita milioni 197 zinazotosha siku 28 na mafuta ya ndege lita milioni 30 yanayotosha siku 56.

"Pia, tuna akiba ya lita 600,000 za mafuta ya taa, hii ni kutokana na kupungua kwa uhitaji wa nishati hii maana Watanzania wengi sasa, hasa maeneo ya vijijini wameunganishwa na Gridi ya Taifa ya umeme," alitamba.

Alisema mafanikio hayo yametokana na uboreshaji wa huduma za uagizaji wa mafuta uliofanywa na serikali tangu mwaka 2012, akibainisha kuwa tangu serikali ya awamu ya tani iingie madarakani, nchi haijakumbwa na tatizo katika upatikanaji wa nishati hiyo.

Dk. Kalemani ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, aliutaka uongozi wa kampuni hiyo kupanua wigo wa biashara na kuyafikia maeneo yote ya nchi, hasa vijijini ambako hakuna vituo vya mafuta, hivyo wananchi wanalazimika kuhifadhi mafuta kwenye madumu na kuyauza kwa rejereja kwenye makopo ya maji.

Aliitaka kampuni hiyo ijenge vituo vya kuuzia mafuta katika maeneo ya mikoa ya Katavi, Mara and Geita ambayo haijayafikia.

Waziri huyo pia aliwataka waongeze mapato ya kampuni ili kodi iongezeke na wahakikishe mwaka huu wanatoa gawio la Sh. bilioni 13 kwa serikali, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni mbili kulinganishwa na gawio lao la mwaka jana.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Puma Energy, Dominic Dhanah, alisema ni mara ya kwanza tuzo hizo zinatolewa nchini kwa lengo la kutambua mchango na kutoa zawadi kwa waendesha vituo bora zaidi vya mafuta vya kampuni hiyo.

"Lengo la tuzo hizi ni kutoa hamasa na kuwapa changamoto waendesha vituo hawa kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wetu kote nchini," alisema.

Dhanah alisema Kampuni ya Puma inaunga mkono juhudi za serikali katika kutoa ajira kwa wananchi na ndiyo maana inawapa fursa Watanzania kuendesha vituo vyake na wao kuajiri Watanzania wengine kama wauza mafuta, waendesha maduka na walinzi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Puma Energy, Dk. Selemani Majige, alimshukuru Waziri Kalemani kwa kukubali mwaliko wao na kushiriki katika tuzo hizo.

Alimhakikisha waziri huyo kuwa watayafanyia kazi maelekezo aliyowapa ili kampuni hiyo iendelee kufanya vizuri zaidi katika kuchangia mapato ya serikali kwa kodi na gawio.

Tuzo zilizotolewa ni pamoja na msimamizi bora wa kituo, mwendesha kituo bora katika huduma za magari, mwendesha kituo bora wa mwaka katika ubunifu na kituo chenye huduma bora kwa wateja kwa huduma tofauti na uuzaji wa mafuta.

Zingine ni mwendesha kituo bora wa mwaka, mhudumu bora katika vituo vya mafuta, mwendesha kituo bora wa mwaka katika huduma za malipo ya kidijitali na mwendesha kituo bora wa mwaka katika uhusiano bora na jamii inayomzunguka.

Puma Energy Tanzania ni kampuni ya mafuta iliyosajiliwa nchini na inamilikiwa kwa pamoja na serikali kupitia Msajili wa Hazina na Puma Investments Limited, kila upande ukiwa unamiliki hisa kwa asilimia 50.

Kampuni hiyo kwa sasa ina uwezo wa kuhifadhi jumla ya lita milioni 94 za mafuta, ikiwa na vituo 52 katika maeneo mbalimbali nchini na inatoa huduma katika vituo vinane vya ndege.



Mawasiliano ya barabara kati ya Kata ya Solwa na Kata ya Salawe, Halmashuari ya Wilaya ya Shinyanga, yakiwa yamekatika baada ya daraja kusombwa na maji na kusababisha usumbufu wa usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Kilimo hai kitainusuru dunia'

**Na Faustine Feliciane,** MOSHI

MKURUGENZI na Mwanzilishi wa Kituo cha Kujifunzia Kilimo Hai (SJS)wilayani Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro, Padri Alwyn de Souza, amesema kilimo hai ndiyo njia sahihi kuinusuru dunia na magonjwa yasiyoambukiza.

Akizungumza na Nipashe wilayani humo, De Souza alisema magonjwa mengi yanayotokea sasa yanatokana na matumizi ya vyakula vilivyozalishwa kwa kemikali na anaona kuna haja ya jamii kugeukia moja kwa moja kilimo hai.

Alisema kuanzishwa kwa kituo hicho (mwaka 2017) kutasaidia Watanzania na nchi nyingine za Afrika kujifunza na kupata ujuzi wa kilimo hai.

"Magonjwa yanayotokea sasa mengi yanatokana na sisi wenyewe wanadamu kutofuata umuhimu wa kutumia mazao yaliyozalishwa kwa njia ya asili pasi na kutumia kemikali, hii ni kama tunajiangamiza wenyewe.

"Kama tutarejea enzi za zamani ambapo watu walikuwa wakilima kwa kufuata njia za asili bila kutumia kemikali, tutaepukana na magonjwa kama kisukari, presha na kansa ambayo sasa yanawamaliza watu wengi," alisema. De Souza aliongeza kuwa kituo chao ni mfano mzuri kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla kwa kuwa wanaendeleza kilimo hai na ufugaji wa njia ya asili.

Mkuu wa Shamba la Kituo hicho, Martin Muhando, alisema wana mimea mingi ambayo ni dawa kwa binadamu, wanyama na mimea mingine. "Kila kitu kinapatikana kwenye shamba hili, mbolea inajizalisha hapa kwa njia ya asili, lakini pia mifugo tuliyonayo hapa ikipata magonjwa, inatibiwa kwa njia ya asili kwa kuwapa dawa za mimea. "Hakuna mmea au wadudu ambao hawana kazi shambani, kila kitu kinajizalisha hapa, hiki ni kilimo ambacho kinatuepusha na magonjwa kwa sababu vyakula vyake havina kemikali hata kidogo, kinachotumaliza binadamu ni matumizi ya kemikali kwenye kilimo na ufugaji," alifafanua.

Kituo hicho kinamilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Mwanga ambalo pia linamiliki Shule ya Sekondari St. Joseph iliyoko wilayani humo.

## Waziri akomalia Soko la Ndugai

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameuagiza uongozi wa Jiji la Dodoma kuhakikisha mkandarasi anayejenga Soko la Ndugai na Kituo cha Mabasi Nzuguni, anakamilisha ifikapo Februari 15 mwaka huu kama ilivyoelekezwa na Rais John Magufuli.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Magufuli aliweka jiwe la msingi katika miradi hiyo na kumwagiza mkandarasi kukamilisha ifikapo Februari 15 mwaka huu kama ilivyopangwa kwenye mkataba wake.

Jafo alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miradi hiyo.

Alimtaka Mkandarasi wa miradi hiyo, Mohamed Builders, kuongeza kwa nguvu kazi ili kukamilisha kwa muda uliopangwa.

"Pia, jiji hakikisheni mnaweka usimamizi mzuri wa uendeshaji wa miradi na wafanyabiashara watakaopata vizimba, wawe ni wafanyabiashara wadogo ili nia na dhamira ya Rais Magufuli itimie.

"Mkurugenzi, wafanyabiashara wadogo wadogo ndiyo wenye thamani kubwa kwa Rais, humu tunatarajia kuwaona wale wafanyabiashara choka mbaya, hatutarajii kuona mtu anachukua vizimba vingi halafu anapangisha kwa wengine, simamieni hili," aliagiza.

Akizungumzia kuhusu suala la usafi, Jafo aliagiza kuwekwa kampuni maalum kwa ajili ya kusimamia usafi.

"Itakuwa ni dhambi kubwa sana soko lililopewa jina la Spika wetu Ndugai lije kuharibiwa siku chache," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema tayari wameanza kutekeleza maagizo waliyopewa ikiwamo ya kuhakikisha wanaweka msimamizi mzuri na kuweka uwazi katika ugawaji wa vizimba.

Mhandisi Mshauri wa miradi hiyo, Emmanuel Mahimbo, alisema katika kituo cha mabasi hatua waliyofikia ya ujenzi kituo cha magari na kwamba sasa kiina uwezo wa kushusha na kupakia abiria.

# Sheria ya ushirika kufumuliwa rasmi

WIZARA ya Kilimo iko katika hatua za mwisho kuwasilisha bungeni mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Maendeleo ya Ushirika yatakayoendana na mahitaji ya sasa.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbinga Mjini(CCM), Martin Msuha, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuondoa upungufu uliopo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashe alisema mabadiliko hayo yatahusisha mfumo na muundo wa uongozi ili kuendana na mahitaji ya teknolojia na kuleta ushindani wa kibiashara.

"Tunaelewa kuwa ushirika ni dhana ya hiari, lakini serikali ni msimamizi mkuu wa vyama vya ushirika. Pale ambapo viongozi wake au vyama vyenyewe havitekelezi malengo yaliyokusudiwa na ushirika, tunakiri vyama vinakabiliwa na changamoto za kiutendaji, usimamizi, viongozi kutokuwa wadilifu na upungufu wa kimfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini," alisema.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

Aidha, alisema viko baadhi ya vyama vya ushirika ambavyo vinafanya vizuri.

"Mfano, Chama cha Ushirika cha Chai Mkonge, Mafinga na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), ushirika ndicho chombo cha kuwaletea wananchi maendeleo ya kiuchumi kwa kuwaunganisha wakulima ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kutoa huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo na kutafuta masoko ya mazao," alisema.

Hata hivyo, alisema Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 - 2020 (Ibara ya 22 (g)(iv) na 86 (a)) inaelekeza kuifanyia mapitio Sera ya Vyama vya Ushirika na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na upatikanaji wa takwimu zitakazosaidia kuandaa mipango.

"Nyingine ni kuleta mageuzi katika sekta ya ushirika na kuimarisha uchumi wa taifa na kuviimarisha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kwa kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na biashara,"alisema.

# Watoto 6,400 wa mitaani watambuliwa

JUMLA ya watoto 6,393 wanaoishi na kufanya kazi mitaani wametambuliwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha na Iringa.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema jana bungeni jijini hapa wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomary Khamis.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani jijini Dar es Salaam hali ambayo inakosesha watoto hao haki zao za msingi kama elimu na malezi bora na kuhoji.

Kutokana na hali hiyo, Khamis alihoji serikali imechukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo la watoto wa mitaani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema katika idadi hiyo watoto wa kiume ni 4,865 na wa kike 1,528 na walikuwa wakiishi mitaani kutokana na sababu mbalimbali.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile.

Naibu waziri alizitaja baadhi ya sababu hizo kuwa ni kufiwa na wazazi, migogoro ya familia, kutengana kwa wazazi, vitendo vya unyanyasaji na ukatili na umasikini katika ngazi ya kaya na kusababisha ongezeko la watoto hao.

"Taarifa ya utafiti ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani uliofanywa na Wizara Mei 2018, iliohusisha mikoa sita nchini, ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha, na Iringa na jumla ya watoto wapatao 6,393; wakiwamo wa kiume 4865 na wa kike 1528 wanaishi na kufanya kazi mitaani walitambuliwa," alisema.


Aidha, alisema katika kipindi cha Oktoba, 2018 hadi mwezi Machi, mwaka jana, watoto 2,702 walipatiwa huduma mbalimbali. Watoto hao katika mikoa na idadi yao kwenye mabano kuwa ni Arusha (330), Dar es Salaam (475), Dodoma (337), Iringa (313), Mwanza (770) na Mbeya (447).

"Huduma zilizotolewa ni pamoja na afya, chakula, malazi, kurudishwa shuleni, stadi za ufundi, stadi za maisha, kuunganishwa na familia pamoja na msaada wa kisaikolojia na kijamii," alisema.

Dk. Ndugulile alisema serikali kwa kushirikiana na wadau, inaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa malezi na ulinzi wa watoto wakiwamo walio katika mazingira hatarishi.

"Pia itaendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi kwenye eneo la stadi za malezi na ulinzi wa watoto," alisema.

Alitoa rai kwa jamii kuhakikisha jukumu la matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto linatekelezwa ipasavyo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Waziri atetea haki vyombo vya habari



NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza (pichani), amesema serikali imekuwa ikichukua hatua bila kupendelea chombo chochote cha habari kinachobainika kukiuka sheria na taratibu ikiwamo kutoa habari za uongo.

Shonza alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza ya Mbunge wa Konde (CUF), Khatib Said Haji, ambaye alidai kuwa ameshuhudia baadhi ya vyombo vya habari hususani magazeti yakipewa adhabu ya kufungiwa kwa kutoa habari za uongo.

Hata hivyo, alisema baadhi ya magazeti yamekuwa hayachukuliwi hatua yoyote licha ya kuwa kinara wa kudhalilisha na kuchafua watu.

Kutokana na hali hiyo, alihoji ni kwanini serikali haichukui hatua kwa vyombo hivyo pamoja na wamiliki wake?

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema suala hilo halina ukweli kwa kuwa serikali inafanya kazi kwa kusimamia sheria na kanuni zilizopo.

"Mara zote ndani ya Bunge tumekuwa tukifafanua kwamba wizara tumekuwa tukichukua hatua kwa magazeti yanayokiuka sheria. Si kweli kwamba hatuchukui hatua kwa magazeti ya Tanzanite kama alivyoesema mbunge. Tumeshajibu mara kadhaa humu ndani kwamba tumeshawaandikia onyo pamoja na mengine yaliyokuwa yanakiuka sheria," alisema.

Alifafanua kuwa sheria ya habari inaeleza kwamba kabla ya kuchukua hatua yoyote kwa chombo chochote cha habari, kwanza wanapaswa kupewa onyo mara ya kwanza.

"Tunatoa nafasi kwa mara ya pili pale ambapo tunaona kwamba hali hiyo inazidi ndio tunachukua hatua," alisema na kusisitiza kuwa hatua hizo zimekuwa zikichukuliwa bila upendeleo.

"Sisi wizara tumekuwa tukichukua hatua pale ambapo tunaona tumeshaonya mara kadhaa lakini bado hawajajirekebisha," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema ni kosa la jinai kwa mtu au vyombo vya habari kutoa, kuandika, kusambaza au kutangaza habari za uongo na kuhoji Jeshi la Polisi linachukua hatua gani kwa watu au vyombo vya habari vinavyofanya makosa hayo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema heshi hilo lina utaratibu unaotumika pindi mtu anapokuwa ametenda makosa ya jinai na ushahidi hukusanywa kisha jalada huandaliwa kwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ushahidi ukijitosheleza mtuhumiwa hufikishwa mahakamani.

Alisema serikali ina mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016. Alisema sheria hiyo inaelekeza kuchukua hatua kwa chombo cha habari kilichotoa taarifa za uongo ikiwa ni pamoja na kufuta leseni au kusimamisha leseni kwa muda pale kinapokiuka masharti ya leseni hiyo.

# Manyara kuadhimisha miaka 43 CCM Mbulu

**Na Allan Isack,** MANYARA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Manyara katika kusherehekea miaka 43 ya chama hicho imepanga kuadhimisha kimkoa Februari 8, mwaka huu, katika uwanja wa Kambarage wilayani Mbulu.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Mkoa wa Manyara, Jacob Siay, akizungumza jana alisema, maandalizi ya maadhimisho hayo yanaendelea vizuri na yatafanyika katika uwanja wa Kambarage .

Siay alisema hata hivyo mgeni rasmi katika maadhimisho hayo hajathibitishwa bado.

"Tulidhani Pinda ambaye ni mlezi wetu wa CCM Mkoa wa Manyara angekuwa mgeni rasmi, lakini haitakuwa hivyo, tutawatangazia nani atakuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo," alisema.

Alisema CCM Mkoa wa Manyara, inampongeza Rais John Magufuli kwa kusimamia na kutekeleza ipasavyo Ilani ya uchaguzi wa CCM wa mwaka 2015/2020.

Hata hivyo, alisema kutokana na juhudi hizo za Rais John Magufuli, CCM inazidi kuendelea kuaminiwa na wananchi wameahidi kumuunga mkono kwenye ujenzi wa taifa.

Katibu wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, Ally Kidunda, alisema watafanya maadhimisho hayo ya kuzaliwa chama hicho Februari 7, kwenye Kata ya Emboreet.

Kidunda alisema pia siku hiyo viongozi wa kata zote 18 za CCM za wilaya hiyo, watafanya mikutano ya hadhara katika kusherehekea maadhimisho ya miaka 43 ya kuzaliwa chama hicho.

"Kila viongozi wa kata watasoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM kwa mwaka 2015/2020 ili wananchi watambue maendeleo yaliyofanyika," alisema.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kichama Meru, Gurisha Mfanga, akizungumza wakati kamati ya Siasa ya wilaya hiyo ilipotembelea katika Jengo la Zahanati ya Elikitumuni, katika Halmashauri ya Meru, wilayani Arumeru mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wanaonyanyapaa wenye ulemavu waonywa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JAMII imetakiwa kuacha tabia ya kuwanyanyapaa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU), badala yake wawapende na kushirikiana nao katika mambo muhimu kwenye jamii.

Rai hiyo, imetolewa jana na Mratibu wa Kituo cha kulelea watoto wanaoishi na Ukimwi, cha St. Lucia Orphanage, kilichopo Kata ya Moshono, jijini Arusha, Allen Gervas, wakati akipokea msaada wa vyakula, sabuni na mafuta.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mratibu wa Kituo hicho, Allen Gervas, alisema watoto hao ni kama walivyo wengine hivyo wanastahili kupewa matunzo na huduma muhimu katika jamii.

Alisema kituo hicho, kinawatoto 27 wanaoishi na VVU, na wanatatizo la kukosa kadi za bima ya afya pamoja na huduma nyingine.

Aliiomba jamii kujitoa zaidi katika jukumu la kuwasaidia watoto hao, kupata mahitaji muhimu ya kibinadamu.

"Watoto hawa kila siku lazima wanywe dawa, wapate huduma muhimu za kijamii hivyo, ni vema jamii kujitokeza kuwasaidia watoto hawa wenye uhitaji wa maalumu," aliomba.

Naye Mwakilishi wa mdau aliyejitolea msaada huo, katika kituo hicho, Japhet Kishumbua, alitaka jamii kujitoa kusaidia watu wengine wenye mahitaji maalumu.

"Naomba tupate ushirikiano kutoka kwa viongozi wa mkoa na Wilaya ya Arusha, wendelee kuwatafuta watoto hao wanaoishi katika mazingira magumu na kuwapatia msaada," alisema.

Mtendaji wa Kata ya Moivaro, Sophia Laizer, alishukuru kwa msaada huo, ameiomba kuwa na utaratibu wa kuwasaidia makundi yenye uhitaji maalumu.

# Wahamasishwa kulima pilipili kwa soko la nje

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI Mkoa wa Mara, wametakiwa kulima kilimo cha pilipili kwa kuwa zao hilo, lina soko kubwa na la uhakika katika mataifa ya nje.

Rai hiyo, ilitolewa jana jiji Arusha na Fadhili Maganya, Mwenyekiti wa Taasisi ya Agricalture Frontiers, ambayo inajihusisha na shughuli za kuendeleza kilimo na wafugaji.

Maganya alisema wameingia makubaliano na Taasisi ya Bredas Tradas and General kwa ajili ya kuwatafutia soko la pilipili nje ya nchi.

Alisema wiki ijayo watatambulisha rasmi mradi huo, wa kilimo cha zao la pilipili kwa viongozi wa serikali ya Mkoa wa Mara na watazindua rasmi kilimo hicho mwezi Machi, mwaka huu.

Alisema hadi sasa wakulima wameandaa jumla ya ekari 200, katika wilaya za Butiama, Musoma na Rorya, mkoani Mara, maeneo hayo yapo kando kando ya Ziwa Victoria.

Hata hivyo, alisema maeneo hayo yametengwa maalumu kwa ajili ya kilimo cha zao hilo, la kibiashara lengo ni kuwainua wakulima kiuchumi.

Aliitaja mikoa mingine ambayo inalima zao hilo kuwa ni mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro Kilimanjaro Manyara na Arusha.

Alisema kupitia taasisi hiyo, wakulima watakuwa na uhakika wa soko la zao la pilipili, katika nchi za nje.

Pia alieleza kilimo cha pilipili hakitumii dawa za viwandani na hazishambuliwi na wadudu.

Taasisi hiyo, imesajiliwa mwaka 2019, kwa ajili ya kuwaunganisha wakulima kupata masoko ya uhakika wa mazao yao, pamoja na kuwapatia maarifa ili kuboresha kilimo na kuwatafutia mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

Alisema wameandaa programu mbalimbali za kuongeza mnyororo wa thamani kwa wakulima katika shughuli za kilimo.

Vile vile, alisema wamelenga kusaidia kukuza kilimo cha mboga, mahindi na mpunga kwenye mikoa ya Arusha na Morogoro katika wilaya za Malinyi na Ulanga.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bredas Traders &General Supply, alisema kampuni hiyo, inahusika kununua na usafirishaji zao hilo nje ya nchi. Alisema pilipili zina soko kubwa katika nchi za Italia, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza na Ghana.

Hata hivyo, alisema bei ya kilo moja ya pilipili kavu ni Sh. 4,500, na tayari kuna ekari 200 mkoani mara za kuzalisha zao hilo, na taasisi hiyo inatakiwa kusafisirisha tani 80 kila mwezi.

Mradi huo wa kilimo cha pilipili unadumu kwa muda wa miaka mitatu hadi tisa na kwa kipindi chote wakulima watakuwa wakinufaika kwa kuwa halina gharama kubwa.

# Waiangukia serikali bandari kuzuia chakula miezi sita

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKURUGENZI wa Shirika la New Life Tanzania, Askofu Glourius Shoo, ameiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia kuingiza chakula cha msaada kwa ajili ya watoto wanaotoka katika jamii zilizo pembezoni, kilichozuiwa bandarini kwa miezi sita sasa.

Kiongozi huyo alitoa ombi jana wakati wa kongamano la 11 la wadau wa masuala ya watoto kutoka nchi mbalimbali dunia, lililofanyika mjini Moshi.

"Kila mwaka tumekuwa tukipewa msamaha wa kodi tukiingiza vyakula vya msaada, lakini kwa mwaka huu tumetakiwa kulipa kodi ambayo ni takriban Sh. milioni nne, tumeshaipata ila bado hela ya hifadhi ambayo kwa sasa ni kama miezi sita imepita," alisema.

Askofu huyo alisema taasisi hiyo iliamua kuwasaidia watoto wanaoachwa pembezoni hasa kutoka jamii za wafugaji za Wahadzabe, Wasonyi na watoto yatima.

Akisoma taarifa fupi kwa mgeni rasmi, Mwenyekiti wa Bodi, Mchungaji Isarael Ndalishao, alisema: "Tupo hapa kwa ajili ya kujenga uelewa wa pamoja kwa jamii kuwajali na kuwapenda watu wenye mazingira magumu na kuwajenga watoto kuwa wakombozi wa taifa letu kwa kuwalea kwenye misingi bora na maadili."

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mgwhira, alisema atafuatilia vikwazo vilivyoibuka ili kufahamu sheria na taratibu zilizokwamisha vyakula hivyo vya msaada kufika kwa walengwa.

"Kama mlivyosema, mmekuwa mkishirikiana vyema na serikali kuingiza vyakula vya msaada na mmekuwa mkisamehewa kodi, lakini mwaka huu imeshindikana, labda ipo sababu ya msingi ambayo nitakaa na maofsa wa TRA kufahamu nini kimezuia ninyi kupata msaada huo," aliahidi.



Watalii kutoka Marekani ambao baadhi yao ni wenye ulemavu, wakijiandaa kwa ajili ya kuanza ziara ya siku sita ya kupanda Mlima Kilimanjaro, katika lango la Marangu, mkoani Kilimanjaro, juzi. Ziara hiyo inaratibiwa na kampuni ya Popote Afrika Adventure.
**PICHA: ASRAJ MVUNGI**

# NIDA, TRA wanyooshewa kidole madai ya kukamilisha uwekezaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKALA wa Usajili wa Biashara (Brela), Mamlaka ya Vitambulisho Tanzania (NIDA) na Mamlaka ya Mapato (TRA), wamedaiwa kuwa chanzo cha ukwamishaji wa shughuli za uwekezaji nchini.

Wadau wa sekta hiyo pia wameishauri serikali kuangalia upya utoaji wa leseni za biashara na vibali mbalimbali hasa kwa wawekezaji ili kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Mwenyekiti Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Mkoa wa Kilimanjaro, David Shilatu, alitoa ushauri huo katika kilele cha Wiki ya Sheria. "Mamlaka hizi pamoja na kazi ngumu zinazofanya, sisi mawakili wa kujitegemea ambao ndiyo tupo nyuma ya uandikishaji wa kampuni nyingi za kibiashara nchini, tunafahamu ni kwa kiasi gani hali ya uandikishaji wa biashara ilivyo ngumu zaidi wakati huu kuliko wakati mwingine.

"Baadhi ya mawakili wamekuwa wakikimbia kazi hizo kwa kuhofia kuitwa tapeli," alilalamika.

Alidai kuwa TRA haina ushirikishaji bora wa namna ya ulipaji wa kodi na badala yake wataalamu hao wamekuwa wakiwawinda wafanyabiashara na wawekezaji, jambo ambalo likifanyiwa kazi na kujenga uelewa wa pamoja, litaleta mabadiliko katika sekta ya uwekezaji.

Mgeni rasmi katika shughuli hiyo, Jaji Mfawidhi wa Mahakamu Kuu Kanda ya Moshi, Beatrice Mutungi, aliwataka wadau mbalimbali kushirikiana kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kumaliza kesi zinazohusiana na biashara.

"Tumeweka utaratibu wa kuhakikisha kesi zote zinamalizika kwa wakati, hasa zinazohusiana na biashara ili mwekezaji kuendelea na uwekezaji, hivyo kuleta matokeo yaliyokusudiwa na serikali," alisema. Akitoa salamu za viongozi wa dini, Askofu kutoka Kanisa la EAGT, Reuben Mollel, aliiomba mahakama kushughulikia rushwa iliyoota mizizi kwa baadhi ya watendaji wa serikali.

"Wapo baadhi ya watendaji wa mahakama bado si waaminifu na wamekuwa wakitumia rushwa na kupoteza haki za watu, jambo ambalo hupoteza uaminifu kwa wananchi juu ya mhimili huo,"

# Chanzo unywaji duni wa maziwa chatajwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

GHARAMA kubwa za lishe, huduma sanjari na uelewa finyu wa mbinu endelevu za ufugaji vimetajwa kuwa chanzo cha Watanzania kushindwa kufika lengo la kunywa lita 200 za maziwa kwa mwaka.

Septemba mwaka jana Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mgwhira, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, walizindua jukwaa la unywaji wa maziwa mkoani hapa huku wakieleza kuwa bado Watanzania hawajafikia lengo la unywaji wa maziwa.

Walibainisha kuwa takwimu zinaonyesha hadi sasa Mtanzania anakunywa lita 49 kwa mwaka.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Mwika(Mwidefu), Freckson Mlay, alibainisha vikwazo vinavyochangia hali hiyo jana wakati wa uzinduzi wa kituo cha kusaidia wafugaji kupata huduma kwa karibu na kwa haraka zaidi.

"Mbali na vikwazo vinavyowakabili wafugaji, pia baadhi ya wataalamu wanakabiliwa na tatizo la uwezo mdogo hasa wa kiteknolojia kuendesha mitambo ya usindikaji wa kisasa na uwezo katika kutafuta masoko ya bidhaa zilizosindikwa.

"Kituo hiki kimetumia gharama ya Sh. milioni 250, kikiwa na lengo la kuwasaidia wafugaji kupata mahitaji yao kwa karibu zaidi, kupata utaalamu namna bora ya kufuga na kuleta tija kwenye jamii,"alisema.

Krzysztof Buzalsk, Balozi wa Poland nchini, alisema serikali ya nchi yake itajitaidi kuhakikisha inaweka misingi imara kwa wafugaji kuboresha sekta ya maziwa.

"Tutashirikiana katika miradi mbalimbali iliyopo nchini Tanzania katika kuhakikisha tunaleta mageuzi kwenye sekta ya maziwa ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla," aliahidi.

Daniel Shayo, mmoja wa wafugaji, alisema bado wanakabiliwa na ukosefu wa elimu ya kutosha juu ufugaji wa kisasa wenye tija kwa jamii, utakaosaidia kuzalisha maziwa bora na kuongeza kipato chao.



Waja na makakati mpya kwa ujasiriamali wenye ulemavu

Ukurasa 15

UCHUMI



# BUFE

Ijumaa Februari 7, 2020
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## Waziri Dk. Kalemani 'mguu kwa mguu' kusimamia umeme

Ukurasa 16



# WATOTO WANNE WATELEKEZWA KWA KISA 'KODI YA MEZA' HAYUPO BABA WALA MAMA

Ukurasa 14

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Watoto wanne wateleke ‘kodi ya meza’ hayupo b

• Wahamia jalalani, majirani wawanusuru • Yupo w
• Wa miaka 12 afunguka ya ajabu kwao • DC ash



Watoto wanaodaiwa kutelekezwa na mandhari ya makazi yao kama walivyokutwa na mwandishi. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

**Na Neema Hussein, KATAVI**

KATAVI, mkoa wenye neema ya kiuchumi, ikiwamo uzalishaji vyakula shambani.

Hata hivyo, unaangukia katika kasoro kwamba baadhi ya wazazi hawawajali watoto waliowazaa na wanasahau uchungu walioupata katika mchakato wa uzazi huo.

Kumekuwapo wimbi la wazazi kutelekeza watoto na kuamua kutokomea kusikojulikana. Ndilo liliko katika Kata ya Kazima, Manispaa ya Mpanda, baada ya watoto watano kukimbiwa na wazazi wawili, wakiachwa katika mazingira hatarishi.

Nipashe lilifanikiwa kufika katika makazi ya watoto hao na kuzungumza na baadhi ya majirani, kuhusu uhalisia wa maisha ya watoto hao tangu kutelekezwa na wazazi.

**MWENYEKITI MTAA**

Flaviana Kisalala, ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Kazima, anayekiri kupokea familia hiyo ya watoto watano iliyofikishwa kwake na majirani waliokuwa wanawasaidia, tangu baba yao kuondoka.

“Ilikuwa saa tatu asubuhi nilipata wageni waliokuwa wamama watatu, wakajitambulisha kuwa ni wakazi wa mtaa wangu, wakasema huko kwao kuna watoto watano wametelekezwa, baba yao hayupo ana mwezi na mama ana miezi minne,” anaeleza Flaviana.

Anaendelea: “Lengo lao lilikuwa niwape kibali wakachange hela, ili wawasafirishe kwa bibi yao, nikawaambia hapana.”

Mwenyekiti huyo anaendeleza simulizi akisema, aliwaeleza mbadala ni kwamba kama litakuwepo suala la kuwasafirisha, serikali itashughulikia.

Anasimulia kwamba baada ya muda mfupi tena walijitokeza wanaume wawili waliowafikisha watoto hao na kuwataarifu ndio hao waliowataarifu wametelekezwa na ndipo akaanzisha taratibu za kulifikisha kituo cha polisi, kwa hatua zaidi.

**MKASA ULIVYOANZA**

Happynes Alphonce, ni mmoja wa majirani walioshiriki kuwasaidia watoto hao kwa kipindi chote walichotelekezwa. Anaanza nasimulizi ya siku ya kwanza ya baba mzazi wa watoto hao, ambaye alipoanza nao maisha ya ujirani alidai hakuwa na watoto

.“Huyu baba alipohamia hapa, alikuja na mwanamke wake ambaye ni bi mdogo, sio mama mazazi wa hawa watoto. Nilipomuuliza, hivi wewe hauna watoto, akasema mimi sina watoto hata mmoja. Baada ya siku kadhaa, naona watoto wanaletwa hapa,” anasimulia Happynes.

Mama hiyo anasimulia, baada ya kuona watoto alipomhoji na akamjibu kwamba alikuwa anamdanganya, ukweli ana watoto waliokuwa kwa mama yao mzazi.

“Siku nilipoona watoto nikamuuliza vipi hawa watoto wa nani, akasema wangu nilikuwa nakudanganya walikuwa kwa mama yao mzazi ambaye tulishatengana,” anasimulia jirani huyo.

“Yule mke kumbe alikuwa mke wa mtu, mme wake alipojua alikuja kumchukua akabaki yeye na watoto wake hao wa tano maisha yao yalizidi kuwa magumu,” anasimulia mama jirani huyo.

Happyness, baada ya siku chache baba wa watoto hao alifika kwake alikomuachia fedha Sh.5000 za matumizi yeye, anasafiri lakini binafsi hakuwa tayari kwa hilo.

Anasimulia, baada majirani wote kukataa, aliamua kuondoka na akawaachia watoto fedha hiyo Sh. 5000 na ilipoisha watoto waliendelea kuishi katika mazingira magumu, hata kufika hatua majirani walipochukua jukumu la kusaidia kuwalisha. “Nikawauliza watoto baba yenu atarudi kweli leo? Ni mbona muda umeenda? Wale watoto walikuwa kwangu, ikabidi niwambie waende wakalale na kutoka siku hiyo hajarudi hadi leo,” Happynes anasimulia mkasa.

Anasema, baada ya mumewe kurudi safari alichukua jukumu la kuwakusanya watoto hao na akawapeleka kwa Mwenyekiti wa Mtaa, baada ya kuona maisha yao yanazidi kuwa mabaya na nyumba walioishi walipewa na mtu, ambayo kwa sasa imeanguka upande.

“Mume wangu alikuwa safari, aliporudi alikuta watoto wanaokota chakula jalalani, alipata huruma akashauri tuwapeleke kwa Mwenyekiti wa Mtaa, basi tuliwachukuwa tukawapeleka, maana hata hii nyumba baba yao alipewa tu aishi na imeanguka kama unavyoona (anaonyesha kwa kidole),”anaeleza jirani huyo.

**WATOTO WAFUNGUKA**

Rosemary Kipeta (12), ni mtoto wa kwanza anayesema wadogo zake hawana uwezo wa kujieleza kutokana na umri wao, akiwaorodhesha kuwa majina na umri:

Francis (8), Selina (5), Fortunata (2) na Maria mweye umri wa mwaka mmoja na miezi minne. Hakuna kati yao anayesoma.

> **“Mume wangu alikuwa safari, aliporudi alikuta watoto wanaokota chakula jalalani, alipata huruma akashauri tuwapeleke kwa Mwenyekiti wa Mtaa, basi tuliwachukuwa tukawapeleka, maana hata hii nyumba baba yao alipewa tu aishi na imeanguka kama unavyoona (anaonyesha kwa kidole),”anaeleza jirani huyo.**

Kuhusu masomo, anaeleza: “Sisi wawili mwanzo kipindi tunaishi mtaa mwingine, tulikuwa tunasoma, ila baada ya kuhamia huku tuliacha shule.”


Rosemary anasimulia mkasa kwamba kulitokea msuguano kati ya baba na mama yao, uliomfanya mama yao kuchukua hatua ya kuondoka, chanzo kikuu ni baba huyo hakutoa ‘kodi ya meza’ mkasa uliofika hatua ya mbali, ugomvi wa kufikishana kituo cha polisi.

Mtoto huyo, anasimulia kwamba katika msuguano huo hawakufikia muafaka, ndipo alisubiri mumewe katoka na aliwaambia watoto anakwenda kuchukua pesa alikofanya kazi ya kuuza baa, hakurudi tena.

Mtoto huyo anasimulia mkasa ulivyokuwa: “Baba alikuwa kazini kwake, alikuwa fundi ujenzi. Mama akafuata hela kwa baba, akasema

# ezwa kwa kisa aba wala mama

## a mwaka mmoja, shule basi tena ituka na aamua kuinunua kesi



yeye hana hela akamwambia nakuletea watoto wako.

“Mama akatubeba, akatupeleka kwa baba, baba naye akatuambia mfuateni mama yenu.Tukaondoka kumfuata mama tena,” anaeleza Happyness.

Anaendelea kwamba, baba yao aliwauliza alokelekea mama yao, wakamwambia ‘mama kasema anafuata hela kwa bosi wake.”

Kwa mujibu wa Happiness, baba yao aliamua kumtafuta lakini hakumkuta mama huyo kazini.

“Baba alituambia hivi mimi iposiku ntakuja niondoke, ila nitawaacha sehemu nzuri tu yenye watu. Zilipita siku tu, akaja rafiki yake akampitia wakaondoka.”

**USTAWI JAMII**

Bahati Mwailafu, ni Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Katavi, anasema suala la utelekezaji familia katika mkoa huo ni mkubwa na takwimu zinaonyesha mwaka jana kuna jumla ya familia 17 zimetelekezwa.

Anasema, uhalisia uliopo ni kwamba, matukio mengi ya namna hiyo hayaripotiwi rasmi katika mamlaka za kiserikali na kisheria, changamoto kubwa ni jamii kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu ustawii wa familia zao.

“Ni kweli kwamba katika mkoa wa Katavi tuna janga la utelekezaji wa familia na takwimu zinaonyesha mwaka 2019 familia 17 zimetelekezwa,” anasema Bahati.

**DC MPANDA**

Kutokana na uhalisia na maana ya mkasa huo na mingine ya namna hiyo, Nipashe lilimtafuta Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Lilian Matinga kupata ufafanuzi wake, anakiri zilikuwa hazijamfikia aliahidi kulifanyia kazi haraka.

“Nilikuwa sijui, lakini kwa ushauri wangu kwa kuwa hawa watoto ni wadogo, tunaweza kuwapeleka kituo cha kulelea watoto yatima,” anasema Mkuu wa Wilaya.

Anaeleza msimamo wa serikali kwamba wazazi watelekezaji wanapaswa kuwajibishwa kisheria na anahitimisha kwa ahadi ya kuwasaka wakosaji hao.





Mkurugenzi Wa Kituo cha Kulea Watoto Wenye Ulemavu wa akili Emferd, Josephine Bakhita, akiwahudumia baadhi ya kuku alioanza kufuga, ili kusaidia watoto waliopo kituoni hapo **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

# Waja na makakati mpya ujasiriamali kwa mlemavu

**Na Christina Haule, Morogoro**

WATOTO wenye Ulemavu wa akili wanaoishi kwenye kituo cha kuwasaidia kinachojulikana kama Emferd cha mjini hapa, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwamo ukosefu wa taulo za kike za uhakika, huku ujasiriamali ukitajwa kuwa mkombozi wao wa kipekee.

Mkurugenzi wa Emfrefd, Josephine Bakhita, anasema ujasiriamali unaweza kuwasaidia watoto wa kike 19 waliopo kituoni hapo, kama miradi mbalimbali iliyopo kwenye kituo itaboreshwa na kufikia hatua ya ujasiriamali wenye faida.

Bakhita anasema, kutokana na changamoto zinazokikabili kituo hicho, wameanzisha miradi kama ya ufugaji kuku walioko 35 kwa sasa, wanafuga nguruwe, sambamba na bustani ya mboga.

Ahadi yake kupita mipango aliyonayo ni kwamba, kuna kiasi cha kuku 200, nguruwe 350 na mashine ya kumwagilia bustani ya mboga maarufu ‘water pump’wanaweza kukua zaidi kibiashara na kujikuta wanatatua wenyewe baadhi ya changamoto walizo nazo.

Kwa mujibu wa Bakhita, suala la ufugaji kuku katika eneo lao la kituo la mjini, pia litawasaidia kuimarisha afya za watoto kituoni, baada ya kupata mlo kamili wenye mayai. Anasema, manufaa ya sasa kuwa na eneo la bustani wilayani Mvomero, imempa uhakika wanapopata wadau wa kuwasaidia kuwa na mfumo wa umwagiliaji, wanafanya bustani kwa mzunguko wa mwaka mzima na wataweza kuona tija na kuboresha kituo.

Bakhita anasema, ufugaji wa kisasa wa nguruwe unaweza kuwasaidia kupiga hatua kwenye uzalishaji, hivyo kufikia malengo yoyote wanayokusudia.

Bakhita anasema, Emferd inahudumia watoto wenye mahitaji maalum 66 waliopo majumbani kwenye wilaya za Gairo, Kilosa na Mvomero na kwamba watoto 33 wakiwemo wavulana 14 na wasichana 19 wanahudumiwa kituoni hapo.

Hata hivyo, amewaomba wadau kuona haja ya kuwasaidia mabinti kuwa na uhakika wa upatikanaji taulo za kike, kutokana na kulazimika kutumia taulo za asili pindi wanapokosa za kisasa.

Anasema, pamoja na uhamasishaji alioanza kuufanya kwa miaka 28 sasa kuhusu umuhimu wa kuwasaidia wahitaji mahali kokote waliko, watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto ya mtazamo hasi kutoka kwa jamii zinazowaangalia, hata ikawarudisha nyuma katika juhudi za wadau.

Anasema, lengo la asasi hiyo ni kuelimisha na kusaidia wenye ulemavu na kuangalia ustawi wao kwa ujumla, ili kuhakikisha haki zao zinaheshimiwa ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, anazitaja changamoto zingine ni pamoja na huduma hafifu za matibabu, licha ya kuwa na kadi za huduma ya bima ya afya.

Anasema, hilo limewafanya kulazimika kutumia fedha nje ya utaratibu kuwatibu watoto, kutokana na huduma za kadi hizo kutokidhi kiwango kikubwa cha mahitaji yao na wanalazimika kugharamia matibabu za watoto hao.

Anasema mtoto anapoumwa wanalazimika kumkimbiza hospitali, wanapaswa kupewa huduma ya haraka pale wanapokuwa wagonjwa sana, hata kuna matukio ya kiwango hicho tarajiwa cha huduma hakipatikani.

Hivyo, anashauri jamii kujenga tabia ya kuwatembelea watoto wenye ulemavu, kwani wanahitaji faraja, ikiwamo kutembelewa na kupewa baadhi ya huduma.

Mratibu wa Emferd, Sylivester Zacharia, anaiomba serikali, watu binafsi na taasisi zisizo za kiserikali, kuguswa na kutoa misaada kwa wahitaji, ikiwamo vifaa kama baiskeli za miguu mitatu za kuwawezesha kwenda shule na kurudi huku wakijiandaa kujisaidia wenyewe hapo baadae

BIASHARA

# Waziri Dk. Kalemani 'mguu kwa mguu' kusimamia umeme machimbo madogo

- Aiagiza Tanesco iwe kote mfano wa Geita
- Aahidiwa gharama ndogo, ajira, kodi juu
- DC adai kufuatilia utekelezaji kila kona

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UCHIMBAJI mdogo wa madini nchini, umekuwa nguzo muhimu ya uchumi kwa wananchi na hasa wakazi wa vijijini, ingawa mchango wa uchimbaji mdogo katika uzalishaji madini na kuliingizia taifa fedha za kigeni, bado si wa ngazi nzuri zaidi. mdogo kulinganisha na uchimbaji mkubwa.

Pia, uchimbaji mdogo unatoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania wanaokadiriwa kufika 680,000 ukilinganisha na wastani wa Watanzania 8,800 walioajiriwa na wachimbaji wakubwa.

Kila mchimbaji mdogo mmoja, huzalisha ajira zisizo za moja kwa moja nne na kuifanya sekta ya uchimbaji mdogo kuajiri Watanzania milioni tatu.

**UHALISIA WAKE**

Licha ya uchimbaji huo mdogo una mchango mkubwa kwenye maisha ya wakazi wengi vijijini, hasa wanaozunguka migodini, sekta bado inalalamikiwa kuleta athari katika mazingira na jamii, kwa 'kumwaga sumu' za kukamatia madini ya thamani katika maeneo mbalimbali ya migodi.

Ni uzalishaji mdogo wa madini unaofanyika katika mazingira ya viwango vya chini kiafya na usalama kazini, uharibifu mazingira, kuzalisha ajira kwa watoto chini ya miaka 18 na kuleta matatizo katika jamii, kama vile migogoro ya ardhi.

Ingawa Sheria na Kanuni zinazoongoza sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini, zimetungwa vizuri na kiuhalisia, shughuli nyingi za wachimbaji wadogo sio rasmi na hufanyika katika maeneo mengi yasiyofikika kirahisi na mamlaka za serikali.

Wachimbaji wadogo wa madini wamekuwa wakitumia nguvu nyingi katika shughuli zao, huku wakiambulia kidogo, ikilinganishwa na nguvu walizotumia kufanikisha wanachokifanya.

Hiyo, inaelezwa kuchangia sekta hiyo kushindwa kukua na kufikia uchimbaji wa kati, hata kubeba sura ya kuwa kimbilio la Watanzania wengu kimaslahi, japo wametumia nguvu nyingi, kupata mali kidogo.

Wachimbaji wadogo wamekuwa wakionyesha ushirikiano wao kwenye jamii, hasa kwa kusaidia sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa na dawati, afya, maji na miundombinu ya barabara.

Serikali nayo imeanza utaratibu wa kuwapelekea huduma ya nishati ya umeme, wachimbaji wadogo waliko, lengo ni kuwapunguzia gharama za uendeshaji majukumu ya uchimbaji migodi, kunuia kufikia uchimbaji wakati, ifikapo mwaka 2025.

Zinapoorodheshwa maeneo ya mageuzi, Wilaya ya Kahama imo katika maeneo yanayokua kwa kasi nchini, hasa katika sekta ya madini ikijumuisha mahsusi wachimbaji wadogo na wakubwa.

Hapo katika nafasi ya kipekee, imo migodi mikubwa ya kampuni za Barrick na Acacia, Bulyanhuru na Buzwagi, ambako katika sura nyinginezo wakitumia zana duni wakati wa uchimbaji madini.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (mwenye shati bluu), akionyeshwa jinsi umeme unavyosaidia kurahisisha kazi ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika mgodi wa Mwabomba wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Endapo migodi yote na viwanda vya uchenjuaji madini vitafungwa nishati ya umeme, hakuna mchanga wa dhahabu utakaosafirishwa kwenda kuchenjuliwa wilaya na mikoa jirani ambako halmashauri imekuwa ikipoteza mapato makubwa na kupata kidogo," anasema Manjonjo.**

**MWENYEKITI WACHIMBAJI**

Diwani wa Kata ya Idahina katika Halmashauri ya Ushetu, mwenye wadhifa wa Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Mgodi wa Mwabomba, Yuda Manjonjo, anasema anajaribu kudokeza uhalisi ulioko.

Anasema, katika Kata ya Idahina kuna viwanda vya uchenjuaji madini 11 vinavyohitaji umeme, vivyo hivyo biashara nyingi zilizoko katika kaya hiyo na Mwabomba, hawana umeme na wanatumia mbadala wa jenereta na vyanzo vya jua, kuendesha biashara zao, hali inayowapa gaharama kubwa.

Manjonjo anasema, endapo viwanda vya uchenjuaji madini vitafungiwa umeme, anaamini mapato ya halmashauri na serikali yataongezeka kwa wastani wa kutoka Sh. milioni 37 hadi milioni 50.

Anaeleza adha iliyopo ni kwamba, mchanga wa madini ya dhahabu umekuwa ukisafirishwa kutoka kata za Idahina na Mwabomba hadi mikoa jirani kwenda kuchenjuliwa na kusababisha mapato ya halmashauri na serikali kuu kupungua, badala ya kuongezeka.

"Endapo migodi yote na viwanda vya uchenjuaji madini vitafungwa nishati ya umeme, hakuna mchanga wa dhahabu utakaosafirishwa kwenda kuchenjuliwa wilaya na mikoa jirani ambako halmashauri imekuwa ikipoteza mapato makubwa na kupata kidogo," anasema Manjonjo.

"Tumekuwa tukipoteza mapato mengi hasa tunapokuwa tunasafirisha mchanga wa madini kwa ajili ya uchenjuaji. Tukuombe Waziri wa Nishati, kuhakikisha migodi midogo yote na viwanda vya uchenjuaji madini vinapata umeme kwa ajili ya manufaa ya halmashauri na wananchi wanaozunguka migodi hii," anasema.



Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akimkabidhi Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kahama Mji, Clemensi Mkusa, hundi ya ushuru wa huduma kutoka mgodi wa Buzwagi.

**WAZIRI NISHATI**

Dk. Medard Kalemani, ni Waziri wa Nishati, anayewatetea wachimbaji wadogo nchini, kwamba wamekuwa na mchango mkubwa kwenye pato la taifa, lakini katika sura ya pili ya shilingi wanakabiliwa na changamoto kubwa, ikiwemo ukosefu wa nishati umeme kufanyia kasi katika maeneo yao ya migodi midogo.

Anasema, hilo limewafanya watumie nguvu au gharama nyingi kuendesha shughuli zao migodini na wanachoambulia ni kidogo zaidi, kulinganisha na wanachokiwekeza kazini.

"Tunataka wachimbaji wadogo wote nchi nzima wasiendelee kuwa wadogo tena, ili uchimbaji wao uwe na manufaa na tija kwenye Taifa kama walivyo wachimbaji wengine wakubwa. Lazima tuhakikishe tunawafungia nishati ya huduma ya umeme," anasema Dk. Kalemani.

"Hata wachimbaji wakubwa mnaowaona leo Barrick na Acacia, nao walianza kuwa wachimbaji wadogo na matumaini ya serikali ni kuona, wachimbaji wadogo nchini wanakuwa wawekezaji wakubwa kwa kuwapunguzia gharama za uendeshaji," anafafanua.

Dk.Kalemani, anamtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani Kahama, Mhandisi King Fokanyam kupeleka nishati hiyo kwa wachimbaji wadogo jirani, ili waondokane na adha ya gharama kubwa za uendeshaji migodi yao.

Katika maelekezo yake ni kwamba, meneja huyo wa Tanesco, afanye upembuzi wa sehemu zote zenye wachimbaji wadogo na kuwapelekea umeme, katika namna ambavyo Mkoa wa Geita ulivyofikishiwa huduma hiyo, kwenye migodi yote 36



Dk. Kalemani anasema hadi sasa katika idadi ya migodi midogo zaidi ya 136, wachimbaji wake wadogo wameshanufaika kwa kupatiwa umeme.

Pia, anataja mwaka jana katika Mgodi wa Mwakitolo na mwaka huu mgodi wa Mwabomba, vyote katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, vilipatiwa umeme.

**MENEJA TANESCO**

Awali katika taarifa yake ya usambazaji umeme, Meneja wa Tanesco Mkoa Shinyanga, Mhandisi Narowil Sabaya, anasema Mkoa Shinyanga una vijiji 509 na kati yake, vijiji 171 vimekwishapata umeme na vingine 318 mpaka sasa havijapata nishati hiyo.

Pia anasema, Shinyanga ina jumla ya kata 130, kati yake 93 zina umeme wa uhakika na 37 hazina umeme. Katika hilo, Kahama Mjini, wilaya alikotembelea Waziri Dk. Kalemani, kuna vijiji 249, kati yake 59 vinapata huduma hiyo na 190 havipati.

Mhandisi Sabaya, anasema Wilaya ya Kishapu ina jumla ya kata 29 na vijiji 117. Hapo kuna kata 22 zenye umeme na saba hazina huduma hiyo, huku kukiwapo vijiji 56 vyenye nishati hiyo na 61 hazina.

**VIWANDA MADINI**

Saidi Kweji, ni mmiliki wa kiwanda cha Kweji kilichopo kijijini Mwabomba, Kata ya Idahina, anasema kabla ya kufungiwa nishati ya umeme, walitumia mafuta zaidi ya lita 40 kwa siku na kila mwezi iliwagharimu fedha zaidi ya shilingi milioni tatu.

Rai yake ni kwamba, endapo watapata huduma ya umeme wa uhakika, wataongeza shughuli za uzalishaji na kupunguza gharama za uendeshaji kiwanda hicho kilichoanza kazi mwaka jana. Kwa mujibu wa Kweji, tayari kiwanda hicho kimeshatoa mrahaba wa zaidi ya Sh. milioni 37na Sh. milioni 1.5, ambayo ni ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoa Shinyanga.

"Waziri kama tutapata huduma ya umeme wa uhakika, tutaongeza ajira kwa vijana wanaozunguka migodi midogo na viwanda vyetu tulivyo navyo kutoka wafanyakazi 50 waliopo hadi kufikia wafanyakazi 100 na tutaongeza mashine nyingine kwa ajili ya kuongeza uzalishaji," anaeleza Kweji.

**DC KAHAMA**

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, anaahidi kufuatilia hilo, kuhakikisjha kwamba vijiji vyote 54 vilivyoko katika Halmashauri ya Ushetu, vinapata nishati ya umeme ifikapo Juni Mosi ya mwaka huu.

Anaeleza kwamba mpaka sasa, kati ya viijiji 54 vilivyopo, 20 vimekwishapata nishati ya umeme ambayo ni sawa na asilimia 53 ya utekelezaji wa miradi anaahidi kuhakikisha maeneo yote muhimu yanapata umeme, hasa iliko migodi ya wachimbaji wadogo.

***Soma zaidi uk. 18***

# BIASHARA KATIKA PICHA



Mkuu wa Idara ya huduma za kifedha Benki ya NMB, Linda Teggisa (Kulia) akifafanua kuhusu bidhaa mbalimbali za benki hiyo kwenye mkutano wa wadau wa bima kubwa uliofanyika Jijini Dodoma. Kushoto Ni mkurugenzi Mkuu wa Africa Trade Insurance Agency Tanzania *(ATI) ,Tusikile Kibonde



Mchuuzi wa mananasi akisubiri wateja kando ya barabara ya Uhuru, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Nanasi mmoja linauzwa kwa bei ya 500/- hadi 2,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mchoma mahindi mabichi, akimhudumia mteja wake nje lango kuu la kuingia viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

BIASHARA

Na Shaban Njia, KAHAMA

WAZIRI BITEKO AWANASA 'LIVE'...

# Wizi dhahabu unavyofa bubu vyanaswa kuhada

- Wanakijiji wafunguka njama zilizojificha
- Wadai kutosikilizwa hadi alipoibuka waziri
- Viwanda majumba, maji kemikali mitaani



Waziri wa Madini, Doto Biteko (aliyeinamisha uso) na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bunango, Kanjanja Kanjanja, wakishirikiana kubeba mchanga wa madini uliokuwa unachenjuliwa kwenye kiwanda bubu kijijini. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**



SHINYANGA na Geita ni kati ya mikoa yenye migodi midogo mingi na inayokuwa kwa kasi kiuchumi. Geita ina migodi midogo 36 ambayo ina umeme wa uhakika na Shinyanga, kazi hiyo inaendelea kuanzia migodi ya wa Mwabomba na Mwakitolio.

Ni dira nzuri inayoashiria hatua nzuri ya maendeleo, kuanzia msukumo rasmi wa serikali. Haya hivyo, waswahili wana usemi 'kizuri hakikosi kasoro.'

Licha ya hatua nzuri kufanikishwa, bado wadau hao wa uchimbaji wadogo na wakubwa, wanakabiliwa na lawama za kuibia serikali madini, huku wakizikera jamii zao, hali inayoipotezea serikali mapato. Kwa vipi?

**MADINI FEKI?**

Kuna kashfa ya kufunguliwa viwanda bubu katika makazi ya sehemu mbalimbali, zikitumia mbinu za kuhadaa ukweli na kuingizwa matumizi ya 'steelwire' (za kuosha vyombo)kwenye mashine za uchenjuaji madini.

Mwaka jana, Waziri wa Madini, Sensilaus Nyingo, alifanya ziara kwenye baadhi ya viwanda vya uchenjuaji madini, maarufu 'elution plant' wilayani Kahama, walipobaini kuwapo baadhi ya wamiliki wa viwanda waadilifu na wamekuwa wakiwaibia wateja wao madini mbadala usio sahihi.

Katika siku ya mwisho mwaka jana, Desemba 31, Naibu Waziri wa Madini, Doto Biteko, alifanya ziara ya kushitukiza katika kijiji Bunango, Kata ya Bugalama, iliyoko katika Halmashauri ya Msalala na kubaini kiwanda bubu cha uchenjuaji madini, kikitiririsha maji yenye kemikali kwenye makazi ya wananchi.

Ziara ya Biteko ilimuwesha kutia mbaroni mifuko zaidi ya 35 ikiwa na madini 'carbon; zinazodhaniwa kuwa na madini ya dhahabu katika kiwanda hicho, huku mashine yenye uwezo wa kubeba kilo 500 za 'carbon' ikiwa malighafi kwa ajili ya uzalishaji, ili kazi ianze.

Vilevile, mwishoni mwa mwezi mmoja baadaye, kwa maana ya mwezu uliopita, Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, alinasa kiwanda kilichopo katila kaya ya Kata ya Malunga, katika Halmashauri ya Mji Kahama, ikiweka 'steel wire' katika mitambo inayohisiwa kuwaibia wachimbaji wadogo wamadini waliofika kuchenjua.

**WAZIRI BITEKO**

Doto Biteko, Waziri wa Madini anasema vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wamiliki wa viwanda vya uchenjuaji madini, kuendelea kuiibia serikali na wachimbaji wadogo, kwa kuweka 'steelwire' kwenye mashine akivitafsiri ni vitendo vya kinyama na havivumiliki.

"Nilishasema, ukikubali kuwa mfanyabiashara wa madini, unakuwa unakaribisha umaskini au kwenda jela, hasa kwa wale ambao wamekuwa wakifanya biashara kwa njia ya udanganyifu. Nitoe wito kwa wafanyabiashara wote wanaomiliki viwanda bubu kujisalimisha haraka kabla hatujaanza msako," anang'aka Waziri Biteko.

> "Kiwanda hiki kipo hapa katika nyumba hii tangu mwezi Julai mwaka jana, huku kikiendelea kufanya kazi. Serikali imepoteza mapato mengi kwa kutochukua hatua za haraka. Tutachukua hatua kali za kisheria kwa miliki ya mtambo huu na nyumba hii," anasema Waziri Biteko.

Anaendelea:" Niwaagize viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mitaa, kata hadi mkoa, kuhakikisha wanakagua viwanda vya uchenjuaji madini, kama wamiliki wake wana vibali, ili kuzuia athari zitokanazo na kemikali zinazomwagwa ovyo na vilivyopo katikati ya makazi."

Biteko anasema, katika Mkoa wa Shinyanga hususani katika Wilaya ya Kahama, bado kuna wafanyabiashara wa dhahabu wasiotaka kuzingatia sheria za madini na mwaka jana pekee, kuna viwanda viwili vilibainika kukiuka sheria na uwepo wa viwanda bubu. Katika msimamo wake anahamisha agizo la utekelezaji kwa Jeshi la Polisi, kumkamata na kumhoji kupata ukweli kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bunango Kanjanja Kanjanja, baada kuhusishwa kushirikiana



Moja ya mashine iliyokamatwa na Waziri Doto Biteko, katika 'kiwanda bubu' kinachodaiwa kutumika kutapeli wachimbaji dhahabu.

# anyika viwanda aa kwa 'steelwire'




Meneja wa Kiwanda cha Uchenjuaji Madini, Amina Hussein, akipandishwa kwenye gari la polisi, kwa dai la 'steelwire' kwenye mashine ya uchenjauji adini.

na watoroshaji madini ya dhahabu, kwa kufungua kiwanda bubu vya kuchenjua wa madini.

Biteko anasema, Ofisa Mtendaji wa Kijiji amekuwa wakipewa taarifa kuhusu kiwanda hicho na viongozi wengine wa kijiji, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa, kuhusu uwepo wa kiwanda hicho.

Anasema, serikali imekuwa ikiiboresha sekta ya madini kwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini wa Kahama, lakini bado kuna baadhi wanaoendelea kuiibia serikali mapato, kwa kuanzisha viwanda bubu kwenye makazi yao.

"Kiwanda hiki kipo hapa katika nyumba hii tangu mwezi Julai mwaka jana, huku kikiendelea kufanya kazi. Serikali imepoteza mapato mengi kwa kutochukua hatua za haraka. Tutachukua hatua kali za kisheria kwa miliki ya mtambo huu na nyumba hii," anasema Waziri Biteko.

Hata hivyo Biteko, anawataka viongozi wa vijiji na mitaa wilayani Kahama, ambako naye ni mwenyeji na jirani na kunakopatikana ubunge wake, wawafichue wafanyabiashara haramu ya madini, wanaoendesha shughuli zao katika makazi ya watu na kuishia kuikosesha serikali mapato.

Pia, Biteko anaagiza viongozi wa mkoa Shinyanga kuthibiti biashara haramu ya madini inayoendelea kushamiri katika maeneo mbalimbali, akisema mpaka wakati huo walishakamata viwanda bubu viwili vya uchenjuaji dhahabu.

**BALOZI KITONGOJI**

Kiongozi katika eneo jirani kulikokabiliwa na mkasa (jina tunalo), anasema alishatoa taarifa kwa mamlaka za kisheria kuhusiana na uwepo wa kiwanda hicho katika eneo lake, lakini hakuona hatua zilizochukuliwa kwa wahusika.

"Kiwanda hiki kipo katika nyumba hii tangu Julai mwaka jana. Kuna vijana wanne ambao walikuwa wakifanya shughuli ya kuchenjua dhahabu hapa. Viongozi wote wa eneo hili wanajua na tumelalamika sana kuhusiana kumwagwa ovyo kwa maji yenye kemikali kwenye makazi yetu" anasema Masoud Bakari, mkazi wa eneo hilo.

Anasema ni kiwanda bubu kilichokamatwa na waziri, kipo katikati ya makazi ya watu na kimekuwa kikifanya kazi kila siku, ikiendana na kumwaga majitaka zenye kemikali kiholela, bila ya kujali uwepo wa watoto wadogo jirani.

"Mheshimiwa Waziri, kiwanda hiki kipo kwenye nyumba hii tangu mwaka 2019 na kimekuwa kikifanya kazi kila siku...kinachotuumiza zaidi, ni pale kinapotiririsha maji yenye sumu, ambayo huchezewa na watoto wadogo

"Tumeshatoa taarifa hizi kwa uongozi wa serikali za kata, lakini hakuna hatua yoyote iliyoweza kuchukuliwa kwa wamiliki wa kiwanda hiki, hadi hivi sasa wewe unafika katika kiwanda na kuwawajibisha kisheria.

**OFISA MADINI (M)**

Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga ni Mhandisi Joseph Kumburu, anayesema katika kupambana na utoroshaji na wizi wa madini wa kuweka 'steelwire' kwenye mashine wakati wa uchenjuaji na ufunguzi wa viwanda bubu, wamekuwa wakishirikana na vyombo vya ulinzi na usalama kupambana na ujalifu huo.

Kumburu anasema, kiwanda cha uchenjuaji kilichonaswa ni sehemu ya viwanda ambavyo vimekuwa vikiweka 'steelwire; kwenye mashine wakati wa uchenjuaji madini na kuwaibia wachimbaji wadogo, huku serikali nayo ikipotezea mapato.

Anasema, Januari 31 mwaka huu majira ya saa mbili usiku, waliweka mtego na kufanikiwa kumkamata Meneja wa Miwanda, baada ya kubainika wanaweka 'steelwire' kwenye mashine wakati wa uchenjuaji madini.

Kumburu anaeleza, baada ya kumkamata na kutolewa 'steelwire' hiyo na kutishiwa na kuchomwa, ilipatikana dhahabu yenye uzito wa gramu 78.9 sawa na asilimia 90, yenye thamani ya Sh. 8,302,277.34, huku wakiokoa mrabaha wa serikali wa Sh.581,159.41.

Kumburu anasimulia mkasa kuwa, walipokuwa wanakagua kujiridhisha, mfanyakazi mmoja ambaye ni fundi umeme na mwendeshaji mitambo (operator) alitoroka baada ya kubainika kuhusika na tukio hilo, hali iliyowalazimu kuwashikilia wenzake.

"Wamiliki viwanda wamekuwa wakivunja sheria ya Madini kifungu cha sita cha mwaka 2010 na kifungu cha 30 cha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji wa Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi... Kanuni za Masoko za Mwaka 2019," anasema Ofisa Madini, anayehitimisha kwa kauli :" Alikuwa anatorosha dhahabu na alikuwa anaenda kufanya biashara nje ya soko."

**SOKO MADINI**

Emmanuel Kidenya ni Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Madini, Soko la Dhahabu Kahama. Kwanza, anaipongeza serikali kwa kuwa makini na kuchukua hatua kwa wafanyabiashara wasio waaminifu anaiomba serikali kubioresha mfumo wa udhibiti wa vitendo vya namna hiyo.

Anasema mchimbaji madini anatumia nguvu nyingi kuyatafuta na anapofika viwandani kupata soko la fedha za kufuta jasho tena anaibiwa tena, hivyo anaiomba serikali katika nafasi ya mlezi wa wachimbaji, idhibiti hilo, kuwezesha hata wachimbaji wasihamie mkoa mwingine.



Msimamizi wa kiwanda cha uchenjuaji madini, Jumanne Ndosi, akitoa steelwire yenye dhahabu kwenye mashine. Kando yake ni Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Joseph Kumburu.



Steelwire' yenye dhahabu ikiwa ndani ya kinu cha uchenjuaji madini.

BIASHARA

# Janga la corona China linafungua neema ya biashara kwa Marekani

## • Dalili ajira mpya kumiminika ‘yanukia’

**Na Nimi Mweta**

HOMA ya corona hivi sasa inaitikisha dunia na kuiweka China njia panda kibiashara, utalii na hata uwekezaji. Hilo limeanza kuangaliwa kwa ‘jicho la tatu’ na baadhi ya watendaji wa taifa mahasimu wao kibiashara, Marekani.

Waziri wa Biashara wa Marekani, Wilbur Ross, mwishoni mwa wiki iliyopita aliliambia gazeti mashuhuri la New York Times, kuwa ugonjwa huo unaweza kuleta mazingira mapya ya kuongezeka kwa nafasi za kazi nchini Marekani.

Hapo anamaanisha kwamba wawekezaji wakiondoka China au wakisita kwenda huko. Sababu siyo tu kuenea hivi sasa,ila kuzuka tena siku zijazo.

Sababu ya hisia hiyo ni kuwa, ugonjwa huo umetokana na tabia iliyokithiri ya hoteli za China za barabarani kutumia nyama za wanyamapori wa kila aina.

Historia inaonyesha kuwa, virusi vinavyotoka kwa wanyamapori au ndege wenye uwezo mkubwa wa kustahimili mazingira magumu, kuliko wanyama wanaofugwa, vikiingia kwa binadamu ni janga la aina yake, kama ilivyo sasa kwa homa ya corona.

Mtu akiangalia kwa upande huo, China inaweza kuleta janga lingine muda wowote, kwani mabadiliko ya hali ya hewa kuwa ya joto, yanaimarisha virusi hivyo.

Mashirika kadhaa ya habari yaliyonukuu matamshi ya waziri huyo, yalitofautiana kwa kiasi fulani kuhusu kile alichokisema, kwa kuhoji kama alisema janga hilo, linaweza kurudisha nafasi za kazi Marekani kwenyewe, au Amerika ya Kaskazini kwa jumla.

Kimsingi, ina maana kuongezeka kwa uwekezaji hasa wa viwanda katika eneo lote hilo, hasa Marekani na Canada, ingawa Mexico ni sehemu ya ‘Amerika ya Kaskazini’ kwa maana ya kijiografia na kiuchumi, inahesabiwa na nchi za Amerika ya Kusini.

Siyo mojawapo itakayolengwa na wawekezaji, baada ya mkataba uitwao, Nafta, ambao ni mkataba wa kibiashara wa nchi hizo tatu, Marekani, Canada na Mexico, ambako soko huria iliundwa na kurekebishwa

Bidhaa ikitengenezwa katika nchi mojawapo, inaweza kuuzwa kwingineko bila ya ushuru wa forodha, hali iliyohamisha viwanda vingi kutoka Marekani kwenda Mexico.

Alipoingia madarakani, Rais Donald Trump alianza kutekeleza ahadi yake ya kampeni ya kurekebisha hali hiyo na hivi karibuni, mkataba mpya umetiwa saini unaorudisha ushuru kidogo tu.

Kinachofanya ajira ianze kupatikana kwa wingi zaidi katika ukanda wa Bara Marekani, kwamba China inapoanza kupoteza mvuto wa kuweka viwanda vipya, kazi zitaelekea zaidi Mexico.

Inaelelezwa, Marekani itafaidika zaidi kwa wawekezaji watakaoondoka China na tayari walikuwa na mitambo au miundombinu Marekani, halafu wakapanua shughuli zao kwa kuanzisha matawi China.




Watumishi wa afya, wakiwa katika mavazi maalum ya kujilinda wakilinda eneo la soko la vyakula lililofungwa huko, Wuhan, China. **PICHA ZOTE: MITANDAO.**

> **Tafsiri yake nini? Kuna maana kwamba mwelekeo huo utapungua, kutokana na hatari za milipuko ya magonjwa kuzidi kwa upande wa China, kwani sababu za kimazingira zinaashiria kwamba siyo salama.**

Tafsiri yake nini? Kuna maana kwamba mwelekeo huo utapungua, kutokana na hatari za milipuko ya magonjwa kuzidi kwa upande wa China, kwani sababu za kimazingira zinaashiria kwamba siyo salama.

Matamshi ya Waziri Ross, ni jambo linalopaswa kueleweka vyema kwamba, maana haishii hali halisi iliyoko sasa, kwani hata maradhi hayo yakitatuliwa leo kama yalivyotatuliwa mengine ya kabla, kuna suala la woga wa baadaye.

Wilbur Ross, anaonekana kupata picha kuwa janga la ugonjwa wa corona kwa njia fulani au nyingine ni ‘game changer’ kuwa ushindani wa kibiashara hautakuwa tena kama mwanzoni na kazi zitarudi Amerika ya Kaskazini.

Sababu pekee ya tamati hiyo, tena aliyotaja kwa kujiamini, ni athari tarajiwa za muda mrefu zinazotokana na kuzuka ugonjwa la corona, mustakabali wa mazingira.

Ni kama vile Waziri Ross alikuwa anaitangazia China janga la kiuchumi la muda mrefu, kwani inaweza kupona na kuliondoa gonjwa la corona katika miezi michache ijayo lakini haitapona hofu inayotokana na gonjwa hilo.

**BAADA MUAFAKA**

Mtazamo tofauti ni kwamba, kuna nguvu mpya ya kupambana na China kiuchumi. Hiyo ni baada ya Marekani na China kufikia muafaka wa hatua ya kwanza kutatua mgogoro wa ushuru wa forodha na kutokuwapo mlingano wa biashara.

China imekuwa ikiuza bidhaa nyingi nchini Marekani na kuipatia kiasi cha wastani, Dola za Marekani billion 350 kwa bidhaa zinazouzwa nchini Marekani, kutoka China.

Hata hivyo, wataalamu wanakumbusha kuwa Marekani ina hisa kubwa katika kampuni zinazozalisha kutoka China, hali inayoingiza faida, ila haziongezi ajira nchini Marekani.

Haitakuwa rahisi kwa China kuondoa vihatarishi vya kimazingira vya aina ya corona, kwani itahitaji kwanza kuacha utamaduni wa kutumia nyamapori za aina tofauti kama sehemu ya kinachopatikana katika hoteli na migahawa nchini humo.

Inaelekea hakuna utaratibu wa kuwa na nyama zinazoruhusiwa na zisizoruhudiwa kwa mpangilio wa kitamaduni. Hapo inamaanisha, vitu kama kanuni za dini husika za wenyeji.

Vilevile, China ina serikali yenye nguvu na hata kufanya ‘uamuzi magumu’ na kuyalazimisha miongoni mwa watu na kuna uwezekano wa kuwekwa sheria bayana, kuhusu utumiaji wa wanyamapori, hata ingekuwa ni kufuta matumizi hayo na kubakizawanyama wa kufugwa pekee.

Ina maana kwamba, Marekani kwa sasa intarajiwa kupaa katika ushindani wa uchumi na China, kwani mabadiliko ya mazingira duniani yanaiweka nchi hiyo katika mazingira magumu ya kushindana kiuchumi.

Wakati ushindani upo katika gharama za uzalishaji (mishahara nguvukazi, wataalamu na ununuzi au ubunifu wa teknolojia), sasa kuna tatizo lingine la kuhofia milipuko kama huo, unaoweza kuvuruga mazingira ya ufanyaji biashara kwa miezi kadhaa.

Sababu ni kwamba, kuna kila aina ya vianzio vya ugonjwa kama huo kwani idadi ya wanyama ‘wasio safi’ wanaoliwa nchini humo ni kama haihesabiki na sasa virusi vyao vinajengeka kimazingira, vikihamia kwa watu wanaokula nyama hizo kwa urahisi zaidi, tofauti na ilivyokuwa awali.

Ni mtego wa kimazingira ambao unaweza kuisaidia Marekani kwa kina kuanzia sasa, kampuni kubwa zikianza kupima shughuli zao China na kuzipangua.




Moja ya eneo la kibiashara jijini Wuhan, China.



## HABARI MBEYA

# Madiwani walia na biashara ya ngono

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameanza kutafuta njia za kutokomeza biashara ya ngono inayofanyika katika baadhi ya maeneo ikiwamo eneo la Mafiati baada ya kuelezwa na wananchi kuwa ni keri.

Mjadala wa kupambana na biashara hiyo, uliibuka jana kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo baada ya Diwani wa Forest, Henry Mwangambaku, kudai kuwa biashara hiyo inafanyika kwenye makazi ya watu na kusababisha kondomu zilizotumika kuzagaa mitaani.

Mwangambaku alisema katika eneo la Mafiati inapofanyika biashara hiyo, yametokea matukio mengi ya watoto kukutwa wakipuliza kondomu zilizotumika wakidhani ni mapulizo hali ambayo ni hatari kwa afya zao.

Aliiomba halmashauri kuweka taa katika eneo hilo ili zisaidie kuwaondoa madada poa wanaofanya biashara hiyo kwa maelezo kuwa hawapatani na mwanga na huwa wanapenda kujificha sehemu za giza kama ilivyo sasa kwenye eneo hilo.

"Tunahangaika namna ya kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi katika jiji letu lakini tujaribu kupambana pia na baadhi ya vyanzo. Pale Mafiati kuna biashara haramu ya kina dada kuuza miili yao na ni eneo la makazi ya watu, tunatakiwa tuitokomeze," alisema Mwangambaku.

Diwani wa Sisimba, Geofrey Kajigili, alisema katika baadhi ya miji iliyoendelea duniani, biashara hiyo imehalalishwa na wafanyabiashara hao wanalipa kodi, hivyo akadai kuwa wanaipinga kwa sababu jiji hilo halijaendelea.

Kajigili alisema kutokana na maendeleo kuongezeka ipo siku watatakiwa kutafuta namna ya kuboresha mazingira ya biashara hiyo ili wahusika walipe kodi.

"Huu ni ukweli ambao lazima upingwe kwa sababu ya mazingira yetu na ndio uhalisia wenyewe, ipo siku hata sisi tutakuja kuhalalisha biashara hii," alisema Kajigili.

Baadhi ya madiwani alipinga vikali hoja hiyo ya Kajigili wakidai kuwa biashara hiyo ni haramu kwa mujibu wa sheria za nchi na ni lazima ipingwe kwa namna yoyote. Diwani wa Nsalaga, David Ngongo, alisema Watanzania hawatakiwi kwa namna yoyote kufikiria kuhalalisha biashara hiyo kwa maelezo kuwa ni biashara ambayo inaendana na tamaduni za wazungu na sio tamaduni za waafrika.

Ngogo alisema biashara hiyo pia inaharibu maadili ya watoto ambao wanawashuhudia kinadada wanaofanya biashara hiyo na kwamba ndio maana wakati mwingine wanaongezeka.

Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi, alisema kwa sasa wanashirikiana na Jeshi la Polisi kutokomeza biashara hiyo kwa kuwakamata madada poa wanaojiuza katika eneo la Mafiati na kuwaweka ndani.

Alisema kwa sasa wataanza kufanya kama Jiji la Dodoma walivyofanya na alidai kuwa wao wakiwakamata wanawafikisha mahakamani na kuwafunga miezi isiyopungua miwili na wakishaachiwa hawarudi tena kwenye kazi hiyo.

"Tunashirikiana sana na OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), wamekuwa wakikamatwa na kushughulikiwa na sisi tunatamani sana biashara ile ikome maana tunaokoa vijana wetu wasijiingize huko," alisema Mwashilindi.

Hata hivyo alisema kuweka taa katika eneo la Mafiati ili kuwafukuza haitasaidia kwa maelezo kuwa machangudoa hao wanapenda kukaa kwenye mwanga ili waonekane na wateja wao na hivyo wakiwekewa taa ndio watajiachia zaidi.



Baadhi ya wajasiriamali wadogo wakiendelea na pilika pilika zao za biashara katika eneo ambalo haliruhusiwi kufanya shughuli zozote, nje ya Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya , jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafanya sherehe kwa kupatiwa umeme

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Ipinda katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamefanya sherehe kuishukuru serikali kwa kuwapelekea umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) wakidai kuwa hawakuwahi kuwa na ndoto ya kupata huduma hiyo.

Walifanya sherehe hizo juzi kijijini hapo kwa kuwaalika viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa vya kata hiyo na baadhi ya maofisa wa Jeshi la Magereza wanaosimamia Gereza la Kawetere ambao pia wameguswa na mradi huo.

Msimamizi wa Gereza la Kawetere, James Kandiro, alisema wananchi wa kijiji hicho hawakuwahi kuwa na matumaini ya kupata umeme lakini kwa sasa wameshaletewa na wanaunganishiwa kwenye nyumba zao kwa bei nafuu kuliko maeneo ya mjini.

Alisema kutokana na huduma hiyo wananchi wa Kijiji hicho pamoja na vijiji vingine jirani wameshaanza kuanzisha shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo zinatumia nishati hiyo.

Alisema baadhi wameanza harakati za kuanzisha viwanda vidogo vya kuchomelea vyuma, wengine wameanza kununua mashine za kusaga na kukoboa zinazotumia umeme na baadhi wameanzisha saluni.

"Tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutekeleza ahadi ambazo alituahidi wananchi wake, amekuwa akitekeleza miradi ya barabara, umeme, viwanja vya ndege na sasa ametukumbuka na sisi ambao hatukuwahi kuwa na fikra za kupata umeme sasa nyaya zimesambaa kila kona," alisema Kandiro.

Alisema mbali na kuwaletea umeme huo, pia Rais John Magufuli aliwachangia Sh. milioni 12 alipokuwa ziarani mkoani Mbeya mwanzoni mwa Mei, mwaka jana, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Ipinda.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mathias Mayemba, aliwataka wananchi ambao hawajaunganishiwa huduma hiyo kuendelea kuwasiliana na viongozi kwa kulipia Sh. 27,000 na kwamba wasikubali kuunganishiwa na mtu ambaye hahusiki.

Aliwataka wananchi kuitumia vizuri huduma hiyo kwa kujiletea maendeleo ikiwamo kubuni miradi mbalimbali ili tija ya serikali kuwapelekea huduma hiyo ionekane.

"Tulikuwa tunauona umeme tukienda mjini lakini sasa hivi na sisi tumekumbukwa, hii inaonyesha kuwa ni kweli serikali yetu ya sasa inawajali pia wanyonge, na sasa ili kufaidi huduma hii ni lazima tuungane na Rais wetu kwa kufanya kazi kwa bidii," alisema Mayemba.

Alisema baada ya Serikali kuwapelekea huduma hiyo kwa sasa wanaendelea na harakati za kuanza kujenga Zahanati kijijini hapo ili kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kufuata huduma za Afya katika vijiji jirani.

Naye Theresia Kandonga, miongoni mwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliohudhuria sherehe hiyo, aliwataka wananchi hao kuchangamkia fursa za kiuchumi zitokanazo na umeme.

Aliwataka wananchi hao kutoishia kuipongeza Serikali kwa maneno bali wafanye kazi kwa bidii kama ambavyo rais Magufuli amekuwa akisisitiza mara kwa mara.

# Wajitosa kilimo cha maparachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa kijiji cha Lunwa Kata ya Igurusi, Mbarali mkoani Mbeya, wameamua kujikita kwenye kilimo cha maparachichi wakiamini kuwa zao hilo litawanufaisha na uchumi wa viwanda.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walisema wameamua kulima maparachichi wakiwa na matarajio makubwa ya kuinuka kiuchumi katika maono ya serikali kuhimiza uwekezaji wa viwanda.

Mmoja wa wananchi hao, Meshack Mkwama alisema wameamua kuanza kuchangamkia fursa kwenye kilimo cha maparachichi kutokana zao hilo kuwa na soko kubwa la ndani na nje ya nchi.

Alisema wamejifunza kwa wakulima wa Wilaya ya Rungwe na Mkoa wa Njombe ambao tayari walianza muda mrefu kunufaika na soko la mazao hayo na kwamba na wao wameona wajaribu kuzalisha ili wanufaike pia.

"Sisi tumekuwa tukizalisha mazao ya chakula ambayo ndio hayo tunayatumia kama mazao ya biashara, sasa tumeamua tuanze kuzalisha zao hili na tulifanye kuwa ndio zao letu rasmi la biashara, tutatumia pia kama chakula kwa ajili ya afya," alisema Mkwama.

Naye Yohana Mgulo, ambaye pia ni mkulima, alisema walishaambiwa na wataalamu wa kilimo cha zao hilo kwamba ardhi yao inaweza kustawisha zao hilo na hivyo ndio maana wameamua kuanza kuzalisha.

Aliwaomba wazalishaji wa miche ya maparachichi kupunguza bei ya miche hiyo ili wakulima wengi zaidi wahamasike na kuanza kulima tofauti na sasa ambapo matajiri ndio wanalima zaidi.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole, baada ya kubaini uwapo wa mwamko mkubwa wa wananchi wa kijiji hicho kwenda kununua miche ya matunda kwenye kituo hicho, wameamua kuanza kutoa elimu.

Mtafiti wa matunda kutoka Tari Uyole, Daud Mbogo, alisema kwa sasa wanatarajia kutoa elimu ya kilimo cha matunda kwa wananchi milioni tano wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema elimu hiyo itakuwa endelevu katika maeneo yote ambayo yamebainika kuwa na uwezekano wa zao hilo kustawi na akawataka wananchi kujitokeza kwenda kununua miche iliyofanyiwa utafiti kwenye kituo hicho.





# Watumishi watakiwa kuwa waadilifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, amewataka watumishi wa wizara hiyo kufanya kazi kwa uadilifu ili Tanzania ifikie uchumi wa kati unaotegemea viwanda.

Prof. Shemdoe alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na watumishi hao baada ya makabidhiano ya ofisi na Katibu Mkuu aliyemaliza muda wake Prof. Joseph Buchweishaija, jijini hapa.

Alisema wizara hiyo imebeba ajenda ya serikali ya kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda, ili kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya watu.

"Tujue sisi tumepewa jukumu kubwa ambalo tunapaswa kufanya ili wizara hii itoe matokeo yanayotarajiwa na Rais John Magufuli," alisema.

Alisema watumishi wanapaswa kufanya kazi kwa bidii, weledi na uadilifu ili kuyafikia matarajio hayo.

"Namshukuru Rais kwa kuniamini na kuniona ninafaa na kuteuliwa kwenye wizara hii, ninachowaomba ushirikiano wa kutosha katika utendaji wa kazi kama mlivyoonyesha ushirikiano kwa Katibu Mkuu mstaafu,"alisema.

Aliongeza: "Nawahakikishia kuwapa ushirikiano na wakati wote ofisi yangu itakuwa wazi bila kikwazo chochote muda wote nitapatikana nitakapohitajika."

Naye, Katibu Mkuu aliyemaliza muda wake Prof. Buchweishaija, alisema wizara hiyo ina watu wanaojituma na kufanya kazi kwa bidii na kuwataka kumpa ushirikiano katibu huyo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, akishiriki katika upandaji miti eneo la Mlimwa West, jijini Dodoma jana. Benki hiyo, kwa kushiriki ana wananchi wa eneo hilo na Mtaa ya Swaswa walipanda miti 500 ikiwa ni juhudi za kuunga mkono utunzaji wa mazingira wa Jiji hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge awataka wanawake kugombea uongozi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda, amewataka wanawake kujitokeza kugombea nafasi ya ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu, mwaka huu badala ya kuwa wapiga debe.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA) kwenye ziara waliyoifanya ya kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa na Bunge na miradi inayotekelezwa na serikali ya makao makuu.

Aliwataka kuwa na ujasiri na kujiamini kwenye uchaguzi huo badala ya kuwa wasindikizaji na wapiga debe wa wengine kila unapofika wakati wa chaguzi.

Aliwahimiza kuhakikisha katika uchaguzi huo wanaingia kwenye ushindani wa kugombea nafasi hizo muhimu kwao bila kuhofia. "Mjipange na mjiamini jitokezeni kwa wingi ili mpate uwakilishi kutoka kwenye maeneo," alisema.

Mwakagenda aliwataka viongozi hao kuitumia ziara hiyo waliyoifanya kuwa chachu ya kujiimarisha wao wenyewe pamoja na chama chao.

"Ziara kama hizi ni fursa kwenu ya kujifunza hivyo ninawaomba muitumie kwa malengo ya kujiimarisha kimaendeleo kwa maeneo yenu mnayotoka na kwa maslahi ya chama chetu na si vinginevyo,"alisema.

Kwa upande wake, mmoja wa wanawake hao, Kissa Swilla, aliiomba serikali kuhakikisha kunakuwa na tume huru ya uchaguzi ili taifa lipate viongozi kwa haki.

Kissa aliwatala Watanzania wajitokeze kwenye kujiandikisha na kupiga kura ili waweze kuwachagua viongozi wanaohitajika katika kuhakikisha maendeleo yanakuwapo ndani ya taifa.

# Tanroad yatakiwa kufanya kazi saa 24

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameutaka Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) kufanya kazi usiku na mchana kuweka mawe katika eneo korofi la Barabara ya Dodoma-Iringa eneo la Mpunguzi, ambayo imeharibika na kusababisha magari kukwama.

Katambi alitoa kauli hiyo jana alipotembelea eneo hilo kujionea kutokana na magari kukwama.

Alisema wanatakiwa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha barabara hiyo inaimarika ili kutatua msongamano wa magari kwenye eneo hilo.

Katambi alisema eneo hilo linapaswa kujenga karavati ili kuruhusu maji kupita kutokana na kuwa na mkondo mkubwa wa maji.

Alisema ubovu wa barabara hiyo umetokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha magari kukaa muda mrefu kwenye eneo hilo.

"Katika eneo hili hapajawahi kutokea tatizo kama hili, lakini mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha madhara haya, tukumbuke kuwa eneo hili lilikuwa ni mkondo wa maji, lakini baada ya lami kuwekwa kalavati halijawekwa, sasa mvua zikizidi maji yanafuata mkondo wake," alisema Katambi.

Alisema eneo lenye shida ni kutoka Nyang'hali hadi Chipogolo na barabara imeharibika kwa kiwango kikubwa.

Naye, Mhandisi matengenezo wa Tanroads, James Ngoswe, alisema awali katika eneo hilo hapakuwa na shida yoyote, lakini baada ya mvua kubwa kunyesha mkondo wa maji umechimba barabara na kusababisha madhara hayo.

"Tumeshachukua hatua tunapeleka mawe ili kujaza katika eneo la barabara lililochimbwa na maji ya mvua zinazoendelea kunyesha, jana tulileta lori tisa za mawe, asubuhi tumeleta lori nne na kuna nyingine mbili zinakuja na mawe yote hayo tutayatumia kujaza hii sehemu kisha tutaweka changarawe laini ili magari yapite wakati tunasubiri hatua nyingine kuchukuliwa," alisema Ngowe.

Mmoja wa madereva, Charles John, alisema madereva, abiria na wakazi wa eneo hilo wanashirikiana kwa pamoja ili kujaza mawe yaliyofikishwa na Tanroads katika eneo hilo.

"Wakati tunaendelea kuweka mawe kuna upande magari madogo kama costa na mengine yanaweza kupita kwa kupokezana, likipita moja lingine litasubiria, huo ndio utaratibu tunaoutumia," alisema.

Kwa upande wake, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliitaka Tanroads kuchukua tahadhari mapema kwa kuwa yapo maeneo yanayoonekana kwa macho kuwa ni mazuri, lakini ni mabovu.



# SMZ yatekeleza malengo ya Mapinduzi 1964

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohammed Aboud Mohammed, amesema serikali katika awamu zote imeendelea kutekeleza malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 yaliyoachwa na marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Kauli hiyo aliitoa wakati akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya Haji, aliyetaka kujua serikali zinayaendeleza vipi malengo ya Mapinduzi hayo yaliyoachwa na Hayati Mzee Abeid Amani Karume.

Alisema Mapinduzi hayo yaliondoa utawala wa kikoloni katika visiwa vya Unguja na Pemba na yalikuwa ni chachu ya harakati za maendeleo ikiwamo elimu na afya bora.

Aboud alisema serikali ya awamu ya saba inachukua jitihada kuhakikisha inafanikisha malengo hayo.

Akijibu swali la kujengwa hoteli katika eneo la Mangapwani lilowekwa jiwe la msingi na marehemu Karume, Waziri Aboud alisema ujenzi huo uliratibiwa kujengwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo serikali itaiandikia barua serikali hiyo ili kujua ujenzi huo umefikia wapi.

Alieleza kuwa historia inaonyesha kuwa jiwe hilo la msingi liliwekwa katika kipindi cha miaka ya 1969/1970.

Naye, Naibu waziri wa wizara hiyo, Mihayo Juma Nunga, akijibu swali la msingi lililoulizwa na Mwakilishi huyo, aliyetaka kujua serikali inatoa kauli gani kuhusu bango la marehemu Karume linalosema marehemu Karume ameuawa kilichokufa ni kiwiliwili mawazo na fikra zake zipo na zinaendelea kudumishwa milele.

Alisema, serikali inaendeleza usemi huo kwa vitendo kwa kuimarisha na kudumisha amani na utulivu na kutoa huduma bora za kijamii ikiwamo maji, afya, elimu, miundombinu mbalimbali na maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni.

# Mil. 65/- kuimarisha zao la karafuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema kuwa imepanga kutumia Sh. milioni 65 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa zao la karafuu.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, wakati akijibu swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid.

Alitaka kujua serikali imepanga kutumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kuimarisha zao la karafuu. Alisema kwa sasa kiasi cha Sh. milioni 50 kimekwishatolewa kwa ajili ya ulinzi wa zao hilo.

Alieleza kuwa serikali kupitia Shirika lake la Biashara la Taifa (ZSTC), imetoa elimu kwa wananchi kuhusu ubaya wa kuchanganya makonyo na karafuu. Alisema inaonekana kwamba kuna watu wamekuwa wakaidi na hawataki kusikia licha ya elimu inayotolewa kuhusu kutochanganya karafuu na makonyo na hali hiyo inasababisha kushusha kiwango cha karafuu.

"Kwa vile serikali imekuwa ikichukua juhudi kubwa kuelimisha watu na bado hawataki kusikia, serikali itamchukulia hatua mtu yeyote atakayepatikana na hatia hiyo kwa mujibu wa kanuni ya 26 ya Sheria ya Maendeleo ya Karafuu," alisema.

Alieleza kuwa mtu yeyote ambaye atachakachua karafuu , ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika.



Mwakilishi wa Viti Maalum Vijana, Viwe Khamis (kulia), akizungumza na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Zanzibar, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Z'bar yakusudia kujenga shule za ghorofa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema malengo ya wizara ni kujenga shule za ghorofa ambazo zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi kwa wakati mmoja.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohamed Said, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua ujenzi wa shule za ghorofa ikiwamo ya Wingwi Pemba kwa kiasi gani utapunguza tatizo la msongamano wa wanafunzi.

Naibu waziri huyo alisema ujenzi wa shule za ghorofa unaofanywa hivi sasa umesaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi ambao umewafanya baadhi ya wanafunzi kusoma huku wamekaa sakafuni.

Alisema Shule ya Sekondari ya Wingwi Pemba, ujenzi wake ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia umeleta unafuu mkubwa na kupunguza wanafunzi kutembea masafa marefu.

Alisema shule sita zilizofunguliwa hivi karibuni katika sherehe za miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimeleta faraja kubwa na matarajio ya wizara ni wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani ya taifa.

"Shule sita zilizofunguliwa hivi karibuni ambazo ni za ghorofa kwa kiasi kikubwa zitapunguza msongamano wa wanafunzi, lakini shule hizo zote zimepatiwa vifaa vya maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi," alisema.

Simai alizipongeza taasisi za fedha za kimataifa Benki ya Dunia pamoja na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) kwa msaada wake katika sekta ya elimu.

Alieleza kuwa BADEA imekubali kujenga jumla ya shule tano za ghorofa Unguja na Pemba, makubaliano ambayo yametiwa saini mwishoni mwaka jana.

# NSSF yaburuza waajiri 34 mahakamani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Arusha, limewafikisha mahakamani waajiri 34, wadaiwa sugu kutoka kampuni mbalimbali mkoani hapa, wakidaiwa kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 7.16.

Akiongea na vyombo vya habari jana, Meneja wa NSSF mkoani hapa, Juma Mwita, amesema kuwa shirika hilo limefikia hatua hiyo baada ya kujiridhisha kuwa kampuni hizo zimeshindwa kuwasilisha michango ya wanachama kwa muda mrefu licha ya hatua ya majadiliano mbalimbali kufanyika.

"Sheria inaelekeza kila mwajiri kuhakikisha anawasilisha michango ya wafanyakazi wake kwa wakati ila kwa baadhi ya waajiri wameshindwa kutii sheria, sisi kama shirika tumeona njia sahihi ni kutumia mahakama," alisema.

Kadhalika, alisema waajiri hao wamesababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi wao licha ya wanachama kuchangia, lakini waajiri wamekuwa wagumu kuwasilisha michango yao jambo ambalo ni ukiukwaji wa sheria.

Alisema kuwa katika kiasi hicho cha fedha baadhi ya waajiri zikiwamo kampuni za ukandarasi, zimeanza kuonyesha nia ya kupunguza madeni na hadi sasa kiasi cha Sh. milioni 400 kimelipwa kati ya Sh. bilioni 7.16 wanazodai. Alizitaja baadhi ya kampuni zinazodaiwa madeni makubwa kuwa ni pamoja na Chuo cha Mount Meru, Kijenge Animal, Pride Tanzania, Tanzania One Mining.

Alisema Shirika la NSSF Mkoa wa Arusha lina zaidi ya kampuni 2,200 yenye wanachama wanaochangia, lakini miongoni mwa kampuni hizo zimeshindwa kuwasilisha michango ya wanachama wao na kufikia deni zaidi ya Sh. bilioni saba.

Mwita aliwaonya baadhi ya waajiri ambao hawawasilishi michango ya wanachama kwa wakati kuwa, watachukuliwa hatua kali kwa kufikishwa mahakamani kwa kuwa wanawanyima haki stahili za wanachama wachangiaji.

Alisema taratibu zinaelekeza kuwa mwajiri asiye wasilisha michango ya wanachama ndani ya miezi sita atachukuliwa hatua kali za kisheria.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Amani, Kata ya Salawe, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga juzi, kwenye sherehe za Maadhimisho ya Miaka 43 ya Kuzaliwa kwa CCM. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Takukuru yaipa angalizo NGS

**Na Happy Severine,** SIMIYU

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Simiyu, imesema kuwa kampuni ya NGS ya mjini Bariadi, ambayo ilikuwa miongoni mwa kampuni zilizonunua pamba mwaka jana, imekuwa na usumbufu kulipa madeni ya wakulima na tozo nyingine.

Kampuni hiyo ambayo inamilikiwa na Mbunge wa Jimbo la Itilima, mkoani humo Njalu Silanga, ilikuwa miongoni mwa kampuni 10 zilizohojiwa na Takukuru na kutakiwa kulipa madeni ya wakulima ndani ya wiki moja.

Kaimu Kamanda wa Takukuru mkoani hapo, Alex Mpemba, alisema hayo wakati wa kukabidhi kiasi cha Sh. milioni 26 za wakulima wa pamba wa Kijiji cha Mwasamba, Wilayani Busega ambazo zilirejeshwa na viongozi wa Amcos baada ya kufanyia matumizi mengine. Mpemba alisema kuwa kampuni nyingine tisa zimetekeleza makubaliano hayo kwa kiwango kikubwa huku baadhi zikimaliza madeni yao kwa wakati ikiwamo kampuni ya NSAGAL Co.Ltd na nyingine ziko kwenye hatua za mwisho.

Alisema kuwa NGS inadaiwa zaidi ya Sh. bilioni tatu yakiwamo madeni ya wakulima, ushuru wa Amcos pamoja na halmashauri, huku wakulima wengi ambao hajalipwa ni kutoka katika jimbo la Itilima ambako mkurugenzi wa kampuni hiyo ni mbunge.

"Hata halmashuari yake inamdai kiasi kikubwa cha pesa, toka tumewekeana hayo makubaliano kampuni hiyo haijaonyesha jitihada zozote za kuanza kulipa deni hilo, wakati wengine wakifanya jitihada za kumaliza madeni yao na wametuletea mrejesho NGS hakuna alichofanya," alisema Mpemba.

Alisema Takukuru itawachukulia hatua kali viongozi wa kampuni hiyo kwa kushindwa kutekeleza makubaliano hayo, huku akibainisha kuwa wameiongezea muda wa siku mbili ihakikishe inalipa deni hilo.

"Tumewasiliana na viongozi wa kampuni, lakini tunaona hawana dalili zozote za kulipa deni hilo, na ndiyo kampuni iliyobaki ikidaiwa deni kubwa sana, tumewapa tena siku mbili walipe deni lote, wakishindwa tutachukua hatua nyingine kali zaidi," alisema Mpemba.

Kaimu kamanda huyo wa Takukuru alisema kuwa taasisi hiyo imefanikisha zaidi ya Sh. milioni 100, pesa mbazo zilikuwa za wakulima kwa ajili ya kulipwa baada ya kutumiwa kwenye matumizi mengine na viongozi wa Amcos.

Katika ulipaji wa pesa hizo, Mrajisi wa vyama vya ushirika mkoa, Ibrahimu Kadudu, aliwataka wakulima kuanza maandalizi mapema ya kufungua akaunti benki, kwa kuwa malipo ya msimu wa mwaka huu yatafanyika kwa njia mfumo wa benki.

# Nyumba salama kuokoa watoto wa kike

**Na Sabato Kasika**

NYUMBA salama huwaokoa watoto wa kike dhidi ya vitendo ya ukeketaji vinavyofanywa na baadhi ya makabila nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania last, Mugumu Serengeti, mkoani Mara, Rhobi Samwelly, kwenye maadhimisho ya kupinga ukeketaji duniani.

Alisema utoaji wa elimu ya kupinga ukeketeji itolewe, lakini kikubwa zaidi ni kujenga nyumba salama ili watoto wa kike wakimbilie huko.

"Shirika letu limeokoa wasichana 1,807 kwa kuwalea katika nyumba salama tunazomiliki ikiwamo ya Suguti na Butiama," alisema Rhobi.

Alisema, serikali na wadau wa kupinga ukatili imejitahidi kutoa elimu, ili jamii iachane na vitendo hiyo, lakini bado vipo, hivyo nyumba salama zitumike kuokoa watoto wa kike.

"Sio kwamba ninapinga elimu, bali ninachoshauri ni kujenga nyumba salama nyingi zaidi kwa kuwa zimekuwa kimbilio la watoto wanaokwepa ukeketaji," alisema.

Naye mwakilishi wa jeshi la polisi kwa upande wa dawati la jinsia, Faidha Suleiman, alisema, ukeketaji ni kosa la jinai.

"Mwaka huu unagawanyika kwa mbili, hivyo tunajua kwamba kwa Mkoa wa Mara kutakuwa na ukeketaji, nasi tumeshajipanga kukabiliana na tukio hilo," alisema Faidha.

Kadhalika, alisema polisi ina mkono mrefu na ina watu wake ndani ya jamii na kwamba ana uhakika wazazi watakaothubutu kukeketa watoto wao, watakumbana na mkondo wa sheria.

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) Tanzania, Jacqueline Mahon, alisema, watoto wa kike wanaokimbia ukeketaji ni wa kupongezwa na kutiwa moyo.

"Hawa wanatakiwa kuwa mabalozi wa kusaidia kupinga vitendo vya ukeketaji katika jamii, hivyo ni muhimu kuwatia moyo kwa uamuzi wa kukimbia ukeketaji nyumbani kwao," alisema Mahon.

HABARI KIMATAIFA

# Mtoto wa siku moja aambukizwa virusi vya ugonjwa wa Corona

**BEIJING, China**

MTOTO mchanga nchini China ameambukizwa virusi vya corona siku moja baada ya kuzaliwa.

Tukio hilo linakuwa la kwanza kuripotiwa tangu kutokea kwa ugonjwa huo ambao umeshaua idadi kubwa ya watu.

Mtoto huyo alizaliwa Februari 2, katika hospitali moja ya mjini Wuhan, nchini China ulio kitovu cha mlipuko wa virusi hivyo.

Mama wa mtoto huyo alikutwa na virusi hivyo kabla ya kujifungua. Haijulikani ni kwa namna gani mtoto huyo aliambukizwa.

Shirika la Habari la China, Xinhua limeripoti taarifa za maambukizi hayo juzi.

Ilieleza kuwa mtoto huyo aliyekuwa na uzito kilogramu 3.25, alikuwa na hali nzuri na alikuwa akifanyiwa uchunguzi. Wataalamu wa afya wanasema inawezekana ni maambukizi yaliyotokea tumboni.

Daktari wa hospitali ya watoto kitengo cha dawa, Zeng Lingkong alieleza kuwa: "Hii inatukumbusha kuwa makini kwamba kuna uwezekano kukawa na maambukizi ya virusi vya corona kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto".

Naye Daktari wa magonjwa ya maambukizi nchini China, Stephen Morse, alisema kuwa kuna uwezekano mtoto huyo aliathirika baada ya kuzaliwa na kuwa karibu na mama yake.

"Inawezekana mtoto alipata maambukizi kwa njia za kawaida kwa kuvuta hewa iliyotoka kwa mama alipokohoa," alisema Morse.

Watoto wachache sana wamegundulika kuwa na virusi vya corona katika mlipuko wa hivi karibuni, sawa tu na aina nyingine ya maradhi ya Sars na Mers.


Ripoti ya jarida la kitabibu nchini China limesema wastani wa umri wa wagonjwa ni kati ya miaka 49 na 56, kwa upande wa watoto ni mara chache kutokea.

Vivyo hivyo, wakati wa mlipuko wa Mers mwaka 2016, Jarida la afya kuhusu maradhi ya watoto lilisema kuwa virusi vilikuwa vikiwaathiri watoto kwa nadra sana, hata hivyo sababu hazijulikani.

Mtoto wa miezi sita nchini Singapore aligundulika kuwa na virusi vya corona, mtoto wa miaka nane aligundulika kuwa na virusi hivyo mjini Wuhan, ambaye kwa sasa yuko Australia.

Virusi hivyo vimesambaa nje ya China, mataifa 25 yakithibitisha kuwa na matukio 191 ya maambukizi, kumeripotiwa vifo viwili pekee nje ya China.

*BBC*



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (kulia) na mkewe Janet Museveni (wapili kulia), wakiwa na Waziri Mkuu wa Israeli, Benjamin Netanyahu (kushoto) na mkewe Sara Netanyahu (wa pili kushoto), ikulu ya Rais Entebbe, Uganda. **PICHA: AFP**

# Kura nne zamwokoa Rais Trump kutumbuliwa

**WASHINGTON, Marekani**

BARAZA la seneti mjini Washington, Marekani limemtakasa Rais Donald Trump, katika kesi ambayo alikuwa akishutumiwa na wabunge wa chama cha Democratic kutumia vibaya madaraka yake.

Katika kura ambazo zilipigwa jana zilifuata msingi wa vyama, na kwamba maseneta 52 walimwondolea hatia Rais Trump dhidi ya 48 waliotaka afukuzwe kazi.

Jaji Mkuu wa Mahakama ya Juu ya Marekani, John Roberts ndiye aliyeyatangaza matokeo hayo.

"Katika shauri hili la mashtaka, maseneta 48 wamesema Rais Donald Trump anayo hatia kwa makosa aliyoshtakiwa, maseneta 52 wamesema hana hatia kwa mashtaka hayo.

Jaji Robert alisema: "Waliomkuta na hatia hawafiki theluthi mbili ya maseneta waliopo. Kwa hiyo Rais Donald John Trump hakukutwa na hatia katika shauri hili la mashtaka".

Rais Trump alikuwa akikabiliwa na shutuma za kutumia vibaya madaraka yake, kwa kumshinikiza Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy kumchunguza makamu wa zamani wa Rais Joe Biden, ambaye anaweza kuwa mpinzani wa Trump katika uchaguzi wa Rais wa Novemba mwaka huu.

Wabunge wa chama cha Republican wanaolidhibiti baraza la seneti walipiga kura 52 kumtakasa Rais Trump, huku mmoja tu, Mitt Romney akijiunga na Wademocrat na kufikisha idadi ya kura 48 zilizotaka atimuliwe kutoka madarakani.

Shitaka la pili dhidi ya Rais Trump lilikuwa kulitatiza baraza la wawakilishi kutekeleza majukumu yake kwa kuwazuia maofisa wa utawala wake kutoa ushahidi mbele ya baraza hilo.

Kuhusu shitaka hilo, Romney alijiunga na Warepublican wenzake na kuwashinda Wademocrat kwa kura 53 dhidi ya 47.

*DW*

## Wakenya kumuaga Moi kuanzia kesho

**NAIROBI, Kenya**

IBADA ya wafu kumkumbuka Rais wa pili wa Kenya, Daniel Arap Moi, aliyefariki dunia wiki hii jijini Nairobi akiwa na umri wa miaka 95, itafanyika wiki ijayo.

Maofisa wa serikali jijini Nairobi wamesema kuwa, siku ya Jumanne wiki ijayo, itakuwa ni siku ya mapumziko, kutoa nafasi kwa raia wa nchi hiyo kuhudhuria ibada hiyo itakayofanyika katika uwanja taifa wa Nyayo, jijini Nairobi.

Katika hatua nyingine, mwili wa Moi utapelekwa katika majengo ya bunge kuanzia siku ya Jumamosi hadi Jumatatu wiki na wananchi watapata fursa ya kumuaga kiongozi wao wa zamani kati ya saa mbili asubuhi na saa 11 alfajiri.

Wakenya wanaendelea na maombolezo ya kitaifa, hadi atakapozikwa kiongozi huyo wa zamani ambaye anakumbukwa kwa mambo mbalimbali aliyoyafanya, waliompenda wakisema, alikuwa kiongozi shupavu, mkarimu aliyehubiri amani na mshikimano nchini humo.

Wakosoaji wa uongozi wake wanasema alikuwa dikteta. Moi aliyeongoza Kenya kwa miaka 24 anatarajiwa kuzikwa wiki ijayo.

**RFI**

## Sudan yatoa ufafanuzi mazungumzo yake na Israeli

**KHARTOUM, Sudan**

BARAZA la Mawaziri la serikali ya mpito ya Sudan, limesema kiongozi wa kijeshi, Jenerali Abdel Fattah al Burhan, hakutoa ahadi zozote kwa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, kuhusu kuanzisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Khartoum msemaji wa serikali, Faisal Mohamed Salih alisema suala la uhusiano Israel sio jukuma la serikali ya mpito kulishughulikia.

Salih alifafanua kuwa Mkuu wa Baraza la mpito alithibitisha kwamba alichukuwa jukumu binafsi na hakushauriana na mtu yoyote na anachukua dhamana yote kuhusiana na suala hilo.

Mkutano wa siri kati ya Jenerali Burhan na Waziri Mkuu Netanyahu mjini Entebbe uliofanyika Februari ulizusha utata mkubwa nchini Sudan, pale waziri mkuu wa Israel alipotangaza kuwa Khartoum itafungiwa ubalozi wake Israeli karibuni.

Kimsingi Israel inaendelea kuwa katika hali ya vita na Sudan ambayo iliunga mkono makundi ya kiislamu yenye itikadi kali chini ya utawala wa Omar Al Bashir aliyepinduliwa mwaka 2019.

**VOA**

# JPM aagiza kupewa majina mahakimu 98

**Na Hellen Mwango**

RAIS Dk. John Magufuli ameagiza kupelekewa majina ya Mahakimu 98 waliopewa hadhi ya kusikiliza kesi 1,132 za Mahakama Kuu ikiwamo za mauaji na kuzitolea uamuzi kwa kusaidia kuondoa mlundikano wa mahabusi gerezani.

Kadhalika amesema katika miaka minne ya uongozi wake, wafungwa 38,801,000 wamepewa msamaha na kusaidia kupunguza mlundikano Magereza.

Rais alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Sheria na Mwaka Mpya wa Mahakama nchini.

Rais Magufuli alisema serikali yake imepambana kuondoa rushwa mahakamani kwa kuboresha kusogeza huduma ikiwamo kufungua kesi mbalimbali kwa njia ya mtandao, kusikiliza kesi kwa njia ya 'video conference' na Mahakama inayotembea.

Alisema pamoja na mambo mengine maboresho hayo yamepunguza matumizi makubwa ya fedha kwa mahakama.

"Mahakimu 98 walipewa mamlaka ya kusikiliza kesi 1,132 za Mahakama Kuu na kuzitolewa hukumu, mheshimiwa Waziri Katiba naomba niletewe majina yao niwe nayapitiapitia, nawashukuru sana mahakama kwa kazi nzuri ya kusikiliza kesi kutoka asilimia 12, 2015 mpaka asilimia tano, 2019 mmefanya kazi nzuri," alisema na kuongeza: "Kuhusu taarifa ya kupokea Sh. bilioni 13.6 na fidia ya Sh. bilioni 30.6 kutoka Mahakama Kuu, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi, Watanzania sasa wana imani na Mahakama, awali walisema wanaokamatwa ni vidagaa tu mapapa yanaachwa wamejionea wenyewe kazi nzuri ya mahakama," alisema.

Kuhusu uanzishwaji wa mahakama hiyo, alisema ulitokana na kukithiri matukio ya uhujumu uchumi na rushwa kwa watumishi.


Alisema jumla ya mahabusi 335 walioomba kukiri makosa yao, wamepata msamaha wa kutoka mahabusu.

Akizungumzia maslahi ya watumishi, alisema kila sekta inalalamika mshahara hautoshi na kwamba hata yeye mwenyewe haumtoshi hivyo watumishi wa mahakama wawe na subira kuhusu maslahi yao.

Kwa upande wa ardhi, rais alisema hana uhakika na mabaraza ya ardhi kama yanafanya vyema na kwamba wenyeviti wa mabaraza hayo wanajifanyia mambo ovyo ovyo, ifike wakati wawe chini ya mahakama.

"Inawezekana tunafanya kosa kuwaacha waendelee tuwalete huku wawe chini ya mahakama, nafahamu baadhi ya wenyeviti wa mabaraza hawafai kwa jamii," alisema Rais Magufuli wakati akiwasuta viongozi hao.

Alisema serikali yake kwa kuanzia itaajiri watumishi wapya 200 kati ya 268 waliohitajika na kwamba itatoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya Mahakama jijini Dodoma. Aliushukuru Ubalozi wa Uingereza na Benki ya Dunia.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi wa Angola nchini Tanzania, Sandro Agostinho De Oliveira, alipofika Ikulu, mjini Zanzibar jana, kwaajili ya kujitambulisha. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Biteko asisitiza mazingira rafiki uwekezaji

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewataka watendaji katika sekta ya madini kwa ngazi zote wakiwamo wananchi wa maeneo ya uwekezaji, kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuongeza fursa za uchumi.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliyasema hayo hivi karibuni wakati akipokea majengo matatu kwa ajili ya serikali za vijiji vya Mdindo, Nahenge na Kisewe, Ulanga mkoani Morogoro yaliyojengwa na Kampuni ya Madini ya Mahenge Resources kwa thamani ya Sh. milioni 51.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri Biteko alisema: "Nikiwa msaidizi wa Rais John Magufuli katika sekta ya madini, ninatoa rai kwa watendaji wote wanaohusika na sekta hii kwa ngazi zote wahakikishe jambo hili linatekelezwa maeneo yao."

Alisema Rais Magufuli ana maono kwamba sekta ya madini itakuwa inachangia asilimia 10 ya pato la taifa ifikapo mwaka 2025 na kwamba hilo litawezekana kama tu wataendelea kuanzisha migodi mipya mikubwa ya kati na midogo.

Biteko alisema ili kufikia ndoto hiyo ni lazima wafanye kazi na wawekezaji kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Waziri Biteko alisema kuwa anaitazama Mahenge Resources kama mradi utakaofungua njia kwa awamu hiyo mpya ya migodi mikubwa na ya kati nchini ambayo itafunguliwa hivi karibuni.

"Ninaamini Kinywe au Graphite itakuwa sehemu muhimu ya ujenzi huu wa mgodi mipya mikubwa. Hii itaifanya Wilaya ya Ulanga na eneo hili la Mahenge litambulike kimataifa kama mzalishaji wa Kinywe bora zaidi duniani.

"Hii itatokana na mahitaji makubwa ya madini ya Kinywe duniani kwa sasa na itafanya Mahenge kuwa sehemu muhimu kwa uwekezaji huu."

Mwenyekiti wa Mahenge, John De Vries ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Black Rock Mining kutoka Australia, alisema wamechangia shughuli za maendeleo maeneo hayo ili kumuunga mkono Rais Magufuli.

"Tupo katika hatua muhimu ya mchakato wa kujenga mgodi, tunawasiliana na benki zenye mitaji mikubwa ili tufanikishe hili na tuweze kukabidhi serikalini asilimia 16 kama mkataba wa madini unavyosema," alisema.

Pia alisema hivi karibuni watalipa fidia kwa wananchi ambao watakumbwa na mradi huo ikiwa ni hatua ya kufuata taratibu za kisheria zilizopo.

## Kanisa lafungiwa madai ya migogoro kuhatarisha amani

**Na Mary Mosha, MOSHI**

SERIKALI wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, imelifunga kwa muda usiojulikana kanisa la Evangelistic Assembles of God lililoko Soweto katika Manispaa ya Moshi kutokana na mgogoro wa miaka 16 unaotishia kuvurugika kwa amani.

Kanisa hilo linafungwa ikiwa zimepita siku tatu tangu Rais John Magufuli kutaka udhaifu uliojitokeza katika matukio ya uendeshaji wa ibada yarekebishwe bila kuzuia shughuli za kidini.

Kauli ya Rais Magufuli iliyotolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ilitokana na vifo vya waumini 20 na kujeruhiwa wengine 16 wakati wa utekelezaji wa imani ya kukanyaga mafuta yaliyodaiwa kuwa na upako katika uwanja wa michezo wa Majengo mjini Moshi.

Tukio la kufungwa kwa kanisa hilo, limetekelezwa na Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro kwa agizo la Mkuu wa Wilaya hiyo, Kippi Warioba, ili kutoa nafasi ya pande zinazosigana kutafuta suluhu ya kudumu, hivyo kuruhusu waumini kuendelea na ibada kanisani hapo.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, Salum Hamduni, alisema jana kuwa hakuna mtu anayeshikiliwa wakati wa utekelezaji wa kufungwa kwa kanisa hilo na kwamba hatua hiyo imelenga kuepusha kutokea kwa vurugu.

Wakielezea chanzo cha mgogoro huo ulioanza mwaka 2004, baadhi ya waumini wa kanisa hilo, Grace Makunzo na Amos Ezekiel, walisema wanapinga kitendo cha makao makuu ya kanisa kumwondoa Mchungaji wao, Frank Mushi, ambaye wanadai ndiye mwanzilishi wa kanisa hilo.

Walisema makao makuu ya kanisa yaliyoko jijini Dodoma, yalitaka mchungaji huyo kwenda kuongeza kiwango cha elimu jambo ambalo halikutekelezwa na mchungaji kwa madai kuwa ni mgonjwa.

"Kitendo cha kumhamisha mchungaji wetu hakijafuata katiba ya kanisa na huu ni uonevu. Tangu tumeanzisha kanisa tulikuwa na Mushi, leo wameona kanisa limekuwa kubwa wanataka kumwondoa, hatukubali," alisema Makunzo.

Waumini ambao nao walimkataa mchungaji mwingine aliyetarajiwa kuletwa na makao makuu ya kanisa hilo wakisema wamejiendeshea ibada bila mchungaji tangu kuondolewa kwa Mchungaji Mushi, Januari 6, mwaka huu.

Aidha, Mchungaji Mushi, ambaye aliondolewa kwa amri ya Mahakama ya Ardhi ya Wilaya ya Moshi katika eneo kanisa, hakupatikana kuzungumzia tukio hilo kwa maeleza ya waumini kwamba anaishi nyumbani kwake Sanya Juu, wilayani Siha.

Dk. Mghwira ambaye alirejea kauli ya Rais alisema bado hajapewa taarifa rasmi katika tukio hilo lakini anaamini ziko sababu za msingi za kufungwa kwa kanisa hilo kama linataka kuhatarisha amani.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**

Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji

**Apige: SImu Namba:**

**0786 641903 au 0716 172929**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

---

**PASSPORT IMEPOTEA**



**SALAMA ALLY MBARAKA**

Anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB 285182** Iliyotolewa tarehe 2 mwezi Julai mwaka 2008 Ofisi ya Idara ya Uhamiaji Dar es Salaam Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.

**Taarifa ya Polisi: MWA/NY/RB/119008/2020**

215619802

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Kuitwa Shaurini Mdaiwa**

**Katika Mahakama ya mwanzo..Dodoma mjini**
**Wilaya ya Dodoma**

**Madai nambari 13/2020**

**Mdai.................................Mariana Casmity Minja**

**Mdaiwa...................................Elda Ernest Hyera**

**Kwa: Elda Ernest Hyera**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta madai yake kwamba : Madai Tshs. 520,000**

Kwahiyo unahitajika kuhudhuria bianfsi katika Mahakama hii siku ya alhamisi 13//02/2020 saa 08:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri Hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohisu shauri Hilo kwa ajili ya kujitetea katika shuri Hilo.

Na Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibisha Kama umepokea kuitwa Shaurini hii, utaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii Leo tarehe 04/2/2020.

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO

115618602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Wilaya ya DODOMA MJINI**

**MADAI 03/2020**
**JOHN KANDAGA MUHANGWA**

**MDAIWA KATARINA HENRY MKAMBA**

**Kwa KATARINA HENRY MKAMBA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**NAMDAI MDAIWA TALAKA**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 17/2/2020 saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 03/01/2020

03/1/2020

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

115618702

---

**JAMUHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Mahakama**

**Usimamizi wa mirathi form II**
**(S.M.M 1984 Nyongeza ya 5 kanuni 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo Dodoma Mjini**

**Usimamizi wa mirathi 11/2020**

**Ombi la KHANIZ SHABANI MOHAMEDkutwuliwa Msimamizi wa Mirathi marehemu SHERUBANU GULAM HUSSEIN**

**Kwa yeyote anauehusika Tanzania Bara.**

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/2/2019. Kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/02/2020.

PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

215618902

---

**TAARIFA YA KUTAFUTWA**

Ndugu Celcius **Eugen Ulanda.** Anatafutwa na Lenard Mihayo Mabula kwa ajili ya kuja kufanya marekebisho ya mkataba wa mauziano ya kiwanja: Plot No,14 Block A Kiegeya Manispaa ya Morogoro. Maamuzi haya yamefanyika baada ya ndugu Mabula Kumtafuta kwa muda mrefu bila mafanikio.Taarifa hizi zimetolewa kwa Umma.Ndugu Ulanda Upatapo taarifa hizi tafadhali fika ofisi za ardhi Morogoro au wasiliana na ndugu Lenard Mabula simu: 0713 295968.

Anaomba tangazo lake litolewe kesho bila kukosa kwenye gazeti la nipashe

115619002

---

**WANATAFUTWA**

**Watoto wa Marehemu Michael G. Mwakapusya**

Aliyefariki mwezi wa nne mwaka 2012 mjini Dar es Salaam wanatafutwa na Baba yao mkubwa anayeitwa Joshua G. Mwakapusya ambaye yupo Dar es Salaam, Tanzania namba yake ya simu ni

**0689 654712/0756 008917 au 0717 962127**

115618802

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI**
**(SURA 334)**
**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI**

HATI NAMBA : 2841 - DLR
MMILIKAJI : ENOCK MWAKANTOBE OF P.O. BOX 156 MBEYA.
ARDHI : L.O. NO.58545,Kiwanja Na.245,Kitalu 'U', Industrial Area,Mbeya Mjini.
ENEO : Meta za Mraba,2761.

TAARIFA IMETOLEWA Kwamba hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Hati ya asili ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati Msaidizi Mkuu,S.L.P.2984,Mbeya.

S.I.Diombanya
MSAJILI WA HATI MSAIDIZI
KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI- MBEYA.

215619702

---

**RE;THE LAND ACT NO 4 OF 1999**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF REF NO;MMC/LD/12919**
**REGISTERED OWNER; TABIA SAIDI KUSENGE**
**LAND; PLOT NO. 582 BLOCK 'BB' KIWANJA CHA NDEGE**
**MOROGORO MUNICIPALITY**

APLICANT;TABIA SAIDI KUSENGE

TAKE NOTICE that the ORIGINAL LETTER OF OFFER to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days(30) from the date of this pubication.

THE ORIGINAL LETTER OF OFFER is found,should be delivered to the office of the ;Municipal Director,Morogoro Municipal Council.P.o box 166 Moro

For: - MUNICIPAL DIRECTOR
MOROGORO

215619302

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie***

***0782253676***

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# JORGINHO

## ATAJWA KUMFUATA SARRI

**LONDON, England**

WAKALA wa Jorginho amebainisha kuwa mteja wake anaweza kuondoka Chelsea mwishoni mwa msimu huu na kuna uwezekano wa kuungana na kocha Maurizio Sarri pale Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia, Jorginho alijiunga na Chelsea mwaka 2018, baada ya Sarri kutua hapo Stamford Bridge akitokea Napoli.

Alikuwa mchezaji nguzo chini ya kocha huyo raia wa Italia, akianza katika mechi 37 za Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza kwenye ligi hiyo.

Kiungo huyo pia amekuwa akicheza mara kwa mara chini ya Frank Lampard msimu huu, akifunga mabao manne kwenye mechi za ligi 23 hadi sasa.

Hata hivyo, mwakilishi wake, Joao Santos, anatarajia ofa za mchezaji huyo wakati wa dirisha lijalo la usajili, licha ya kuwa bado amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa.

"Kwanini siyo?" Santos aliuambia mtandao wa Tuttomercatoweb alipoulizwa kama Jorginho anaweza kuondoka Chelsea.

"Nina uhakika kuna ofa zitakuja, ambapo zitachambuliwa kwa pamoja na Chelsea."

Hata hivyo, Santos alibainisha wazi kwamba kipaumbele cha Jorginho kwa sasa ni kuiwakilisha Italia kwenye michuano ya Euro 2020.

## Reus aipa pigo Dortmund

**DORTMUND, Ujerumani**

MARCO Reus atakuwa nje ya dimba kwa angalau wiki nne baada ya kuumia nyama za paja wakati Borussia Dortmund ikifungwa na Werder Bremen kwenye mchezo wa Kombe la DFB-Pokal, Jumanne.

Kikosi hicho cha kocha, Lucien Favre kilichapwa 3-2 na wanaojikongoja hao kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wakati Reus akilazimika kutolewa nje baada ya kupata maumivu hayo.

Dortmund waliandika kwenye ukurasa wao wa Twitter Jumatano kwamba nahodha wao hatakuwa fiti hadi mwezi ujao, akikosa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora dhidi ya Paris Saint-Germain utakaopigwa Februari 18, mwaka huu.

"Nahodha Marco Reus aliumia nyama za paja kwenye mchezo wa DFB-Pokal," twitter ya Dortmund ilisomeka.

"Kutokana na hali halisi ilivyo kwa sasa, hataweza tena kurudi kwenye mazoezi ndani ya wiki nne zijazo."

Kiungo huyo ataukosa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora, lakini anaweza kuwapo kwenye mchezo wa pili utakaopigwa jijini Paris, Machi 11, mwaka huu.

## Ighalo: Nilikubali kukatwa mshahara nitue United

**MANCHESTER, England**

ODION Ighalo alikuwa na furaha kukatwa mshahara wake ili kuharakisha uhamisho wake wa mkopo siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili mdogo, ili kutua Manchester United.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, Ighalo alijiunga na United kwa mkopo akitokea Shanghai Shenhua hadi mwishoni mwa msimu huu, akiwa amerudi kwenye Ligi Kuu England ambapo awali alicheza pale Watford.

Ingawa mpango wa United kumtaka Ighalo ulikuja dakika za mwisho, mchezaji huyo alisisitiza hakusita kukubali kukatwa mshahara ili kujiunga na klabu iliyokuwa ikimvutia zaidi.

Aliiambia MUTV: "Kutoka saa 11 alfajiri kulikuwa na makaratasi ya kukubaliana kuhusu mkataba wa mkopo. Nilimwambia wakala wangu sijali kuhusu kukatwa mshahara nitachotaka ni kwenda Manchester United."

Ighalo anaweza kupata nafasi zaidi ya kucheza pale Old Trafford katika safu ya ushambuliaji baada ya kuumia kwa Marcus Rashford.

Aliongeza: "Nina furaha kubwa. Ni kama ndoto imekuwa ya kweli kwangu mimi kuja hapa.

"Watu ambao wananijua mimi, hata kule Nigeria, na hata wakati nikiwa nacheza pale Watford, na wachezaji wenzangu wanajua kwamba ninaipenda Manchester United, na ndio ninayoishabikia."




# GUARDIOLA

## AIONYA BARCA KUHUSU MESSI

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ameweka wazi kuwa Barcelona watahitaji muda wa kujijenga upya wakati Lionel Messi atakapoondoka klabuni hapo, baada ya Real Madrid kujikuta kwenye wakati mgumu alipoondoka Cristiano Ronaldo.

Ronaldo aliondoka Madrid kwenda Juventus Julai mwaka 2018 na miamba hao wa soka la Hispania walikabiliwa na wakati mgumu msimu huo, wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya pekee na wakabadilisha makocha mara tatu, ikiwamo na kurudi tena kwa Zinedine Zidane.

Na sasa kocha wa Manchester City, Guardiola anaona klabu yake ya zamani ya Barca ikielekea kwenye matatizo kama hayo wakati Messi atakapoondoka Camp Nou.

"Haitabiri, wachezaji hawa ndio wanaoleta hamasa kwenye timu," amesema akiliambia gazeti la Post United.


"Wakati Messi atakapoondoka Barca itawachukua muda kuijenga timu hii. Mambo hayatabiriki.

"Wanafunga mabao 40 hadi 50 kwa msimu."

Guardiola baada ya kufurahia mafanikio pale Barcelona, aliondoka na kwenda Bayern Munich kabla ya kujiunga na Manchester.

Akiwa na City ameshinda mara mbili mataji ya Ligi Kuu England.

# BAYERN HAINA HARAKA NA MIKATABA YA NYOTA WAKE



**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI wa soka wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesisitiza hawana haraka ya kuingia kwenye mazungumzo ya mkataba mpya na nyota wao, kwani akili yao kwa sasa ni kufikiria kwanza changamoto iliyopo mbele yao kwenye mashindano.

Bayern ilitinga robo fainali ya Kombe la Ujerumani, DFB-Pokal, baada ya kuifunga Hoffenheim 4-3 juzi Jumatano.

Wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na wanakwenda kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na hilo ndilo wanalolifikiria kwa sasa licha ya wachezaji kama Manuel Neuer, Thomas Muller, Javi Martinez, David Alaba na Thiago Alcantara mikataba yao inamalizika mwakani.

"Kwa muda fulani tutakuwa na muda wa mazungumzo, lakini kwa wiki chache zijazo tutajikita zaidi kwenye mashindano," amesema Salihamidzic akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni muhimu kwa sasa akili yetu ipo kwenye mechi zinazokuja ndani ya wiki zijazo. Huku ndiko tunakokufikiria kwa sasa."

Alipoulizwa kama anahofia klabu nyingine kuwatolea macho nyota wao hao ambao mikataba yao inakaribia kumalizika, Salihamidzic alisema: "Hapana. Kwa uhakika hili huwa linatokea kwa wachezaji wakubwa, lakini tuna uzoefu mzuri wa kujikita kwanza kwenye mashindano na hicho ndio tunachokifanya kwa sasa.

"Lakini kama nilivyosema hapo kabla, tutafanya mazungumzo, wachezaji wanajua kuhusu hilo na hakuna tatizo lolote."

Bayern watarudi kwenye mchezo wa Bundesliga keshokutwa Jumapili wakati watakapocheza na RB Leipzig nyumbani.

# Mourinho: Spurs ilistahili ushindi kwa Southampton

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amesisitiza Tottenham walistahili ushindi dhidi ya Southampton katika mchezo wa marudiano wa Jumatano wa Kombe la FA raundi ya nne, uliomalizika kwa kufunga magoli 3-2,licha ya kuzidiwa kwa ubora na timu hiyo.

Spurs walijikuta wakiwa nyuma kwa mabao 2-1 huku zikiwa zimesalia dakika 18 mpira kumalizika pale kwenye uwanja Tottenham Hotspur kwa mabao ya Shane Long na Danny Ings baada ya Jack Stephens kujifunga.

Hata hivyo, Lucas Moura alifunga bao la kusawazisha kwa shuti la umbali wa yadi 18 na Son Heung-min alifunga la ushindi kwa mkwaju wa penalti dakika ya 87 baada ya kufanyiwa madhambi na golikipa Gunn Angus.

Tottenham sasa itakutana na miamba wenzao kwenye Ligi Kuu England, Norwich City katika raundi inayofuata, lakini Mourinho alibainisha kwamba kikosi chake hakikuwa kwenye ubora wake.

"Lazima niwe mkweli na nasema nafikiri timu bora ipoteza mchezo uwanjani, lakini timu yangu ilishinda ingawa haikuwa kwenye kiwango bora," alisema BT Sport.

"Kuna magumu mengi, kuijenga timu hakukuwa na chaguo la kuibadilisha timu. Timu yangu ilistahili ushindi lakini timu bora ilipoteza."

Mourinho kwenye mchezo huo aliwaanzisha, Dele Alli na Tanguy Ndombele, na kiungo huyo wa England alikuwa nguzo ya Tottenham kupata sare kwa kumtengenezea pasi nzuri Lucas na kufanya matokeo kuwa 2-2.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GREALISH AMEINGIA RASMI SOKONI ULAYA

Saini ya nahodha na kiungo huyo wa Aston Villa inawindwa na Barca, Madrid na United...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inatarajia kukutana na ushindani kutoka kwa Barcelona na Real Madrid katika mbio za kuwania saini ya kiungo na nahodha wa Aston Villa, Jack Grealish baada ya klabu hizo kutangaza nia ya kuhitaji huduma ya nyota huyo.

United imemtaja kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 kuwa mchezaji namba moja inayemhitaji katika usajili wa majira ya joto lakini imejipanga kuchuana na kumshawishi kutua Old Trafford.

Villa ikiwa katika janga la kupambana isishuke daraja, inawafanya vigogo hao wa Hispania kuwa na nafasi ya kumsajili Grealish katika majira ya joto, limeandika gazeti la The Sun.

Ni jukumu la United, ambayo wiki hii iliweka wazi nia yake ya kumtaja nyota huyo ni mchezaji namba moja watakayesaka saini yake badala ya James Maddison, ambaye ameshaweka wazi msimamo wake kwamba hana mpango wa kujiunga na timu nyingine kwa sababu anataka kubakia Leicester.

United itajiweka kwenye nafasi nzuri ya kuwapata nyota inaowahitaji, kama itafanikiwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa sasa iko pointi sita nyuma ya Chelsea iliyoko kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Grealish amekuwa na mchango mkubwa katika kikosi cha Villa msimu huu, akikiongoza kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Carabao baada ya kufunga magoli tisa na kutengeneza nafasi tano za kupachika mabao.

Imekuja baada ya Neil Warnock kuishawishi United kumsajili Grealish, ikiamini kwamba nyota huyo ana uwezo mzuri na anamfananisha na aliyekuwa mkongwe wa klabu hiyo, Eric Cantona.

"Man United iko katika nafasi ya kumsajili, ni suala la wao kulipa fedha sasa na si jambo lingine," aliiambia talkSPORT.

"Nafiriki anaweza kuwa msaada mkubwa kwenye kikosi chao. Nafikiri ameumbwa kwa ajili ya kuonyesha kipaji chake.

"Sitaki kuona anatumika kimakosa, lakini kama unajua na unafikiria kuhusu Cantona na watu wengine kama yeye ambao wamekuwa na vitu kama miujiza. Anastahili kusajiliwa."

## KWA UFUPI

**AUBAMEYANG ATAKIWA BARCA**

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Eric Abidal amesema klabu hiyo itakaribu kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), katika majira ya joto. ***(Mirror)***

**MESSI AITAJA CITY**

MANCHESTER City itakuwa ni chaguo la kwanza kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (32), endapo ataamua kuondoka Barca kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

**TRAORE ANUKIA WOLVES**

WOLVES inajiandaa kuvunja rekodi yake kwa kumsajili winga Mhispania, Adama Traore (24), katika dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. ***(Telegraph)***

**CHELSEA, UNITED VITANI**

CHELSEA na Manchester United zinajiandaa kupambana katika kuwania saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Sun)***

**DEMBELE ANUKIA ENGLAND**

MANCHESTER United na Chelsea zinachuana na kuwania huduma ya mshambuliaji wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Moussa Dembele, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

**ARTETA KUSAJILI VIUNGO**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anataka kusajili viungo wawili pamoja na beki mmoja mapema katika majira ya joto ambapo fainali za Kombe la Euro 2020 zitakuwa zinaendelea. ***(Mail)***

**UNDER AITEGA SPURS**

WINGA wa Roma na Timu ya Taifa ya Uturuki, Cengiz Under (22), anawindwa na Tottenham, lakini imeelezwa kuwa klabu hiyo itafanikiwa kupata saini ya nyota huyo kama itapata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Gunes, via Mail)***

**SANE, CITY HAKIJAELEWEKA**

MANCHESTER City bado inaendelea kupambana kuhakikisha inazuia mchakato wa winga Leroy Sane kuelekea Bayern Munich katika majira ya joto baada ya Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 24 kubadilisha wakala. ***(Telegraph)***

**ADRIAN KUREJEA HISPANIA**

GOLIKIPA wa Liverpool, Mhispania, Adrian, ambaye ana umri wa miaka 33, yuko katika mchakato wa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Real Betis. ***(Mail)***

**CHALOV ANUKIA PALACE**

CRYSTAL Palace inatarajia kufanya tena mchakato wa kuwania saini ya straika wa CSKA Moscow na Timu ya Taifa ya Urusi, Fyodor Chalov (21), katika kuhakikisha pia inambakisha klabuni hapo kocha wake Roy Hodgson. ***(Star)***

**NOLAN KUREJEA WEST**

NAHODHA wa zamani wa West Ham, Kevin Nolan (37), anatarajia kurejea katika klabu hiyo kama kocha kwenye timu ya kwanza. ***(Sun)***

**UNITED, CITY VITANI**

MANCHESTER City na Manchester United zote zimeonyesha nia ya kusaka saini ya kiungo wa Birmingham City, Jude Bellingham, ambaye ana umri wa miaka 16 na ni raia wa England. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# REFA SIMBA, NAMUNGO AFUNGIWA MIAKA MITATU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imemfungia mwamuzi msaidizi namba mbili, Kassim Safisha, miaka mitatu kwa kosa la kushindwa kutafsiri sheria ya kuotea, imeelezwa.

Uamuzi huo umetolewa na kikao cha kamati hiyo kilichokutana Februari 03, mwaka huu na kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya mechi za Ligi Kuu Bara na Ligi Daraja la Kwanza.

Safisha alishindwa kutafsiri kwa usahihi na kuruhusu bao lililofungwa na John Bocco wakati Simba ilipowakaribisha Namungo FC, Januari 29, mwaka huu, mchezo huo kumalizika kwa mabingwa watetezi kupata ushindi wa magoli 3-2.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema adhabu hiyo imetolewa kwa mujibu wa Kanuni namba 39(1)(a) ya Ligi Kuu kuhusu Udhibiti wa Waamuzi.

Ndimbo alisema pia kamati hiyo imemwandikia barua ya kuombwa kufanya kwa umakini majukumu kwa mwamuzi, Meshack Suda, ambaye alichezesha mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya Azam FC dhidi ya Mtibwa Sugar ambayo ilichezwa Januari 3, mwaka huu na kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Alisema pia aliyekuwa Kamishina wa mchezo huo, Abdallah Zongo ameondolewa kwenye orodha ya makamisaa kwa kosa la kutoa taarifa yenye upungufu na adhabu hiyo ni kwa mujibu wa Kanuni namba 40 (1) kuhusu Udhibiti Kamishina.

Aliongeza kuwa kamati hiyo imempeleka katika Kamati ya Nidhamu ya TFF, Kiongozi wa Friends Rangers inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, Heri Chibakasa, kwa kosa la kupigana na mashabiki wa timu pinzani huku mwamuzi aliyechezesha mechi ya Ligi Daraja la Pili kati ya Dar City Fc dhidi ya African Sports, Salum Mkole, amefungiwa miezi mitatu kwa kosa la kuonyesha udhaifu katika usahihi wa kutoa kadi.

Aliongeza kuwa mchezaji wa African Sports ya jijini Tanga, Rajabu Kipango amepelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu kwa kosa la kumpiga mchezaji wa Dar City FC katika mchezo huo uliochezwa Februari Mosi mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume, Ilala jijini.



Wachezaji wa Yanga, wakishangilia pamoja na meneja vifaa wa timu hiyo (katikati) baada ya kupata bao la pili dhidi ya Lipuli FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Zanzibar yajipanga kuendeleza vijana

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeandaa mikakati maalum ya kukuza na kuendeleza soka la vijana kwa ajili ya kufikia malengo ya mafanikio.

Imeelezwa kuwa mpango huo utakuwa ni wa kudumu kwa ajili ya kuwaandaa nyota wake kucheza soka la ushindani.

Akizunguma na gazeti hili jana, Kaimu Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana, Mohammed Seif King, alisema mkakati huo utalenga kuwa na timu za Taifa za vijana za zitakazokuwa na umri tofauti na wachezaji wake watakuwa wanakutana kufanya mazoezi kwa pamoja.

King alisema mkakati huo utasaidia kuandaa mapema kikosi kitakachoiwakilisha Zanzibar katika mashindano yanayoandaliwa na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) na uamuzi huu utawafanya wachezaji kuwa tayari kushindana na changamoto mbalimbali.

"Timu ya vijana ya Zanzibar inashiriki mashindano ya Cecafa tu, hakuna mashindano mengine ambayo Zanzibar inasimama kama nchi, hii inapelekea hata vijana wenyewe kubweteka na hata kutochukulia mpira ni kazi kama kazi nyingine, hivyo mpango huu wa kuwa na timu za Taifa za kudumu, utapelekea kuwatoa vijana katika mawazo hayo," alisema King.

Aliongeza kuwa programu hiyo itasaidia vijana wenye uwezo kuteuliwa kirahisi katika timu za Taifa za Tanzania kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

## Kocha Prisons alia na mabeki

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kuendelea kupata sare mfululizo katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Bara zinazoendelea, Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Mohammed Adolph, amesema safu ya ulinzi inawaangusha.

Hata hivyo Adolph alisema ameshaanza kulifanyia kazi tatizo hilo ili kikosi chake kirejee katika ushindani kwenye mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

"Safu yangu ya kati ina matatizo, nakiri tatizo hili limetuumiza katika mechi hizi zilizopita hivi karibuni, nitayafanyia kazi haraka iwezekanavyo," alisema Adolph.

Aliongeza kuwa anaamini wataanza mzunguko wa pili wakiwa tofauti baada ya kurekebisha upungufu waliyokuwa nayo ili kuzoa pointi nyingi katika hatua hiyo ya lala salama.

"Nashukuru wachezaji wangu walifuata maelekezo vizuri tukapata sare, naomba mashabiki wetu wazidi kutusapoti ili tusishuke daraja," Adolph alisema baada ya kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC.

Kocha huyo aliongeza kuwa ushindani katika msimu huu umeongezeka kutokana na timu zote kujiandaa na kujipanga vema.

## Taswa FC, Stanbic uwanjani kesho

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Waandishi wa Habari za Michezo Nchini (Taswa FC), inatarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya kikosi cha Benki ya Stanbic utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Gymkhana, jijini Dar es Salaam.

Mchezo huo utaambatana na hafla fupi ya kufahamiana na kuimarisha uhusiano baina ya wanahabari na wafanyakazi wa benki hiyo.

Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Stanbic, Desideria Mwegelo, alisema wamefikia uamuzi wa kucheza mchezo huo ili kuimarisha uhusiano na wanahabari hao.

"Wanahabari ni sehemu muhimu mno katika jamii, hivyo sisi kama benki ya Stanbic, tumeona kuna umuhimu wa kukutana na hawa wenzetu kupitia tukio hili la mechi ya soka ya kirafiki ili kufahamiana zaidi, kubadilishana mawazo na kuimarisha uhusiano baina yetu," alisema Mwegelo.

Alisema timu yao ipo 'fiti' na inafanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kuwakabili Taswa FC na wanaamini pia utasaidia kuimarisha afya za wachezaji wa pande zote mbili.

Naye Mwenyekiti wa Taswa FC, Majuto Omary, aliishukuru benki hiyo kwa kuwakumbuka, akiahidi soka maridadi katika mchezo huo.

# Michezo

Ijumaa Februari 7, 2020

Nipashe




## Grealish ameingia rasmi sokoni Ulaya

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Yanga, Yikpe Gislain (katikati), akijaribu kuwatoka mabeki wa Lipuli FC, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda 2-1. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAIPIGIA HESABU KALI JKT

●●● Vinara hao wajipanga kushuka uwanjani kwa tahadhari wakianza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara...

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Simba kikiwa kamili kinatarajia kuanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara kwa kuwakaribisha 'Maafande' wa JKT Tanzania katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi mfululizo wa mechi tano wakati JKT Tanzania wao wametoka kubanwa nyumbani kwa kulazimishwa sare dhidi ya Coastal Union kutoka jijini Tanga.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili timu yake iko tayari na kamili kwa mchezo huo na kuitaja JKT Tanzania ni moja ya timu zenye wachezaji walioimarika na wenye kutoa ushindani kwa klabu pinzani.

Matola alisema wamewaandaa wachezaji wao kupambana katika mechi zote kwa sababu hatua ya lala salama ndio wakati wa kukamilisha 'hesabu' za ubingwa.

Alisema hakuna mechi rahisi na hatuna timu ndogo katika Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo watakuwa makini katika kila mpira watakaokuwa nao wachezaji wake.

"Ni mechi ngumu, hatutarajii kitu kingine, msimu huu na hasa mzunguko huu mambo yatazidi kuwa magumu, kila timu inahitaji kukamilisha malengo yake, bado hakuna ambaye yuko salama, walioko chini wanataka kukimbia na walioko chini yetu wanatukimbiza," Matola alisema.

Nahodha na kiungo huyo wa zamani wa Supersport ya Afrika Kusini alisema wanahitaji kuendeleza matokeo mazuri katika kila mechi ili watangaze ubingwa mapema.

"Hatutaki presha huko mbele, ukifanikiwa kushinda mechi nyingine tano za mzunguko wa kwanza, unakuwa nafasi salama, dua na mipango yetu ni kutoangusha pointi katika mechi hizi za nyumbani, tumejiandaa kukabiliana na kila ushindani," alisema Matola.

Naye Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema wachezaji wote wapo salama na wanaendelea kujipanga kwa ajili ya mechi hiyo ya leo.

"Tuliendelea na mazoezi kama kawaida, kama unavyojua kwa sasa huwezi kufanya mazoezi magumu, mwalimu huangalia na kuwapa mbinu zake za kiufundi baada ya kurekebisha makosa ya mchezo uliopita, tuko vizuri, tunaamini tuna nafasi ya kupata pointi tatu nyingine," alisema Rweyemamu.

Aliongeza kuwa nyota wao wawili, Shiza Kichuya pamoja na Luis Miquissone, tayari wamepata ITC na uwezekano wa kuonekana uwanjani leo utatokana na uamuzi wa Kocha Mkuu Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Baada ya mechi ya leo, Simba itasafiri kwenda Morogoro kuwafuata Mtibwa Sugar katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa Jumanne na Februari 15, mwaka huu watakuwa ugenini Iringa kuwakabili Lipuli FC kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani humo.

## Eymael: Yanga itapanda kileleni

**Na Mwandishi Wetu**

TUMEJIPANGA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, ambaye ameanza kukibadilisha kikosi hicho ambacho kiko kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20.

Akizungumza na gazeti hili jana, Eymael alisema licha ya changamoto mbalimbali zinazowakabili wachezaji na klabu zinazoshiriki ligi hiyo, bado ushindani unatakiwa kuongezeka kwa faida ya maendeleo ya soka hapa nchini.

Eymael alisema anaamini Yanga itaonyesha soka la 'ufundi' , kisasa na kurejesha heshima yake ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ya juu kwa Tanzania Bara.

"Timu imeanza kuwa na mwelekeo, itabadilika na kufika mahali ninapopataka, ni vigumu wachezaji kubadilika kwa wiki mbili au tatu, lakini tayari kuna mabadiliko yanaonekana kwenye kikosi na wachezaji mmoja mmoja, nafikiri tutafikia malengo, nafasi yetu si mbaya," alisema Eymael.

Aliongeza ushindani kwenye ligi utasaidia kuwajenga wachezaji na baadaye kikosi cha Taifa kitakuwa na wachezaji bora na imara kwa ajili ya kupambana na wenzao wa mataifa mengine.

"Nimegundua ushindani uko katika baadhi ya mechi, ni wazi mechi hizo ni chache, lakini ili uwe na timu ya taifa bora, ni lazima uwe na ligi yenye ushindani na imara, nimetazama ligi ya hapa kuna matatizo ambayo yanapaswa yafanyiwe kazi, kuanzia waamuzi na wachezaji, kuna vitu vinahitaji kufanyiwa mabadiliko," Eymael aliongeza.

"Timu nyingi zinacheza vizuri lakini si kwa kiwango ambacho kinatakiwa, ni lazima ligi iwe ya ushindani katika mechi zote, ligi ikiwa imara kutakuwa na timu bora ya taifa,".

Mbeligiji huyo anayesaidiwa na Boniface 'Masters' Mkwasa, alitua Yanga kuchukua mikoba iliyoachwa na Mkongomani Mwinyi Zahera.

Kikosi cha Yanga jana kiliendelea na mazoezi yake kwa ajili ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa kesho katika Uwanja wa Taifa jijini na baada ya hapo itaendelea kubaki Dar es Salaam kuwakaribisha Mbeya City hapo Jumanne.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >